ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	- Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Nne – Tarehe 24 Januari, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda, Masoko na Utalii: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uendelezaji, Ukuzaji na Uwekaji wa Viwango na Ubora wa Bidhaa na Usimamizi wa Huduma zinazolingana na hizo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamwita anayefuata naomba turekebishe *order paper* yetu kidogo. Kwa mujibu wa kanuni ambazo wiki iliyopita tulizifanyia marekebisho makubwa na tukakubaliana kwamba Kamati ya Fedha na Uchumi sasa iitwe Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Ni mazoea tu na utamu wa jina hilo la Kamati ya Fedha na Uchumi ilivyokuwa watendaji wetu wamekosea na wakaiita Kamati ya Fedha na Uchumi.

Kwa hiyo, hapo penye Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi iwe Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Halikadhalika katika hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha tuondoe ile na Uchumi na tutie Biashara na Kilimo.

Baada ya marekebisho hayo Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo juu ya Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uendelezaji, Ukuzaji na Uwekaji wa Viwango na Ubora wa Bidhaa na Usimamizi wa Huduma zinazolingana na hizo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Nam. 70

Ushiriki wa Watendaji wa Baraza katika Vikao vya Bunge la Afrika Mashariki

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Aliuliza:

Kwa kawaida Bunge la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki linapofanya kazi zake, huwashirikisha watendaji wa Mabunge na Mabaraza mbali mbali ya Wawakilishi katika nchi wanachama ili waweze kupata uzoefu na kuongeza ufahamu wa utendaji wa utumishi katika Mabunge ya nchi zao.

(a) Je, Mhe. Waziri, unafahamu kwamba watendaji wa Baraza letu la Wawakilishi nao pia wana haki ya kushiriki katika vikao vya Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki kama watendaji wa Mabunge mengine.

(b) Je, ni lini watendaji hao waliwahi kushiriki katika vikao ama shughuli za Bunge hilo.

(c) Je, Wizara ina mkakati gani kuhakikisha kwamba watendaji wetu pia wanashiriki katika vikao na shughuli nyengine za Bunge la Afrika Mashariki.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 70 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki linapofanya kazi zake huwashirikisha watendaji wa Mabunge na Mabaraza ya Wawakilishi katika nchi wanachama ili waweze kupata uzoefu na kuongeza ufahamu wa utendaji na utumishi katika Mabunge ya nchi zao. Lakini pia Bunge hili huwa na kawaida ya kufanya vikao vyake katika nchi wanachama ili kukuza uhusiano mzuri baina ya nchi hizo na kuwawezesha na kuwawezesha Waheshimiwa Wajumbe na watendaji wa Mabunge husika kupata uzoefu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 70.

Mhe. Spika,

(a) Nafahamu kwamba watendaji wa Baraza la Wawakilishi nao pia wana haki ya kushiriki katika vikao vya Bunge la

Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa ajili ya kujifunza na kubadilisha uzoefu kama ilivyo kwa watendaji wa Mabunge mengine ya nchi wanachama. Watendaji wetu wamekuwa wakipata fursa hiyo ya kushiriki katika vikao mbali mbali vya Jumuiya.

(b) Katika miaka ya nyuma kabla ya mwaka 2005 baadhi ya Makatibu Mezani wa Baraza la Wawakilishi walikuwa wakipata fursa ya kushiriki kwenye vikao vya Bunge la Afrika Mashariki. Aidha, kwa kupitia mialiko mbali mbali inayotolewa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Katibu wa Baraza na watendaji wengine wa Baraza wanashiriki katika semina na mialiko mbali mbali kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya Baraza la Wawakilishi na watendaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vile vile watendaji wa Baraza la Wawakilishi walipata fursa ya kushiriki na kutoa huduma mbali mbali katika Mkutano wa Nne wa Bunge la sasa la Afrika Mashariki uliofanyika hapa Zanzibar kuanzia tarehe 3 Disemba, 2007 hadi 14 Disemba, 2007.

(c) Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais itaendelea kuchukua juhudi mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha mashirikiano na Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuhakikisha kwamba tunapata nafasi nyingi zaidi kwa madhumuni ya kuongeza idadi ya watendaji wa Baraza la Wawakilishi kushiriki katika vikao na shughuli nyengine za Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe naarifiwa kuna matatizo kidogo ya mitambo ambayo kiutaratibu ni sawa sawa na kama pale umeme unapozimwa mitambo ikiwa haifanyi kazi. Sasa sina hakika kama ni zote au vipi. Lakini hebu Katibu nitafutie taarifa huko kama hali ikoje. Maana utaratibu wajumbe wazungumzie kwenye mic hizi, kama hawazungumzi kwenye mic hizi basi haiingii kwenye hansard na hiyo maana yake mawasiliano kiutaratibu hayapo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, hii ndio raha ya kuwa na kiongozi mwenye busara.

Nam. 77

Ujenzi wa Bustani ya Jamhuri na Kwa Mchina

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Baada ya Serikali kuamua kufanya ujenzi na matengenezo makubwa ya Bustani ya Forodhani, Taasisi za Umma na Watu binafsi zimeanza kushawishika na kuona kuwa kuna umuhimu wa kuweka mazingira bora ya kuchezea watoto na mapumziko kwa watu wazima. Kwa msingi huo, ziliimarishwa Bustani ya Jamhuri (Jamhuri Garden) na bustani ndogo ilioko eneo la Kwa Mchina mwisho (Mini Foro Garden) ambazo zimekuwa ni vivutio vikubwa kwa umma hapa Zanzibar na vyanzo vizuri vya mapato.

(a) Je, Mhe. Waziri ni taasisi gani iliyotengeneza Bustani ya Jamhuri (Jamhuri Garden).

(b) Watoto na watu wazima wanapoingia kwenye eneo la michezo la Bustani ya Jamhuri hutozwa fedha zisizopungua Tsh. 1,000/= kwa mtu mmoja. Je, fedha hizo hupatikana kiasi gani kwa mwezi na huingia katika mfuko gani wa Serikali.

(c) Napongeza sana mandhari na huduma zitolewazo eneo la Bustani ya Kwa Mchina *(Mini Foro Garden)*. Je, Mhe. Waziri katika eneo hilo Serikali huchukua kodi ya kiasi gani na kwa utaratibu upi.

(d) Kwa kuwa watu binafsi tayari nao wameshajiishika na kuamua kuanzisha maeneo ya michezo kwa watoto. Je, ni lini Serikali kupitia Mikoa na Wilaya itaamua kuweka maeneo kama ya Kwa Mchina kwa ajili ya mapumziko kwa watoto wetu na kujiongezea mapato.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.77 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Katika kuimarisha mazingira ya Mji wa Zanzibar na kuuweka katika hali ya kuvutia, Baraza la Manispaa linaendelea na juhudi zake mbali mbali za kuzifufua bustani zilizo chini ya mamlaka yake. Katika lengo hilo, Baraza la Manispaa linatekeleza azma hii kwa njia mbili. Aidha, kwa kutumia wao

wenyewe au kwa kushirikiana na sekta binafsi au kwa mashirika. Kwa kuanzia bustani ambazo zimeimarishwa ni pamoja na Mnazimmoja karibu na Makumbusho, Kiembesamaki (kwa Sheikh Al – Youseif), Forodhani, Jamhuri Garden na Mini Foro Garden.

Mhe. Spika, baada ya majibu hayo ya utangulizi sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 77 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika,

(a) Bustani ya Jamhuri imetengenezwa kwa ubia wa makubaliano ya Tengeneza, Endesha, Rudisha (Build, Operate, Transfer) kati ya Baraza la Manispaa na mfanyabiashara mzalendo (Bi. Asya Mohammed Bafadhili) kwa kuimarisha sehemu za kuchezea watoto, usambazaji wa maji, uwekaji wa taa za umeme na uwekaji wa uzio. Kwa upande wa Baraza la Manispaa imeshughulikia ukataji majani, uungaji umeme, uwekaji vyombo vya kuhifadhia taka na matengenezo ya njia za waendao kwa miguu pembezoni mwa njia kuu.

(b) Makusanyo ya fedha za kiingilio hukusanywa na mkodishwaji na baadae huilipa Baraza la Manispaa kwa mujibu wa mkataba Tzs. 1,000,000/=. Kati ya fedha hizo mkodishwaji anajilipa asilimia 90 ya kodi hadi atakaporudisha gharama zake za ujenzi.

(c) Eneo la Bustani ya Kwa Mchina (Mini Foro Garden) ni eneo linalosimamiwa na mtu binafsi. Eneo hilo kwa ukweli hapo mwanzo ilikuwa ni mafichio ya wavuta unga na wavuta bangi pale. Sasa huyo mtu binafsi yeye aliliomba katika Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi na akapatiwa kwa njia ya kuliendeleza. Katika utaratibu wa ukusanyaji wa mapato Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi hukusanya kodi ya leseni kwa mwaka ambayo Tzs. 150,000 na Tzs 6,000 kama ada ya ukusanyaji taka kwa kila mwezi.

(d) Mipango imeanza kupitia Serikali za Mikoa na Serikali za Mitaa kutenga maeneo ya kuchezea watoto kwa mujibu wa mipango miji iliopo. Changamoto kubwa iliopo ni kwamba sisi kama serikali hatuna budi kusimamia pamoja na kushirikiana na Serikali hizo za Mitaa na Mikoa kuona kwamba maeneo matupu yaliyotengwa hasa kwa kuweka bustani na michezo kwa vijana

wetu tunayaimarisha, tunayatunza na kuyabakisha kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika: Kabla Mhe. Hija Hassan Hija hujauliza swali nimepewa taarifa na mafundi wetu mitambo kwamba kinachohitajika kwa Mhe. Mjumbe ni kusimama. Kwa kuwa huku mimi nataja jina basi majina haya yamekuwa *computerized* kule kwenye *control room*. Kwa hiyo, hatuna haja ya kubonyeza bali ni kusimama na lile jina wanapolipata basi moja kwa moja wanakupa mawasiliano kutoka hapo hapo ulipo bila ya kubonyeza. (Makofi)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa amekiri kwamba eneo la Jamhuri Garden sasa anakodishwa Bi. Asya Mohammed Bafadhili kwa ubia. Kwa kuwa malengo ya mzee wetu Marehemu Abeid Amani Karume yalikuwa ni kuwapatia watoto wetu wa Kizanzibari maeneo ya kucheza bila ya malipo.

(a) Je, tuseme kwamba utaratibu wa malengo ya Mapinduzi ya Zanzibar sasa unakiukwa.

(b) Hivyo mapato ya Tsh. 1,000,000 kwa eneo kama lile ambalo liko katika mji na linaingiza fedha nyingi. Nyinyi kama Serikali mnaridhika nalo au ni upotevu wa mali ya serikali.

(c) Utaratibu wa kutoa maeneo ya serikali hutegemea tenda kwa maana ya *three quotation.* Je, unaweza ukanambia kwamba Bi. Asya Mohammed Bafadhili alikuwa na wenzake wangapi walioshindana katika tenda ile.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakubaliana kabisa na Mhe. Hija Hassan Hija kwamba malengo ya awali yaliyowekwa na mzee wetu muasisi wa taifa hili ni kuwapatia burudani vijana katika sehemu hizo bila ya malipo. Lakini lazima tukubali kwamba malengo yale inabidi kila baada ya muda twende na wakati kutokana na gharama ambazo zinahitajika kuyatengeneza, kuyatunza na kuyaendeleza.

Nafikiri Mhe. Hija Hassan Hija utakumbuka pembea zilizokuwepo Rahaleo pale wakati huo wa zamani ilikuwa pembea za aliakweche tu moja kwa moja hamna hata kupita kwa treni, hamna lifti, hamna vyenginevyo sasa vyote hivyo vinahitaji mapesa.

Mhe. Spika, lazima tukubali kutokana na mambo mengi ambayo serikali imekabiliana nayo tumeona ni jambo jema kuikaribisha sekta binafsi kusaidiana nayo katika shughuli hizi.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija alizungumzia juu ya mapato yanayoingia pale. Lazima tukiri kwamba utaratibu huu wa kujenga kwa kutumia *Build, Operate, Transfer (BOT)* mara nyingi ni ghali lakini inategemea zaidi na makubaliano yaliyopo kati ya mwenye mali na huyu anayekuja kutusaidia ujenzi.

Sasa sisi mkataba tulioukuta ni huu lakini kama serikali tuna wajibu wa ku-*review* na kuupitia tena kila mara kadri ya miaka inavyokwenda. Kwa hiyo, nakuahidi Mhe. Hija Hassan Hija kwamba tutakaa chini kuupitia mkataba unasemaje na vipengele na tuone kwamba mwekezaji anapata chake na serikali inapata kodi inazostahiki kama ipasavyo.

Lakini swali (c) kuhusu tenda. Mhe. Spika, mimi sikuwepo wizara hii kabla ya hapo yaani hii ya section ya Tawala za Mikoa na Baraza la Manispaa. Lakini ninachotaka kusema kwa suala hili zile bustani sote tukumbuke zilikuwaje. Bustani zile kwa kweli kama Jamhuri Garden nakubali walikuwa wanasoma watoto nyakati za mchana, lakini ukenda jioni pale ni hatari kubwa. Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi jana nilikwenda makusudi hasa mchana na usiku, basi ule upande ambao haujaendelezwa maana yake kila aina ya vitendo vibovu viko pale na pamekuwa *nicknamed guest houses.*

Sasa kupaacha vile pakafanywa mambo yaliyokuwa hayana maana haitusaidii. Kwa kweli ile bustani yule mama kafanya kazi nzuri sana ya kupigiwa mfano kabisa. Maana yake watoto wanakwenda tena kwa wingi, pana amani na utulivu, pana biashara. Mhe. Spika, si hapo tu, hata Mini Foro Garden kama una harusi yako, una karamu yako unataka kwenda kule mwenyewe utafurahi.

Kwa hiyo, mimi ninachoshauri tuwa-encourage watu kama hawa wajitokeze kadri pahala pana open space pana bustani nzuri iendelezwe kwa manufaa ya watoto wetu.

Mhe. Spika: Naona maelekezo ya mafundi mitambo yamekuwa yana tofauti kidogo. Kwa hiyo, nimeona nisimame ili nibadilishe usemi wa kwanza ule kufuatia taarifa mpya niliyopata.

Wanachosema mafundi wetu ni kwamba Mheshimiwa anapotajwa au anapotaka kuomba nafasi basi ni kiasi cha kusimama pale alipo, abonyeze

mara moja. Mwanzo niliambiwa kwamba asibonyeze kabisa asimame tu, lakini abonyeze mara moja ili kule ita-*detect* kwamba kuna maombi, sio abonyeze mara nyingi nyingi. Kwa hiyo, abonyeze mara moja aachie asubiri majibu ya maombi aliyoyatoa. Akibonyeza ndio maana yake anaomba kule wakati huku tayari ruhusa imeshatoka na kule sasa fundi mitambo anamuunganisha. Nafikiri tumekubaliana na tumefahamu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nashukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri kampongeza sana mwekezaji huyu aliyejenga bustani hii na mimi pia nampongeza sana kwa juhudi yake kubwa aliyoifanya kupaweka pale pahala pakawa na mandhari mazuri.

Lakini kwa kuwa nchi yetu ina matumizi madogo watu wetu wengi ni wanyonge. Kwa kuwa mwekezaji ameweka ada ya kiingilio katika bustani ile shilingi elfu moja kwa mtoto na mtu mzima. Kwa kuwa serikali ndie msimamizi wa wafanyabiashara.

Je, kwa sababu watu wanakwenda kwa wingi haoni kama kuna haja ya kuwapunguzia watu ada. Kama hatopunguza haoni kama anapunguza watoto wengine waliokuwa wanyonge wasiingie katika bustani hiyo na kupata mapumziko na kucheza na watoto wenzao.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, bei iliyowekwa pale yaani gate fee kwendea kwenye yale mapembea yenyewe ni shilingi elfu moja kwa siku za weekend na shilingi mia tano kwa siku za kawaida. Ukenda siku za weekend Mhe. Spika, pakutia mguu hapana, kila mtoto ana hamu aende akapumzike pale.

Zaidi ya hayo vile vivutio vilivyoko ndani kule kama viburudishaji, mapembea niliyoyasema, yote yale hiyo package inclusive kwa kweli kwa hali ilivyo hivi sasa hii ni bei mjarab kabisa hasa ukilinganisha na hizo gharama zake za muda mrefu za kujilipa. Mhe. Spika, nahisi kwa sasa hii bei sio kubwa.

Nam. 10

Uvamizi wa Maeneo ya Kilimo

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Kwa kuwa maeneo mengi yaliyotengwa kwa ajili ya kilimo yamevamiwa na kujengwa nyumba za kuishi na hivyo kuathiri maendeleo ya kilimo kwa kiasi kikubwa.

(a) Wizara ina mipango gani katika kukabiliana na tatizo hilo.

(b) Kwa kuzingatia kuwa Zanzibar ni kisiwa chenye ardhi ndogo, Wizara inakusudia kuweka utaratibu gani katika kuhakikisha ardhi hiyo ndogo inatumika vizuri na kwa mujibu wa mipango iliyowekwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika,Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kuzingatia umuhimu wa ardhi kwa uzalishaji wa mazao, inachukua hatua muafaka za kukabiliana na uvamizi wa ardhi ya kilimo.

Mhe. Spika, Wizara yangu pia inashirikiana na taasisi nyengine ikiwemo Serikali za Mikoa, Wilaya, Masheha pamoja na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati katika kuhakikisha kuwa maeneo yenye rutba kwa kilimo yanabakishwa kwa ajili ya kilimo. Tayari kuna makubaliano ya kuwa na kamati ya pamoja kati ya Wizara yangu na ile ya Ardhi ili kusimamia matumizi ya ardhi ya kilimo.

- Kuwaelimisha wananchi kutouza ardhi yenye rutba kwa matumizi mengine yasiyokuwa ya kilimo.

Mhe. Spika, wimbi la uvamizi wa ardhi yenye rutba kwa kilimo umekuwa mkubwa na ni changamoto kubwa kwa sekta ya kilimo. Ardhi inavamiwa kwa matumizi yasiyokuwa ya kilimo hasa zaidi ujenzi wa makaazi ya watu. Uvamizi huu ulikuwa zaidi katika Wilaya ya Magharibi lakini sasa umetambaa hadi katika Wilaya nyengine.

Mhe. Spika, kwa upande wa mashamba ya Serikali yaliyo chini ya Wizara ya Kilimo, Wizara imekamilisha zoezi la kuyaorodhesha

mashamba yote na sasa kazi itakayofuata ni kuyapima na kuyawekea mipaka ili kuyadhibiti vizuri. Mpango huu pia utahusisha mabonde ya mpunga.

(b) Mhe. Spika, mamlaka ya kumiliki na kumilikisha ardhi yote yako chini ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Nidhati na Maji, Wizara ya Kilimo na Maliasili inamiliki baadhi ya mashamba ya serikali tu yaliyo chini ya wizara na vituo vya utatifi. Kwa hivyo, suala la mipango ya matumizi ya ardhi yote inaratibiwa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Nishati na Maji. Wizara yangu ina wajibu wa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Nishati na Maji katika kusimamia matumizi bora ya ardhi na mashirikiano yaliyo karibu yataendelezwa ili kufikia malengo ya nchi yetu.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili naomba nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Sasa hivi heka moja kuchimbua ni Shs. 20,000/- na kuburuga ni Shs.20,000/- jumla inakuwa Shs. 40,000/-. Lakini hivi karibuni bei ya mafuta imepanda. Je, Mhe. Waziri anaweza akawasaidia wananchi ikabakia bei hii hii ili wakaweza kulima kama walivyojipangia?

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, tunaelewa kwamba bei ya mafuta imepanda na tumo kwenye msimu wa kilimo cha mpunga. Pia nimuhakikishie kwamba serikali inataka kutizama kwa upana zaidi namna ya kuwawezesha na kusaidia wakulima wetu waweze kulima, na kilimo hicho kiwe chenye tija kwao wao na nchi yetu kwa jumla. Kwa hivyo, ni suala ambalo linaweza kuzingatiwa na tunaendelea kulizingatia.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, yapo maeneo mengi makubwa ambayo yamezungushiwa uzio hayajengwi nyumba wala hayatumiki kwa kilimo, yamekaa tu. Je, Mhe. Waziri maeneo haya ambayo hayajengwi nyumba wala hayalimwi kwa serikali hii ya umoja wa kitaifa kuna mpango gani wa kuyakomboa maeneo haya ili yaweze kuendeleza shughuli za kilimo ahsante.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa vile umenielekeza, lakini zaidi hili ni la utawala na usimamizi wa ardhi ambalo, sidhani wizara yangu ndio yenye mamlaka ya kulijibu hilo. Lakini naomba maelekezo yako.

Mhe. Spika: Kama sio suala linalohusu wizara yako moja kwa moja, basi nadhani tunaweza tukaliwacha na hasa kwa kuwa hakuainisha lile eneo lenyewe ambalo pengine mlikuwa mnalitumia baadae mkawacha, basi nadhani tungemalizia hapo hapo tu, tunakushukuru Mhe. Waziri.

Nam. 46

Karakana ya Matrekta

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa tumekua tukipiga kelele juu ya hali mbaya na uchakavu wa Karakana ya Matrekta ya Mbweni Unguja na Machomanne Pemba.

(a) Je, Mhe. Waziri, kuna sababu zipi zinazopelekea mtizamo wa Wizara kutoeleweka juu ya hatua zinazostahili kuchukuliwa ili kunusuru hali mbaya ya Karakana zote mbili.

(b) Hivi unafahamu kwamba kitendo cha Wizara kushindwa kuzifanya Karakana kuwa ni Mashirika yanayojitegemea ama Idara kunazifanya ziendelee kupoteza haiba yake.

(c) Katika kuliangalia suala la kilimo na umuhimu wake, Je, Wizara ina mtazamo gani mpya kuhusiana na Karakana hizo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 46 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Waheshimiwa Wawakilishi kwa muda mrefu wamekua wakizungumzia sana kuhusu suala zima la mfumo wa uendeshaji wa karakana hizi mbili ama kuwa Shirika kamili au kuwa Idara. Kwa muda wote huo, Wizara imekua ikitafakari na kutafuta mfumo ambao Karakana hizi zingeweza kujiendesha vizuri kwa manufaa ya sekta ya kilimo.

Mhe. Spika, hatimae Wizara yangu imeona kuwa hapana njia yoyote ile kwa Karakana hizi kujiendesha kibiashara au kama Shirika kamili. Uzoefu kwa kipindi chote ambapo Karakana zilikua zikijiendesha katika mfumo huo wenye utata umejidhihirisha hivyo.

Mhe. Spika, kwa kuona na kutambua umuhimu wa Karakana hizi pamoja na kuzingatia muundo mpya wa sasa hivi, Wizara tumeonelea ni busara kuzifanya

Karakana hizi kuwa Kitengo cha Matrekta (Mechanization) chini ya Idara ya Kilimo.

Mhe. Spika, kwa kufanya hayo kutakuwa na uwezekano mkubwa wa kuzisaidia kifedha kwa kupitia bajeti kuu ya Serikali tafauti na mfumo uliopo ambapo karakana haipati ruzuku yoyote kutoka serikalini.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mafupi yaliyotolewa, lakini tatizo la karakana hili ni kubwa zaidi, kwa kuwa zimekuwa ni za muda mrefu na pia zina umuhimu mkubwa katika suala zima la kuimarisha harakati za matrekta katika wizara ya kilimo.

(a) Mhe. Spika, mimi napenda nimuulize Mhe. Waziri je, tutegemee muda gani karakana zile zitakuwa ni idara au kitengo katika idara ya kilimo.

(b) Kutakuwa na mabadiliko gani ya kuzitononesha yaani kuziendeleza zile karakana ili ziweze kufikia kile kiwango ambacho angalau zilipoanzia, wachilia mbali kuziendeleza, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kama tunavyotambua sote, wizara zote za serikali zimeundwa upya na maelekezo ya kuunda upya idara zetu na maeneo ya vitengo vyetu tumeshapewa. Kwa hivyo, muda ni huu tunaendelea katika kujipanga upya, kwa hivyo muda ni huu ambao tunakwenda nao. Nini tutafanya ili hali iwe nzuri zaidi, ndio tumo katika harakati hizo za kuwapatia zana bora na kuwawezesha ili waweze kuhudumia sekta ya kilimo ipasavyo. Lakini kama tunavyoelewa jambo hilo litaendelea kuwa endelevu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Waziri anasema kwamba baada ya mpango wa serikali kukamilika huwenda matrekta ikawa ni idara au taasisi fulani. Lakini kwa kuwa matrekta wanaongoza kwa kudai hapa Zanzibar, wanawadai watu binafsi na wanaidai Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(a) Je, wakati mnazingatia marekebisho ya eneo hilo, madeni ya matrekta yatazingatiwa.

(b) Kwa sababu dhani ya (BOT) kwa serikali ni nzuri, basi kwa nini musiifanye hii matrekta ikaingia kwenye dhana ya (BOT)?

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, nikuombe Mhe. Mwakilishi arejee sehemu ya pili ya swali lake, sijalisikia vizuri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwa kuwa serikali inaamini kwamba dhana ya (BOT) yaani *Build Operate and Transfer* ni nzuri, kwa nini eneo lile lisiingie huko?

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, bila shaka masuala ya madeni yatazingatiwa na yatapewa umuhimu wake. Sehemu ya pili ya Build Operate and Transfer amesema kwamba anaamini kwamba serikali inaamini kuwa ni mfumo mzuri.

Mhe. Spika, serikali kuamini au kutokuamini kwamba ni mfumo mzuri, siwezi kulijibu hapa, kwa maana hilo ni suala la sera na linataka maelekezo thabiti na mahususi kutoka kwenye serikali yenyewe. Lakini ninachoweza kusema ni kwamba lengo na dhamira ya wizara yangu ni kuhakikisha kwamba karakana hizi zinachukua nafasi yake katika kuihudumia sekta ya kilimo. Yakijitokeza maelezo mahususi ya serikali, bila shaka kuna mengine ambayo tunayoyazingatia sisi na yakitokezea maelekezo ya serikali tutayazingatia na kuyasimamia ipasavyo.

Nam. 13

Utengenezaji wa Madawa

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziko katika maandalizi ya mpango wa utekelezaji wa utengenezaji wa Madawa katika kipindi cha mwaka 2010 – 2016, na kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya utekelezaji wa mpango huo.

Je, Mhe. Waziri, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejiandaa vipi katika utekelezaji wa mpango huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 13 kama ifuatavyo:-

Ni kweli Jumuiya ya Afrika Mashariki imeandaa mpango wa utekelezaji wa utengenezaji dawa kwa kipindi cha mwaka 2010 – 2016 *(East African Community Regional Pharmaceutical Manufacturing Plan of Action 2010 –*

2016) ambao unategemewa kuwasilishwa katika kikao cha Baraza la Mawaziri wa Afya wa Jumuiya Machi 2011.

Hii inatokana na World Trade Organisation (WTO) kupitisha Article 31 ya *Trade Related Intellectual Property Rights (TRIPS*) pamoja na kupitishwa kwa Sheria ya Ataza *(Palent Act)* nchini India, ambayo itazifanya nchi zetu kutoweza kumudu kununua dawa kutoka India ambazo zitakuwa ghali.

Mhe. Spika, katika kuandaa mpango huo kuliandaliwa timu ya wataalamu waliopita katika nchi za Afrika Mashariki ikiwemo Zanzibar. Aidha, kulifanyika mkutano wa siku mbili hapa Zanzibar uliowashirikisha wataalamu kutoka Biashara, Viwanda, Afya, Fedha, ZIPA na Jumuiya za wafanyabiashara na Wakulima. Zanzibar imejiandaa kufanya utafiti na mafunzo pamoja na mambo mengine kuhusu uanzishwaji wa viwanda vya dawa.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Afya inayo mpango wa utekelezaji wa Sera ya dawa 2008 – 2012 ambao unahimiza kuwepo kwa viwanda vya dawa, kwa vile viwanda vya dawa vinahitaji utaalamu mkubwa Wizara ilianzisha mafunzo ya Ufundi Sanifu wa Dawa *(Pharmaceutical Technician)* katika Chuo cha Afya Mbweni. Mwaka 2009 kulikuwa na wahitimu 32, 2010 42 na mwaka huu tunategemea kupata wahitimu 64 wa fani hiyo.

Hatua hii itaongeza ufanisi katika utoaji huduma mahospitalini, pia kuwarahisishia wenye nia ya kuanzisha viwanda vya dawa hapa Zanzibar, chini ya utekelezaji wa mpango wa utengenezaji dawa kwa kipindi cha 2010 – 2016 wa *(East African Community Regional Pharmaceutical Manufacturing Plan of Action).*

Jibu la nyongeza

Katika miaka ya 80 kwa msaada wa UNIDO serikali ilijenga kiwanda cha Madawa kilichokuwa kinatengeneza dawa za vidonge na za maji, hata hivyo kiwanda hicho kilibinafsishwa baadae. Pamoja na kubinafsishwa mwekezaji alishindwa kukiendesha kiwanda hicho na ndipo hivi karibuni kiliporejeshwa Wizara ya Afya kutoka Wizara ya Fedha.

Wizara ina mpango wa kulitumia jengo hilo kwa upanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kujumuisha sehemu ya kupokelea wagonjwa wa dharura *(accident and emergency),* sehemu ya wagonjwa wa nje *(out patient*) na Wodi ya Watoto *(Paediatric Ward).* Hiyo itaipa nafasi Hospitali ya Mnazi Mmoja kufanywa *restore* baada ya vitengo hivyo kuondoshwa.

Hivi karibuni serikali ilitia saini katika mkataba na Nertherland kuimarisha huduma za hospitali ambao pamoja na maeneo mengine utahusisha matumizi ya jengo hilo. Michoro ipo tayari. Kwa sasa jengo hilo linatumika kama ofisi na maabara ya Bodi ya Chakula na Dawa, Watengenezaji wa viungo bandia na afisi za mradi wa afya za kinamama na watoto *(Reproductive and child Health).*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar siku za nyuma tulikuwa tuna kiwanda cha madawa, ambacho kiwanda hiki kilibinafsishwa, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, lakini aliyebinafsishwa alishindwa kukifanyia kazi.

Mhe. Spika, juzi Mhe. Naibu Waziri katika maelezo yake na leo ameeleza kwamba kiwanda hicho sasa kimebadilishwa matumizi yake na kufanywa *extension* ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Swali langu liko hapa.

Kwa kuwa sasa hivi nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi nyingi zimekuwa na viwanda. Kwa mfano, Kenya tayari inavyo viwanda 11, Uganda ina viwanda 7 na Tanzania Bara ina viwanda 7 vya madawa.

Je, Mhe. Naibu Waziri, serikali kwa kuzingatia ushindani wa Jumuiya isiyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, haina mpango wowote wa kujenga kiwanda ili kwenda katika hali ya ushindani kwenye nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, tunafahamu hayo unayoyasema, kwa sababu tunashiriki kikamilifu katika mchakato huu wa kutengeneza viwanda. Kama ulivyosema Kenya wako tayari, Uganda na Tanzania Bara wako tayari, halikadhalika na Zanzibar iko tayari.

Lakini Mhe. Spika, kuna suala hapa la kwamba sio lazima serikali, na nafikiri nimeongelea hapa kwanza. Tunaandaa wafanyakazi na serikali inaandaa mazingira mazuri tu, hata wawekezaji sekta binafsi ina nafasi ya kufanya hivyo.

Mhe. Spika, serikali baada ya kuchukua hii sehemu iliyokuwa kiwanda cha zamani na kuifanya kwamba ni sehemu ya Mnazi Mmoja Hospitali, sio kwa sababu haikutaka kiwanda kile kiwepo pale. Isipokuwa kwanza hospitali tunataka kuifanya ya rufaa, halafu na bahati mbaya mjini hakuna sehemu nyengine ya hospitali ya *district*. Kwa hivyo, vyote vile vinakuwa ni mzigo kwa Wizara ya Afya.

Kwa hivyo, Wizara ya Afya inajipanga na itatengeneza kiwanda, lakini nje ya pale kilipo. Kwa hivyo, kiwanda kitajengwa cha Wizara ya Afya na bohari kuu ya madawa pia itajengwa. Wizara iko katika *process* ya kuomba kiwanja hicho na watu wa nje wa binafsi nao pia wana nafasi hiyo. Maana hata hivyo viwanda vya Tanzania Bara sio vyote ni vya serikali, vingi vyao ni viwanda vya watu binafsi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba na mimi kidogo nichangie hapa ili wajumbe wapate kuelewa.

Mhe. Spika, tuna kampuni mbili, moja kutoka China na moja kutoka India, tumo katika mazungumzo ya kuanzisha viwanda vya dawa nchini. Kwa hivyo, tukifanikiwa tunaweza kuleta *report* kamili baadaye. Kwa hivyo, huo mpango upo na tunawashajihisha zaidi wawekezaji wa nje waje kuwekeza katika viwanda vya madawa na Inshaallah iko siku viwanda vitashamiri hapa Zanzibar.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa ndani ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kuna sera za kuondoa ushuru wa viwanda vilivyomo nchini vya wenyewe. Je, hivi viwanda tunavyoelekeza sisi ni viwanda ambavyo vitakuwa vyetu, ili tuweze kupata huo ushuru katika kuzisambaza hizi dawa au vitakuwa ni viwanda vya kigeni na nafasi hiyo itakuwa haipo?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, suala la kujenga viwanda katika sekta binafsi inategemea wale watakaounda na suala la ushuru haliko chini ya Wizara ya Afya. Taratibu ziko, watapita kunakotakiwa kupita na kama wanapaswa kutoa ushuru watatozwa na kama hawapaswi basi watasamehewa kwa kupitia huko kunakotozwa ushuru.

Nam. 43

Matayarisho ya Mitihani ya Kidato cha Sita

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza:-

Inafahamika kwamba ifikapo mwezi wa Febuari 2011, Wanafunzi wetu wa Kidato cha Sita *(Form VI)* wanakabiliwa na mitihani yao ya Taifa.

Kwa kuwa muda tulionao hadi kufanyika kwa mitihani hiyo ni mfupi mno, Je, Wizara imejiandaa vipi na mitihani ya vitendo (*practical*) kwa masomo ya sayansi, hususan somo la *Chemistry*.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba wanafunzi wetu wa Kidato cha Sita watafanya mitihani yao ya taifa ifikapo mwezi Februari, 2011, ikiwemo mitihani ya vitendo (*practical*) kwa wanaochukua masomo ya sayansi.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki, Wizara kwa kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya lazima (ZABEIP) unagharamiwa na SMZ na Benki ya Dunia imezipatia baadhi ya Skuli za Sekondari vifaa vya maabara pamoja na madawa kwa ajili ya kufanyia mazoezi ya vitendo. Skuli za Sekondari zilizopatiwa vifaa hivyo ni Benbella, Haile Selassie, Lumumba na Chuo cha Kiislamu kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Skuli za Pemba ni Chuo cha Kiislamu, Micheweni na Skuli ya Sekondari ya Konde. Skuli nyengine ambazo zitafanyiwa matengenezo makubwa na skuli mpya za Sekondari zinazojengwa kupitia mradi huu, itazipatia vifaa hivyo mara tu baada ya shughuli za ujenzi kukamilika. Aidha, Wizara itazipatia skuli zinazofanya mitihani ya Kidato cha Sita dawa za kufanyia mazoezi ya vitendo mara mitihani inapokaribia na hili limeshafanyika hivi sasa Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimikunipatia nafasi hii. Mhe. Spika, imekuwa ni kawaida wakati wa mitihani hasa kwa somo la *Chemistry* kukosa zana muhimu kama *burette*, *pipette* na hata zile *beaker* sasa hivi skuli zinanunua hizi *disposable glass* zinazotumiwa katika shughuli za harusi ili kuwekea *solution*. Sasa kuna mabadiliko gani ambayo wizara imejitayarisha ili wanafunzi sasa wafanye mitihani kwa ufanisi zaidi, badala ya kufika saa 2:00 kwa kungojana na *burette* mbili zilizopo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama hivyo ilikuwa ni kawaida kwa wakati huo, labda tulikuwa hatujaamua kuimarisha elimu ya sayansi. Lakini sasa kama nilivyomjibu, mimi nimekuta pale vifaa vya sayansi vimeshanunuliwa *burette, pipette* na mambo mengineyo na tayari vimeshagaiwa katika baadhi ya maskuli. Kwa hivyo, tunategemea suala hili Mhe. Spika, litakuwa halipo tena katika kipindi kinachoendelea.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, tunapozungumzia masomo ya

sayansi huwa yana matayarisho yake, tokea mwanafunzi anapoingia darasa la tisa mpaka anapofanya mitihani. Mitihani yao ya *practical* mara nyingi sio mitihani kwa lile darasa la kumi na mbili tu, lakini ni pamoja na mchanganyiko na haya madarasa ya nyuma.

Mhe. Sipika, hivi sasa maskuli yetu mengi sana hayana maabara na kama mwanafunzi anaposoma sayansi hakufanya *practical* akayaona hasa yale mambo yanavyokua, yaani zile *practical* zinavyofanywa, basi kwa kufanya mitihani tu, itakuwa haimsaidii ipasavyo. Suala langu.

Je, wizara hasa imejiandaa vipi kuona kuwa wanafunzi wa sayansi wanapata somo hilo na wanatumia vifaa vya *practical* tokea wanapoingia mpaka siku ya mitihani, kwa maana ya kuwa wana uzoefu navyo vifaa hivyo na kuweza kulimudu lile somo la sayansi linaposomeshwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, sio skuli zote zinasomesha masomo ya sayansi. Kwa hivyo, mkazo unawekwa katika zile skuli ambazo zinasomesha somo hili la sayansi. Hiyo kama haitoshi kwa sababu tunataka kuimarisha somo hili la sayansi, ndio maana sasa hivi kuna ule mradi wa kujenga skuli za sekondari na kila skuli ya sekondari itakuwa ina maabara tatu pale ilipojengwa katika wilaya zetu, kwa madhumuni ya kuboresha suala hili la elimu ya sayansi ili walimu wetu na wanafunzi wetu wawe wanaipata kwa nafasi.

Mhe. Spika, hizo skuli mpya zinazojengwa kila skuli yenye maabara yake itakuwa na vifaa vyake tayari itakuja pamoja na itakuwa imechanganywa pamoja kwa ajili ya kuimarisha elimu hii ya *basic education*.

Nam. 15

Utekelezaji wa Mradi wa Matengenezo ya Nyumba za Wazee Sebleni

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza:-

Serikali katika mwaka wa Fedha 2010 – 2011, imetenga jumla ya Shillingi Millioni mia moja (100,000,000/=) kwaajili ya mradi wa kuzifanyia matengenezo makubwa nyumba za wazee za Sebleni. Na kwa kuwa hivi sasa tayari tuko nusu mwaka ya utekelezaji wa bajeti hiyo ya Serikali.

(a) Je, Mhe. Waziri, utekelezaji wa mradi huu ukoje.

(b) Je, Mhe. Waziri utakubaliana nami kuwa ipo haja ya Serikali hii mpya ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa

kuangalia upya suala la uhifadhi wa wazee hawa wanaohifadhiwa na Serikali ili waweze kuishi kama wananchi wengine.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 15 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Kwa bahati mbaya sana utekelezaji wa mradi huo bado haujaanza, kwani bado Wizara haijapatiwa fedha hizo, lakini kwa bahati nzuri wizara imeshafanya makisio ya kujenga uzio katika nyumba hizo na ukarabati wa nyumba ambao unakisiwa kugharimu Tshs. 800,000,000/-. Makisio haya yatawasilishwa Serikalini ili kupatiwa fedha na kufanikisha ujenzi na ukarabati unaohitajika.

b) Mhe. Spika, ndio nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kuna haja ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuangalia upya suala la uhifadhi wa Wazee wanaohifadhiwa na Serikali ili waweze kuishi kama wananchi wengine.

Mhe. Salmini Awadh Salmin: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wakati alipokuwa akijibu swali langu alisema kwamba Shs. 100,000,000/-. Lakini pia amezungumzia juu ya suala la upatikanaji wa Shs. 800,000,000/- kwa ajili ya kufanya matengenezo. Nataka kumuuliza Mhe. Waziri.

Je, serikali mpaka leo imeshindwa kutoa Shs. 100,000,000/- ndio itakuja kuweza kutoa Shs. 800,000,000/-?

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, inawezekana ikawa serikali kwa wakati wa kipindi kile haikuweza kutoa shilingi milioni 100. Lakini hivi sasa inao uwezo wa kutoa shilingi milioni 800. (Makofi)

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Hivi karibuni kumetokezea tatizo pale kwenye Nyumba za Wazee kuungua moto. Kwa hivyo, ni hatua gani za dharura serikali imechukua juu ya tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ni kweli kwamba hivi karibuni tulipata maafa katika jengo la Wazee wa Sebleni liliungua moto. Kwa kweli hatua mbali mbali zimechukuliwa kama vile misaada tofauti ilitolewa.

Lakini suala jengine ambalo serikali imelitia mkazo kwamba tulitakuwa na serikali tufanye makisio kwa ajili ya kulijenga paa la ile nyumba iliyoungua na tayari tumeshafanyakazi hiyo, ambayo itagharimu shilingi milioni 81 na laki 5. Kutokana na hali hiyo, serikali yetu imeahidi kwamba itahakikisha jengo linarudi hali yake kama ilivyokuwa au zaidi. (Makofi)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sikusudii kuzuia haki yetu ya kuuliza maswali hadi matatu, lakini muda na kwa sababu muda mrefu ulipotea kutokana na mawasiliano. Kwa hivyo, naomba mniwieradhi na niseme tuendelee, kwani bado maswali ni mengi. (Makofi)

Nam. 4

Kutafuta Wafadhili Watakaoisaidia Timu ya Taifa ya Zanzibar

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Timu ya Taifa ya soka hapa Zanzibar iliyokuwa ikishiriki mashindano ya soka ya Afrika Mashariki na Kati ‘’Challenge’’ ilizawadiwa kiasi cha fedha cha shilingi 3,000,000/- kutoka Uongozi wa Hoteli ya Ocean View pamoja na kiasi cha shilingi 500,000/- kutoka kwa Mwakilishi wa Jimbo la Rahaleo.

(a) Mbali na juhudi hizo za taasisi na watu binafsi, wizara imetoa motisha gani kwa timu hiyo.

(b) Je, wizara inachukua jitihada gani za kutafuta wadhamini watakaosaidia katika kuleta maendeleo katika michezo, kama ilivyo kwa wenzetu wa Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara kwa upande wake ilitoa shilingi milioni kumi (10,000,000) ikiwa ni posho za wachezaji pamoja na viongozi wote walioandamna na timu.

Nafikiri ni vizuri pia kuzitaja taasisi nyingine ambazo walituchangia timu iliposhiriki mashindano ya Challenge nazo ni:-

- Uongozi wa Kampuni ya *FUTURE CENTURY Ltd*. Kwa kugharimia timu yetu kwa kupiga kambi na jezi.

- Uongozi wa Kampuni ya *ZIZOU SPORTS TIPPO* ya Dar-es-Salaam kwa kutoa fulana "T-shirts".

(b) Mhe. Spika, wizara kupitia Baraza la Taifa la Michezo imekwishafanya hivyo kwa vyama tofauti vya michezo.

Jitihada za kutafuta wadhamini watakaosaidia juhudi za kuleta maendeleo ya michezo ni za pamoja kati ya vyama vya michezo vya taifa husika. Kwa kawaida juhudi hizo huanza na vyama vyenyewe na wizara hufuatia kuviunga mkono, kwa kuvipa msukumo vyama husika katika kufanikisha kupata uhisani au ufadhili.

Kwa mfano, Basketball (BAZA), Mpira wa Miguuu (ZFA), Riadha (ZAAA) Hand Ball (ZAHA), Netball (CHANEZA). Wafadhili na wahisani kwa kawaida huwa hawakubali kutoa msaada au udhamini kwa vyama vya michezo bila kuwepo mkono wa serikali.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kabla sijauliza swali langu naomba nifanye marekebisho nilisahau katika swali langu. Wenzetu wa Ocean View walichangia shilingi milioni 4 badala la shilingi milioni 3. Sasa naomba niulize swali moja la nyongeza.

Hivi karibuni ZFA ilifanya uchaguzi wao wa Kitaifa na katika uchaguzi huo ulileta mzozo mkubwa kwenye vyombo vya habari na hata mitaani. Kwa kweli sisi wanamichezo tuliona ni taaswira mbaya. Je, wizara imeshughulikia vipi suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli wizara yangu imeshirikiana na Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFA) katika kulipatia ufumbuzi suala hili kwa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Nassor Salum Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri. Katika suala hili la Uchaguzi wa ZFA kumekuwa na malalamiko mengine mengi kuhusu Katibu Mkuu au Katibu Mtendaji wa ZFA, yaani kuna mambo mengi amefanya ndivyo sivyo (kuchakachua). Je, wizara imemchukulia hatua gani Katibu huyu, ili kuepusha kuleta aibu au jambo lolote la lawama la wizara husika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, naomba kuweka wazi kabisa. Kwa kweli kulikuwa na mgogoro na yalikuja malalamiko mengi kuhusiana na Katibu, lakini kwa wakati ule tuliona hakuna haja ya kumuondoa Katibu, kwa sababu chanzo hakuwa Katibu pele yake. Kutokana na hali hiyo, tuliona hata tukimuondoa Katibu bado yapo matatizo, kwa hiyo tulisema bora kwanza tumuache kwanza na tuangalie hali itakuwa vipi.

Kweli mgogoro ulikuwepo na wizara ililiona hili. Sasa baada ya kuona hali inazidi kuwa mbaya, basi Mrajis wa Vyama vya Michezo kwa mujibu wa mamlaka aliyopewa na Baraza la Michezo ya Sheria Nam. 5 kifungu 19 cha (a), (b), (d) na (v) alitoa agizo kwa Viongozi wa ZFA kukaa kwenye meza na na kutafuta chanzo ni kitu gani kwa lengo la kumaliza mgogoro huo.

Kwa hivyo, kweli baada ya kukaa waliona kulikuwa na mambo mengi ambayo yalijitokeza. Kwanza ukiukwaji wa Katiba, vile vile ndani ya ZFA kulikuwa hakuna Mshika Fedha Mkuu wala Msaidizi. Pia kulikuwa kunafanyika vikao bila ya kupitia Kamati Tendaji ya ZFA. Kwa hiyo, huo ulikuwa ni udhaifu wa Kikatiba. Hatimaye ikabidi kwa vyovyote Mrajis kwa mujibu wa mamlaka aliyopewa kusimamisha uchaguzi ambao ilibidi ufanyike tarehe 19 Nungwi.

Kutokana na hali hiyo, ikabidi kwanza lazima turejeshe uongozi uliopo kama kawaida uendelee na shughuli zake na watafanya shughuli zao kama kawaida, lakini shughuli zetu lazima ziwasilishwe kwa Mrajis kwa maandishi. Vile vile kuhakikisha wakaguzi wa fedha wanapelekwa Unguja na Pemba kwa lengo la kupitia shughuli zote za kifedha.

Mhe. Spika, katika ngazi ya Wilaya hakuna tatizo lolote ambalo lilijitokeza na uchaguzi ulikwenda sana, isipokuwa juu ndiko ambako kulikuwa na matatizo hayo.

Pamoja na hayo, kikao hicho kimeamua kwamba uchaguzi utafanyika mwishoni mwa mwezi wa Febuari au mwanzoni mwezi wa Machi, baada ya kupitia taratibu zote za kikatiba na hapo ndipo utakapoitishwa uchaguzi. Kwa hivyo, nadhani suala la kumuondoa Katibu kwa hivi sasa nafikiri hali ni shuwari ni vyema kufanya subira na tuangalie hali itakuwa vipi. (Makofi)

Nam. 25

Uanzishaji wa Mabaraza ya Biashara ya Mikoa

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza:-

Kwa kuwa Baraza la Biashara la Zanzibar ni chombo ambacho kwa njia moja au nyengine kimeweza kusaidia sana kutatua matatizo mbali mbali ya wafanyabiashara wa Zanzibar; na kwa kuwa wizara yako imepanga kuzindua Mabaraza ya Biashara ya Mikoa (Regional Business Councils) katika kipindi cha mwaka 2010/2011, ili kusaidiana na Baraza la Biashara la Zanzibar (ZBC).

(a) Mhe. Waziri hadi sasa ni mabaraza mangapi ya mikoa yamezinduliwa na ni mikoa ipi.

(b) Kama bado ni sababu zipi zilizopelekea kushindwa kuzinduliwa Mabaraza haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante sana kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais kwa kunipa imani ya kushika nafasi hii. Pili niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Fuoni kwa kunichagua kwa kura nyingi sana za kishindo. (*Makofi*)

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 kama ifuatavyo:-

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inafarijika kuona kwamba Wajumbe wa Baraza lako na wananchi kwa ujumla wanatambua na kutathmini mchango unaotolewa na Baraza la Biashara la Zanzibar (ZBC), pamoja na kwamba tokea kuanza kufanyakazi ni kipindi cha miaka 5 tu. Miongoni mwa kazi zinazofanywa na Baraza hili ni pamoja na kutatua kero mbali mbali zinazowakabili wafanyabiashara na kutoa msukumo kwa sekta mbali mbali, ili ziweze kukua na kuimarika zaidi.

Kutokana na mafanikio yaliyopatikana kwenye Baraza la Biashara la Zanzibar na uzoefu wa wenzetu katika kuendesha Mabaraza ya Biashara ya Mikoa. Wizara iliahidi kwenye hotuba ya Bajeti ya mwaka 2010/2011 kuunda na kuyazindua Mabaraza ya Biashara ya Mikoa *(Regional Business Council*) ifikapo mwisho wa mwaka huu wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huu sasa napenda kujibu swali Nam. 25 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mpaka sasa hakuna Baraza lolote la mkoa lililozinduliwa isipokuwa *Secretariat (Starring Committee*), ambayo inatakiwa kuishauri wizara juu ya umuhimu wa kuundwa kwa mabaraza hayo. Aidha Secretariat imeagizwa kufanya kazi zake kwa umakini mkubwa, ili iweze kufikia malengo yaliyokusudiwa.

(b) Kwa sasa *Secretariat* ya Baraza la Biashara la Zanzibar (ZBC) ipo kwenye hatua za mashirikiano na asasi mbali mbali, kwa madhumuni ya kutathmini haja ya kuwa na mabaraza hayo katika ngazi ya mikoa.

Kwa upande wa Pemba suala la kuwepo kwa mabaraza ya mikoa linaweza kuangaliwa kwa aina yake kutokana na hali halisi ya kisiwani Pemba. Hatua hii ni muhimu na yenye kuhitaji umakini mkubwa, ili kupata uwakilishi wenye kufaa kwenye mabaraza. (*Makofi*).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Miongoni mwa mambo ambayo yanayolalamikiwa sana na Wafanyabiashara wa Zanzibar katika Mkutano uliofanyika mwaka jana wa Baraza la Biashara la Zanzibar pale Bwawani, ilikuwa ni mambo yanayohusiana na mambo ya Muungano hasa suala la ulipaji wa kodi mara mbili kwa bidhaa zinazopitia Zanzibar na baadaye kupelekwa Bara.

Sasa sijui Mhe. Naibu Waziri anaweza kutueleza wizara yake imechukua hatua gani mpaka sasa kuona tatizo hilo linapatiwa ufumbuzi, kwa sababu linaonekana kuendelea. Kwa mfano, jana Mhe. Spika, nilikuwa Dar-es-Salaam na katika kusafiri nilikutana na wafanyabiashara za Zanzibar, ambao waliokuwa wakilalamika juu ya tukio ambalo limetokezea ndani ya wiki hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mjumbe arudie swali lake kwa sababu mawasiliano si mazuri.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ahsante swali langu ni kwamba katika Mkutano wa Baraza la Biashara la Zanzibar uliofanyika mwaka jana pale Bwawani. Miongoni mwa malalamiko makubwa yaliyoibuliwa na wafanyabiashara ni suala la usumbufu wanaoupata katika kusafirisha bidhaa, ambazo tayari zimeshalipiwa ushuru Zanzibar na wanapoziingiza upande wa

Tanzania Bara hutakiwa wazilipie tena ushuru na masuala mengine yanayohusika na kodi.

Kwa kweli suala hili inaonekana bado linaendelea. Sasa sijui wizara yake imechukua hatua gani za kuyafanyiakazi malalamiko haya ya wafanyabiashara yaliyoibuliwa kwenye vikao vya Baraza la Biashara hasa kuhusiana na suala hili la ulipishwaji wa kodi mara mbili kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar kuingia Bara.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, swali hili naona limeulizwa katika swali la msingi. Lakini kwa ufupi tatizo hili limeshughulikiwa kupitia vikao vya Kutatua Kero za Muungano chini ya Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea kidogo majibu kwa faida yetu sote.

Katika sheria zetu za Kodi ya Forodha inatamka wazi kwamba mzigo unapoingia katika bandari halali yoyote iliopo Tanzania ndipo itakapolipiwa kodi. Sasa unapotaka kuusafirisha mzigo ule kuupeleka sehemu nyengine ya Muungano haitakiwi kulipiwa tena kodi nyengine yoyote. (*Makofi*).

Kweli limejitokeza tatizo hilo kwa wafanyabiashara kutoka Zanzibar kulipa kodi na baadaye wanapotaka kuisafirisha mizigo ile kuipeleka Tanzania Bara kulipa difference ya kodi.

Kwa hivyo, tumeanza kuzungumza na wenzetu kupitia Kero za Muungano na hatua ya awali ambayo tumeshafikia ni kwamba yeyote ambaye anatoza kodi ya ziada pale Dar-es-Salaam atakuwa anafanya makosa. Kwa kweli tumewataka wenzetu watuandikie rasmi na afisa yeyote atakayefanya hivyo kwa mujibu wa sheria atapaswa achukuliwe hatua za kisheria. (Makofi).

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa taratibu zinaeleza hivyo alivyoelezea Mhe. Waziri wa Fedha na tayari wapo wafanyabiashara ambao wameathirika na suala hilo la kutozwa kodi mara mbili. Je, serikali iko tayari kuwafidia wale ambao wamefikwa na tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, hakuna utaratibu wa kufidia katika eneo hili kama limeshatokea basi ndio limeshatokea. Lakini hivi sasa kinachopaswa ni kwamba baada ya kupata

maelekezo kutoka kwa wenzetu pamoja na barua basi isingepaswa kutokea tena hicho ambacho kilichokuwakikitokea. (*Makofi*).

Nam. 26

Utolewaji wa Elimu Juu ya Soko la Pamoja

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza:-

Kwa kuwa itifaki ya uanzishwaji wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki tayari imeanza kutekelezwa na Soko la Pamoja limeanzishwa tokea mwezi wa Julai 2010; na kwa kuwa wafanyabiashara wa Zanzibar ni wadau wakubwa wa soko hilo.

(a) Je, Mhe. Waziri, wafanyabiashara wetu na wananchi kwa ujumla wameelimishwa vipi juu ya jambo hili jipya katika mataifa yetu haya.

(b) Utakubaliana nami kwamba hadi sasa wananchi hawajaweza kuelewa chochote juu ya dhana hii hususan Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 26 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, katika kutoa elimu juu ya Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambapo itifaki hiyo ilianza rasmi Julai 2010. Wizara kupitia kikao cha nne cha Baraza la Biashara (ZBC) iliwasilisha mada maalum kuhusu Itifaki ya Soko la Pamoja la EAC kwa wafanyabiashara pamoja na wananchi kwa jumla, ambao waliokuwa wakifuatilia kikao hiki kupitia vyombo vyetu vya habari.

   Vile vile, mkutano huo ulielezea fursa za biashara na masoko zinazopatikana kutoka nchi wanachama, jumuiya pamoja na changamoto na namna ya kukabiliana nazo.

b) Mhe. Spika, kwa sasa serikali imo katika mchakato wa kuandaa na kutaratibu mpango maalum, utakaowezesha kutoa mafunzo kupitia semina, warsha na vyombo vya habari juu Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa wafanyabiashara,

wanasiasa wananchi, Makatibu Wakuu, watendaji mbali mbali pamoja na waandishi wa habari. (Makofi).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ahsante kwa mara nyengine tena. Tukiangalia kwa makini itifaki ya Soko la Pamoja na Afrika ya Mashariki inagusa maeneo mengi ambayo kwa upande wa Jamhuri ya Muungano si masuala ya Muungano.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Naibu Waziri kwa niaba ya serikali anisaidie, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango gani wa kuona itifaki kama hizi ambazo zinagusa ni sehemu ya Uhusiano wa Kimataifa, lakini inagusa ambayo si ya muungano zinafikishwa katika Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuidhinishwa. Pamoja na kwamba mambo hayo, hufikishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, ili kuona sauti ya Wazanzibari kwa mambo yasiyo ya muungano ambayo yanasimamiwa na chombo hiki inawakilishwa ipaswavyo kupitia wawakilishi wao. (Makofi)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli tatizo hilo limejitokeza. Lakini kwa sasa serikali inachukua hatua ya kuandaa waraka, kwa ajili ya kushirikiana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili itifaki ambazo zinazohusu Jumuiya ya Afrika ya Mashariki baada ya kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ziweze pia kupitia katika Baraza lako tukufu kwa yale mambo ambayo si ya muungano. (*Makofi*)

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tumo ndani ya utekelezaji wa Soko la Pamoja la Afrika ya Mashariki.

Je, kwa mwaka huu Zanzibar inategemea kuingiza bidhaa za aina gani katika soko hilo na zenye thamani ya kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kama alisikiliza vizuri katika jibu langu kwenye swali la msingi nimesema kwamba tume katika mchakato na unaendelea na pale utakapokamilika basi taarifa hizo Mhe. Mwakilishi atazipata. (*Makofi*).

Nam. 42

Kiwanja cha Ndege, Pemba

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza:-

(a) Kwa kuzingatia viwango vya viwanja vya ndege Kitaifa na Kimataifa na viwango vyengine vinavyotambulika. Je, Kiwanja cha Ndege cha Pemba kiko katika kiwango gani cha Kiwanja cha Ndege.

(b) Je, serikali ina mpango gani wa kukipandisha daraja.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Kiwanja chetu cha Ndege cha Pemba, kwa kuzingatia dajara na viwango vya viwanja vya ndege kiko katika category ya kiwanja cha ndege cha kitaifa.

(b) Serikali inao mpango wa kukipandisha daraja kiwanja hicho kwa kurejesha taa za kuongozea ndege, ili kuweza kuruka na kutua kwa nyakati zote, yaani usiku na mchana.

Aidha kiwanja hicho pia kiweze kutumika pale panapotokea hali ya hewa kuchafuka pamoja kufanya ukarabati na utanuzi wa jengo la abiria, utanuzi wa barabara ya kurukia na kutulia ndege pamoja na uimarishaji wa huduma za zimamoto.

Serikali inakusudia kutekeleza mpango huo wa uimarishaji huduma katika Kiwanja cha Ndege cha Pemba kupitia msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, ambapo hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kwamba matayarisho ya hadudi rejea zinaangaliwa, kufanya upembuzi yakinifu pamoja na uchunguzi yakinifu kwa ajili ya kujua gharama, mahitaji halisi na kwa hali hiyo mpango utakuwa umekamilika.

Wizara yangu katika mpango huo inaendelea na mchakato wa upatikanaji wa kampuni ya kufanyakazi hiyo haraka iwezekanavyo. Baada ya kukamilika kazi hiyo serikali itaendelea kuwasiliana na benki hiyo na Maendeleo ya Afrika, kwa ajili ya kupatiwa fedha za kugharamia mpango huo kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa kati ya serikali na benki hiyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kweli wewe ni shahidi Mhe. Spika kwamba ndani ya miaka mitano iliyopita 2005 mpaka 2010 tumekuwa tukizungumza kuhusu suala la taa za uwanja wa ndege wa Pemba bila ya mafanikio yoyote.

Kwa utaratibu wa dunia kile kiwanja inawezekana kisiitwe Airport Mhe. Spika, mimi nimesoma kidogo nadhani kinaitwa aerodrome, kwa sababu hakina usalama wa kutosha wa kutua ndege na hali hiyo imethibitishwa na watu wa control.

(a) Je, Mhe. Waziri anatuhakikishia sasa kwa muda gani kiwanja kile kitaitwa Airport, ili ndege ziweze kutua wakati wowote.

(b) Kwa kuwa kiwanja kile ni kiwanja cha kitaifa. Mimi napenda nimuulize Mhe. Waziri, hivi kile kiwanja kina urefu gani ukilinganisha na kiwanja cha ndege cha Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Ni kweli kauli hizi zimekuwepo muda mrefu za kuweza kufanya ukarabati katika uwanja wa ndege wa Pemba hasa kuhusiana na suala la taa, lakini kama tutakumbuka mchakato huu wa ukarabati wa uwanja wa ndege Pemba umeanzia katika Secretarieti ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, kwa upande wetu Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano tumefanya mazungumzo na wenzetu wa Hazina na hivi lipo katika mikono ya Wizara yetu, kama nilivyosema kwamba tunaanza upembuzi yakinifu tutakapokamilisha na tukiweza kupata fedha za kulipa kampuni husika wenzetu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika wako tayari kutufadhili.

Nalihakikishia Baraza hili tukufu tutafanya hivyo pindi tutakapopata fedha na ukarabati utafanywa.

Suala la pili, kwa haraka urefu uwa kiwanja cha Pemba siukumbuki lakini niko tayari kukuletea kwa maandishi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuendelea kutoa ufafanuzi zaidi wa swali lililoulizwa na Mhe. Rashid Seif Muwakilishi wa Jimbo la Ziwani.

Kwanza urefu wa kiwanja chetu cha Pemba ni mita 1,320 hilo la kwanza.

Lakini la pili ni kwamba hatutaweza kusema ni kesho au keshokutwa kiwanja hiki taa zitawaka kwa ajili ya kutua ndege usiku au wakati hali ya hewa

inapochafuka. Lakini nimhakikishie tu Mhe. Rashid Seif kwamba hata jana siku ya Jumapili timu ya wataalam kutoka Uturuki, katika juhudi za serikali kuhakikisha kwamba katika kipindi kifupi kiwanja cha ndege cha Pemba kinatimiza masharti yote ya kutua ndege wakati wowote, ndende ndege kubwa kuliko sasa hivi.

Kutanua jengo lenyewe na kuhakikisha kwamba kiwanja kile hakina sura iliyo sasa hivi, basi hata jana wataalam kutoka Uturuki wamekuweko huko katika kuweko juhudi za serikali kuhakikisha kwamba hili linafanyika.

Kwa kuongeza zaidi ni kwamba sisi tuna ule msemo unaosema mfungeni sio mtafuteni pamoja na kwamba tunawasiliana na ADB, lakini tuna juhudi nyengine za wafadhili au wawekezaji watakaokubali kuwekeza katika kiwanja kile. Kwa hivyo yoyote atakayekuja mwanzo ndie ambae tutamdhamana, dalili zipo na kama nilivyosema si muda mrefu kiwanja cha Pemba kitakuwa kimebadilika.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Viwango ya Zanzibar 2011

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na afya nzuri na leo kwa furaha kuweza kuja hapa kwa furaha Alhamdullillah.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tana nakushukuru kunipa fursa hii asubuhi ya leo kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Viwango ya Zanzibar ya mwaka 2011.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo naomba tena nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi Mhe. Salmin Awadh Salmin pamoja na wajumbe wote wa kamati yake kwa kuweza kupata wasaa wa kupitia mapendekezo haya kwa kujadiliana, kushauriana na hatimae kukubaliana nayo.

Katika miaka ya 1980 Serikali ilichukua uamuzi wa makusudi wa kufanya mageuzi makubwa ya kisera kuhusu usimamizi na uendeshaji wa biashara nchini kwa kuruhusu sekta binafsi, kushiriki katika eneo hilo la uchumi. Mwitikio wa Sekta binasi kuhusu mabadiliko hayo ulikuwa kuridhisha na kufanya Serikali kujenga imani kubwa kutokana na ufanisi wa sekta hiyo.

Mhe. Spika, sekta binafi imeendelea kuimarika na kwamba hivi sasa, uingizaji wa bidhaa na chakula, kwa ajili ya mahitaji ya wananchi kwa kiasi kikubwa unafanywa na sekta hiyo. Ushirikiano wa sekta hiyo na serikali umeendelea kuimarika zaidi baada ya kuanzishwa kwa Barazaz la Biashara la Zanzibar (ZBC).

Mhe. Spika, katika hotuba ya Rais ya mwezi Novemba, 12/11/2010 naomba ninukuu maneno aliyoeleza ukurasa wa kumi na tisa.

Ukurasa wa 19

> "Mwelekeo madhubuti katika hali ya uchumi wetu utategemea sana ushirikiano baina ya vyombo vya umma na taasisi binafsi, serikali itaimarisha mashirikiano kati ya serikali na sekta binafsi kwa misingi ya public private partneship (PPP) au kwa njia nyenginezo, mafanikio katika ukuzaji wa porogram hii ya mageuzi inatarajiwa yapelekee ongezeko la ukuaji wa uchumi kutoka ukuwaji wa asilimia 6.5 mpaka 2009 hadi asilimia 10 ifikapo mwaka 2015"

Mhe. Spika, hata hivyo ushamirishaji wa sekta binafsi ni lazima ujengee misingi madhubuti ya usimamizi ili matunda yatokanayo na uchumi yanayoendeshwa kwa njia ya soko la ushindani yaweze kuwafikia wadau wote.

Mhe. Spika, bila ya kutokuwa na mwendo wa soko la ushindani upo uwezekano mkubwa kwa soko hilo kuzalisha matokeo mabaya, hivi sasa wafanya baishara wanaoagiza bidhaa na kuleta katika soko la Zanzibar wengi wao hawatumii mfumo wa mabenki. Kadhalika bidhaa nyingi zinazoingizwa hazina uthibitisho rasmi wa kukaguliwa kabla ya kusafirishwa. Uendeshaji huu wa biashara una athari nyingi wa kuinyima Zanzibar taarifa muhimu za kutathmini mwendo wa biashara na faida zake kama vile, ukusanyaji wamapato, ukuwaji wa huduma za kibenki na ubora wa bidhaa. Mazingatio muhimu kwa sera za uchumi kwa madhumuni ya kuchochea uzalishaji wa ndani na utoaji huduma na kupeleka kuathiri mbinu za kuandaa mikakati ya kukuza ajira.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia umuhimu huo zipo hatua zilizochukuliwa za serikali kwa madhumuni ya kuweka misingi na taratibu za kusimamia maeneo yasiyokuwa na bidhaa na huduma mbali mbali nchini. Sheria ya kumlinda mtumiaji iliwekwa kwa madhumuni hayo. Kadhalika sheria ya biashara, sheria ya mizani na vipimo, sheria ya leseni pamoja na sera mbali mbali kwa ajili hiyo zilianzishwa. Pamoja na juhudi hizo za kuweka sera na sheria mbali mbali uendeshaji na usimamizi wa biashara nchini uliendelea kugubikwa na upungufu

na mapengo ya kisheria kwa upande mmoja. Udhaifu wa kitaasisi kwa upande mwengine, athari hizo kwa pamoja imesababisha kuwepo na miyanja kwa biashara iliyosababisha kufifia kwa ushindani wa kibiashara katika soko.

Uingizaji wa bidhaa zisizokuwa na viwango, ushirikiano haramu wa wafanya biashara katika kupanga bei za bidhaa na huduma mbali mbali, kadhalika lipo tatizo la bidhaa kuingizwa katika soko bila ya kulipiwa kodi kikamilifu au kutolipiwa kabisa. Hivyo kusababisha bidhaa za aina hiyo zinazozalishwa nchini kuwa na nguvu dhaifu za kushindana katika soko.

Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya mswada huu ni kutunga sheria itakayoweka masharti ya uendelezaji, ukuzaji na usimamizi wa viwango na ubora wa bidhaa hili ili basi serikali iweze kusimamia vyema viwango na ubora wa bidhaa hizo kwa afya za watumiaji na jamii kwa ujumla, na kuchochea sekta binafsi kuzalisha bidhaa bora ili kuiwezesha Zanzibar kupenya katika masoko ya kimataifa.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia haja ya madhumuni yaliyotajwa hapo juu inapendekezwa kutungwa sheria itakayoweka masharti na viwango vya ubora wa bidhaa, kuanzisha chombo cha utekelezaji wa masharti hayo na mambo mengine yanayohusiana na uendeshaji wa biashara katika soko la Zanzibar.

Mhe. Spika, nina matumaini na imani kubwa kuwa nakala ya mswada wa sheria hii imewasilishwa kwa wakati ili kuzingatiwa na Baraza lako na hatimae kupata ridhaa, kwa ujumla mswada wa sheria hii umegawika katika sehemu kuu sita, ambazo kila sehemu inafafanuliwa madhumuni yake kama ifuatavyo.

Sehemu ya Kwanza: Kama ilivyo kawaida ya uandishi wa Sheria, sehemu hii ya kwanza ni utangulizi ambayo inaeleza jina fupi na kuanza kutumika kwa sheria, matumizi ya Sheria, pamoja na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika katika Sheria. Majina 26 yamafafanuliwa kinaga ubaga katika mswada huu.

Sehemu ya Pili: Sehemu hii inapendekeza kuweka masharti ya kisheria ya kuanzisha chombo kitakajulikana kama “Zanzibar Bureau of Standards (ZBS), kubainisha kazi zake, uwezo, uongozi na hadhi yake na mambo mengine yanayohusiana na shughuli za chombo hicho.

Sehemu ya Tatu: Sehemu hii inahusu masharti ya uwekaji wa viwango ambapo inaeleza alaka za viwang, maombi ya kutumia alama za viwango, rufaa, viwango vya lazima, viwango vya Zanzibar, masharti ya kutumia neno viwango na ukaguzi wa bidhaa zilizoingizwa Zanzibar.

Sehemu ya Nne: Sehemu hii inahusu ukaguzi wa viwango ambapo inaeleza uteuzi wa wakaguzi wa viwango, uwezo wa wakaguzi, kosa kwa chombo kinachojitemgea kwa mwajiri au wakala, kumaliza kosa na adhabu za jumla.

Sehemu ya Tano: Inahusu masharti ya Fedha ambapo onaeleza fedha na vyanzo vya fedha za Taasisi, matumizi ya fedha, bajeti ya mwaka na ya ziada ukaguzi wa hesabu za Taasisi na tarifa ya mwaka ya mkurugenzi mkuu.

Sehemu ya Sita: Sehemu hii inahusu masharti ya jumla ambapo inaeleza uwezo wa Mheshimiwa Waziri kutoa maelekezo kwa Bodi, alama za viwango kutolalamikiwa, ulinzi kwa Bodi au maafisa wa taasisi, kutoa taarifa, kanuni na masharti ya mpito, sehemu hii pia inaonyesha Jedweli linaloeleza utaratibu wa mwenendo wa vikao vya Bodi, itakayoundwa.

Mhe. Spika, katika maelezo yangu hapo juu nimejaribu kujenga hoja ya kwa nini imeonekana ni muhimu kutunga Sheria hii na kwa muundo unaopendekezwa. Kadhalika maelezo ya uchambuzi ya kila sehemu ya Mswada wa Sheria yenyewe yametolewa ili kurahisisha mazingatio ya Waheshimiwa Wajumbe. Ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa wajumbe wamepitia mapendekezo yaliyomo pamoja na kuzingatia maudhui ya mswada wenyewe kwa uzito na umakini unaostahili. Hivyo, kwa imani na matarajio hayo Mhe. Spika, naomba Baraza lako tukufu lizingatie na hatimae kukubali pendekezo la kutunga sheria ya kuweka masharti ya uendelezaji , ukuzaji na uwekazi viwango na ubora wa bidhaa na usimamizi wa huduma zinazolingana na hizo na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba vile vile ninukuu ukurasa wa 57 wa hotuba ya Mhe. Rais ambao umetupa sisi changamoto wawakilishi katika Baraza lako tukufu.

Ukurasa wa 57

"Nafahamu kwamba Baraza hili tukufu la Wawakilishi linao wajibu mkubwa katika kuilinda na kuitetea nchi yetu, maendeleo Baraza lina jukumu la kuchochea maendeleo na pia lina wajibu wa jumla wa kusimamia serikali, hivyo Baraza litakapotekeleza wajibu wake vizuri ndivyo jinsi serikali itakavyoweza kutekeleza wajibu wake kwa mafanikio zaidi. Kwa kuwa Baraza hili limeundwa kwa mchanganyiko mzuri baina ya wazoefu na vijana na kuwa na Idadi kubwa zaidi ya wanawake kuliko Baraza lolote lililopita na kwa kuwa utendaji wake utakuwa na dhamiri ya umoja wa kitaifa, nina matumaini makubwa kwamba Baraza litatoa mawazo yaliyo bora zaidi kwa faida ya nchi yetu na wananchi wake."

Kama dira ya kazi zetu hotuba ya Mhe. Rais ya tarehe 11 November, 2010 Mhe. Spika, nawaombwa wajumbe waheshimiwa wa Baraza lako tukufu kuchangia ipasavyo, mapendekezo ya mswada huu na hatimae kuukubali ili uwe sheria na kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha biashara.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

(Hoja ilijadiliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo: (Mhe. Salmin Awadh Salmin): Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyokuwemo ndani yake, kwa kutujaalia uzima, afya na salama, na leo tukiwa tumekusanyika hapa kujadili mambo yenye kheri kwa wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

Pili nichukue nafasi hii kwanza kukupongeza wewe binafsi kwa kuweza kuchaguliwa tena kuliongoza Baraza letu Tukufu hasa katika wakati huu ambapo Serikali yetu imeundwa katika mfumo wa Serikali ya Umoja wa kitaifa. Hongera sana na nakutakia kila la kheri katika changamoto hii.

Kwa nafasi hii hii naomba niwapongeze pia waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza waliopata fursa hii ya kuwemo katika Baraza hili la Nane, wale waliochaguliwa na wananchi majimboni, walioingia kwa uteuzi wa Rais na wale wa viti maalum. Wote kwa pamoja ninawaambia hongereni sana.

Mhe. Spika, pia nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwa kuteuliwa kuwa waziri wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi kwa kuteuliwa kuwa Naibu waziri wa wizara hiyo. Aidha nimpongeze Ndugu Julian Rapheil kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa wizara hiyo, nampongeza pia Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na maofisa na Wafanyakazi wote kwa jumla.

Mhe. Spika, naomba nikushukuru pia kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo ya kutoa maoni kwa niaba kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo juu ya mswada uliyopo mbele yetu, na kwa mnasaba huo huo sitaki niwe mpungufu wa fadhila kwa kuanza kuwapongeza wajumbe wenzangu wa kamati kwa kuteuliwa kuwa wajumbe wa kamati hii lakini pia niwashukuru kwa dhati kabisa kwa wao kunichagua mimi niwe Mwenyekiti wa kamati. Kwangu mimi binafsi uamuzi wao huo nimeupokea kwa moyo mkunjufu nikiupa thamani kubwa.

Mhe. Spika, naomba sasa niwatambue wajumbe hao wa kamati kwa kuwataja kama ifuatavyo:

1.	Mhe Salmin Awadh Salmin	-	Mwenyekiti
2.	Mhe Abdallah Mohamed Ali	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe Mahmoud Moh'd Mussa	-	Mjumbe
4.	Mhe Rufai Said Rufai	-	Mjumbe
5.	Mhe Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
6.	Mhe Bikame Yussuf Hamad	-	Mjumbe
7.	Mhe Mlinde Mabrouk Juma	-	Mjumbe
8.	Ndg Amour Moh'd Amour	-	Katibu
9.	Ndg Asha Said Mohamed	-	Katibu

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kila binaadamu anahitaji kuishi katika mazingira mazuri ya afya njema na kuridhika na thamani ya ubora ama wa bidhaa au huduma anayoipata. Kwa maana hiyo si vyema hata kidogo maisha ya binaadamu yakachezewa au kuhatarishwa kwa kutumia bidhaa au huduma zisizo na viwango kwa sababu tu ya tamaa ya utajiri walionao watu wachache.

Mhe. Spika, mambo haya yanaonekana kujitokeza katika nchi yetu. Kumekuwa na baadhi ya wafanyabiashara wengi wamekuwa wakitumia mwanya huu wa kuingiza nchini bidhaa zisizo na viwango, wakati mwengine ni mbovu za

kuhatarisha maisha ya watu, na hasa chakula. Lakini pia na bidhaa nyengine za matumizi kama zinazotumia umeme, na nyenginezo na kuifanya nchi yetu kuwa kama jaa la kutupia takataka.

Mhe. Spika, kamati inachukua nafasi hii kumpongeza sana muheshimiwa Waziri wa Biashara na masoko pamoja na wasaidizi na watendaji wake wote, kwa uamuzi wao wa busara wa kuandaa na kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu rasimu ya Sheria ya kuanzisha chombo cha kusimamia Udhibiti wa Viwango vya Bidhaa zinazoingia au kuzalishwa ndani kwa ajili ya soko la Zanzibar na nje. Hii inaonesha ni kwa kiasi gani wanavyokereketwa na masuala haya ya uingizwaji na matumizi ya bidhaa zisizo na viwango ambazo kwa kweli hazina usalama kwa maisha ya watu wetu.

Mhe. Spika, matatizo haya ndio yanayozifanya nchi nyingi duniani kuwa na sheria makhususi katika kudhibiti na kuratibu ubora wa viwango vya bidhaa katika kuingiza, kutoa, kutengeneza au uzalishaji wake. Na kwa maana hiyo basi, nasi ni vyema tuwe na sheria hiyo ili iweze kufanya kazi na kujaribu kuondoa matatizo hayo yaliyokuwepo. Lakini pia utekelezaji wa sheria hiyo utasaidia kuliweka vyema soko la bidhaa zetu ambazo tutakuwa tunazisafirisha nje ya nchi yetu na kujenga mahusiano mema ya kibiashara kati yetu na nchi hizo katika kuhakikisha kila mmoja anapata bidhaa iliyo bora na yenye kiwango kilichothibitishwa.

Mhe. Spika, kabla ya kuanzisha mswada huu wa sheria ulio mbele yetu. Serikali kwa madhumuni ya kuweka misingi na taratibu za kusimamia mwenendo wa soko la bidhaa na huduma mbalimbali nchini, ilitunga sheria mbali mbali kama vile,sheria ya Dawa,Vyakula na Vipondozi namba 16 ya mwaka 2003. Sheria ya kumlinda mtumiaji namba 2 ya mwaka 1995, sheria ya Mizani na Vipimo namba 4 ya mwaka 1983 kama ilivyorekebishwa na sheria namba 1 ya mwaka 2004.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi zote hizo za Serikali kutunga sheria hizo, bado hali ya uingizwaji wa bidhaa nchini sio mzuri, bidhaa nyingi zinazoingizwa nchini hazina uthibitisho rasmi wa kukaguliwa na zile zinazotaka kusafirishwa nje ya nchi nazo ni vile vile.

Mhe. Spika, migongano katika utekelezaji wa sheria sio jambo zuri, kumekuwa na migongano katika utekelezaji wa sheria hasa hasa kwa sheria ya Dawa,Vyakula na Vipodozi na ile sheria ya kumlinda mtumiaji.Kamati inazitaka Taasisi zinazotumia sheria hizi, kuacha kabisa tabia hii kwani kwa kufanya hivyo kunatoa fursa kwa wafanyabiashara waovu kutumia mwanya huo katika kupitisha bidhaa zisizokubalika katika soko.

Mhe Spika, Kitengo cha Mkemia Mkuu wa Serikali ni kitengo muhimu sana katika utekelezaji wa sheria hii kwani mfanyabiashara asiporidhika na matokeo ya ukaguzi yaliyofanywa na Afisa wa Ukaguzi wa Taasisi ya Viwango nchini atalazimika kukata rufaa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaitaka serikali kupitia wizara ya afya kuandaa sheria ya Mkemia Mkuu wa serikali, sheria ambayo itamuwezesha kufanya kazi zake kisheria na sio kama ilivyo sasa. Mbali na kuandaa sheria, wakati sasa umefika kwa serikali kuandaa mazingira mazuri kwa Mkemia Mkuu wa serikali, kama vile vifaa vya kisasa, ofisi zenye hadhi, maslahi mazuri yanayolingana na Afisi yenyewe ikiwa ni pamoja na kumpatia usafiri Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, kwa kufanya hivyo tutajijengea mazingira yaliyobora na kupata heshima kubwa ya chombo chetu hiki pia tutaepukana na vishawishi vya baadhi ya wafanyabiashara wanaotumia fedha kama ndio ngao yao ya kuwalinda na maovu. Sheria hii inayopendekezwa inaanzisha rasmi Taasisi ya Viwango ya Zanzibar *(Zanzibar Bureau Standard)-ZBS*. Chombo kinakusudia kuwa ni chenye kujitegemea katika kutekeleza majukumu yake. Kitakuwa na Bodi lakini pia kitakuwa na watumishi wake. Nidhahir kwamba kwa umuhimu wake kitakuwa na kazi nyingi ambazo zinahitaji umahiri, umakini na utaalamu.

Mhe. Spika, miongoni mwa kazi hizo ni kuweka utaratibu au kufanya majaribio na viwango vya alama za vipimo vya ubora wa zana, vifaa na vyombo vya kisayansi, au kufanya ukaguzi wa kuchukua sampuli kwa ajili ya kufanya majaribio lakini pia kuna suala la uanzishaji wa maabara kwa madhumuni ya kazi hiyo.

Mhe. Spika, kazi na majukumu hayo ili yaweze kutekelezwa kwa ufanisi, yanahitaji gharama kubwa, kwani vifaa vinavyohitajika katika maabara ya aina hii ni ghali mno. Kwa kuwa lengo letu ni kuwa na Taasisi ya Viwango yenye kukubalika kitaifa na kimataifa ni lazima serikali iubebe mzigo huu, venginevyo tunaweza kuwa na sheria lakini kwa mapungu tu ya nyenzo basi sheria hiyo isitimize ile kiu ya wengi kama walivyotarajia.

Mhe. Spika, katika kufanikisha haya mkazo usibakie kwenye upatikanaji wa vifaa na nyezo tu lakini na watendaji nao lazima watunzwe. Tunaamini kwamba mafanikio ya Taasisi ni nyenzo na utaalamu, basi tusipoweka malipo yenye vivutio kwa wataalamu wetu wanaweza kutukimbia au wakabakia lakini ikawa rahisi kushawishika na kwenda kinyume na maadili ya kazi zao.

Mhe. Spika, suala la ukaguzi wa bidhaa zilizoingizwa wakati wa kuingizwa kwake au hata baada ya muda wakati zikiwa sokoni ni muhimu sana. Hili

liangaliwe kwa umakini sana kwani kuna wafanyabiashara wengine ni wajanja na wanapokwepa na kuhakikisha kwamba bidhaa zao tayari zimeshafika ghalani na wakiamini kwamba hakuna ukaguzi wa mara kwa mara wanaweza kuuza hata zile bidhaa ambazo hazikuthibitishwa na taasisi hii (ZBS). Lakini wakielewa kwamba suala la ukaguzi ni la mara kwa mara na wanapobainika sheria hii inachukua mkondo wake bila ya huruma tabia hiyo itaondoka.

Mhe. Spika, mapendekezo ya sheria hiyo yamempa uwezo mkubwa mkaguzi kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Hivyo ni lazima uwezo huo autumie kikamilifu.

Suala la utoaji wa adhabu inayostahiki kwa wanaokwenda kinyume na sheria hii lizingatiwe. Kwani mara nyingi tunaweza kusikia kukamatwa kwa muhusika kwa kuvunja sheria lakini pengine taratibu za ushahidi zikawa na mapungufu na watuhumiwa wakaachiwa huru na mahakama. Jambo kama hilo litawakatisha tamaa wasimamizi wa sheria hii.

Mhe. Spika, wakati mwengine kosa linakuwa kubwa kwa mfano anaweza akaleta bidhaa ya chakula ambayo ni mbovu na pengine mtumiaji inaweza ikamsababishia maradhi makubwa lakini zaidi ya adhabu ya kuharibu bidhaa hapati adhabu nyengine. Kamati yetu inasisitiza kwamba adhabu zitekelezwe, kama vilivyo sheria. Mhe. Spika, Kamati yetu inasisitiza adhabu zitekelezwe kama zilivyo sheria.

Mhe. Spika, Zanzibar inataka kuingia kwenye Soko la Afrika Mashariki kama mshindani na sio mshiriki. Ni lazima kujiandaa kwa kuwa na vyombo vyenye kulinda ubora wa bidhaa zake na ulinzi wa soko kwa ujumla. Kuwa na taasisi ya viwango Zanzibar ni mwanzo mzuri.

Mwisho Mhe. Spika, Kamati yetu ya Fedha Biashara na Kilimo inaunga mkono hoja hii. Nami kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Magomeni naunga mkono hoja ya kuwepo kwa Sheria ya Viwango Zanzibar tukitarajia kwamba wajumbe wako wote wa Baraza nao watauchangia Mswada huu kutoa maoni yao na hatimaye kuukubali na kuwa sheria.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza baada ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kutoa mchango wake kwa niaba ya kamati yake.

Namshukuru Allah kutupa uhai, tukawa na uzima na tukapata fursa hii ya kuzungumza machache katika Baraza lako tuku. Kwanza napenda nimshukuru

Mhe. Waziri pamoja na naibu wake na uongozi mzima wa Wizara hii kwa kuweza kuanza na mapema kufanya shughuli katika muelekeo tunaoutaka.

Haidhuru wametukosea kidogo lakini kwa sababu mtoto wa mwanzo huwa anapendwa sana akizaliwa. Mswada huu umeletwa haraka haraka kabla ya kutimiza zile siku ishini na moja (21) lakini kwa sababu ni mwanzo nasema haya. Tunawaomba Waheshimiwa wengine wajitahidi kutekeleza ile kanuni ile wajumbe wapate fursa ya kujitanua katika kutoa michango na kuufahamu vizuri zaidi Mswada.

Mhe. Spika, umuhimu wa mswada huu haujataka kusisitizwa zaidi kwa sababu unamgusa kila mtu kuanzia chakula anachokula, vitu anavyotumia na mambo yote ambayo yanahusiana na maisha yetu. Ni muhimu kwamba tunachokizungumza hapa kiwe kinatekelezwa na tunaweza kutekeleza kidogo kidogo lakini kile kinachotekelezwa kinajulikana kinabaki katika hali ile ile iliyokwisha kutekelezwa. Tusende mbele na kurudi nyuma. Mimi binafsi naitakia kazi njema tasisi itakayoundwa.

Mhe. Spika, sehemu ya kwanza nina mchango wa kilugha. Nilijaribu kupitia maneno kwa lugha ya kiingereza na lugha ya Kiswahili nikaona kuna mambo kidogo yangekaa vizuri kwa yale maneno kutumika vizuri zaidi kwa mantiki yake. Katika kifungu cha kwanza cha maana ya maneno. Neno kitu na neno bidhaa naona lina maana moja, kwa hivyo tusingekuwa na haja ya kuandika maneno mawili, huku kitu huku bidhaa. Tungekubaliana kwamba kwa sababu kwa jumla bidhaa inafahamika basi neno kitu tuliache.

Mhe. Spika, sehemu ya pili kifungu cha 5 (c) nahisi kwamba maneno haya yangepatiwa marekebisho zaidi ya kiutalamu katika kiingereza yametumika mane. nayo ni *manufacture, produce, profess and treated*. Sasa maneno haya kila moja kitaalamu yana maana inayokuwa yanajitegemea kwa mfano neno *profess* imetafsiriwa kutengeneza. Lakini *processing industry* ina ile inayokamilisha ule utengenezaji, vitu vimeshatayarishwa katika kila kiwanda wao wanakuja kukamilisha. Kwa hivyo ingekuwa ni rahisi kusema kukamilisha utengenezaji. Neno *treated* pia naona hivyo ilivyoandikwa inavyokuwa kidogo haileti ile ladha nazuri. Ku- *treat* kitu ni kukipa *added value* ya kile kitu, kukiongezea thamani kile kitu. Hakikamiliki ule utengenezaji wake lakini umekiongezea thamani ya pale kilipokuwa.

Mhe. Spika, tukija kifungu cha (f) kuna neno maintain limetafsiriwa kulinda, lakini ku- maintain hasa ni kudhibiti. Kwa hivyo ingesomeka kuanzisha, kudhibiti na kuridhia. Kifungu (g), neno *recognizes* wameandika kutoa kibali na kuridhia, lakini ukitizama mtu unaridhia kwanza halafu ndio unatoa kibali. Kwa hivyo ilikuwa isomeke kuridhia na kutoa kibali.

Kifungu (h) *evew securing adoption* inatafsiriwa kulinda vile vile. Nayo ni madhumuni ya kufikia matumizi ya viwango ku-*secua* ni kufikia pahala.

Kifungu (a) kushirikiana na mashirika ilikuwa ile ya kikanda ije mwanzo ya kikanda na ya kimataifa kama ilivyo katika kiingereza.

Kifungu (L) kushajihisha na kusimamia wakati hapa imeandika kusimamia au usimamizi wakati neno lililotumika ni *advoca* ni ushawishi.

Kifungu (M) la mwisho ni neno *renew* kwa sababu mbele kunakuja leseni imeandikwa kutoa na kutoa tena si kutoa tena kutoa na kuongeza muda. Kwa sababu leseni unapokwenda kukata unaiongezea muda ile leseni. Sio kutoa na kutoa tena. Kwa hivyo baada ya maneno hayo ya kilugha kidogo ikiwa nimekosea na miye ni binaadamu kwa hivyo naendelea na mchango wa kisheria sasa.

Mhe. Spika, kifungu namba 6(1) katika Mswada huu imeandikwa hivi naomba ninukuu.

> "Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ambaye atateuliwa na Rais"

Mhe. Spika, mimi napenda nimuulize Mhe. Waziri hii kuteuliwa na Rais ni kiitikio cha ushauri. Kwa sababu hizi taasisi za kitaalamu tukiripiti neno hili kila siku lina matatizo yake. Haidhuru Mhe. Rais ndio kiongozi mkuu lakini hii ni nafasi ya kiutaalamu. Lakini haitolewi nafasi ya kuomba na ikatangazwa hii nafasi. Ingakuwa wanapatikana watu wenyeuelewa mkubwa zaidi na nafasi nzuri ingelipatikana ya kuwachambua hawa waombaji.

Mhe. Spika, ushahidi umejotokeza hivi karibuni mara baada ya uchaguzi huu tulioufanya sisi wa 2010. Mhe. Rais aliteuwa majaji wanne wa Mahakama Kuu, notion ni ile ile kwamba Rais atatumia hekma yake kuteuwa. Lakini Chama cha Wanasheria wa Zanzibar kiliandika katika makala mbali mbali ya vyombo vya habari kwamba uteuzi ule haukuowana na taratibu za kisheria. Sasa na hizi taasisi za kitaalamu kuendelea kusema kwamba atateuliwa na Rais bila ya kutia vigezo vyovyote kwamba itatangaziwa, tutaendelea vile vile katika tradition hii.

Mimi naomba Mhe. Waziri kwanza unijibu kwamba hii ni tradition iliyozoeleka au ina mantiki fulani na pia haisaidii kupatikana viongozi au mkurugenzi Mkuu akawa bado kuna wenzake ambao wangelipata zaidi wao.

Je, hakuna njia nyengine ya kurekebisha ili mtaalamu huyu akapatikana kwa njia ya matangazo kama matangazo ya kazi.

Mhe. Spika, kifungu cha 6(3) kinasisitiza hoja yangu. Kinasema hivi Mkurugenzi Mkuu atakuwa ni mtendaji Mkuu wa taasisi na atawajibika kwa bodi kwa uendeshaji wa shughuli na kazi. Mimi namuuliza Mhe. Waziri mtu ambaye ameteuliwa na Rais atawajibikaje kwa bodi wakati sio iliyomteuwa. Yeye atawajibika kwa Mhe. Rais ambaye amemteuwa, hapa ndio panamigongano. Kiutaratibu bodi ilikuwa iyundwe mwanzo, itoe matangazo ya mkurugenzi Mkuu ndivyo atakavyochaguliwa. Yoyote yule akayechaguliwa atawajibika kwa ile bodi kwa sababu ndiyo iliyomteuwa baada ya kupitia sifa zake na vyeti vyake. Tukiendelea na tradition hii ya kwamba ateuliwe na Rais halafu awajibike kwa bodi kutakuwa na ugumu katika utekelezaji.

Mhe. Spika, kifungu namba 6(4) Mkurugenzi Mkuu atateuliwa kufanya kazi kwa mujibu wa masharti yatakayoelezwa katika barua yake ya uteuzi. Huku kaambiwa atawajibika kwa bodi, huku masharti ya kazi yake yamo ndani ya barua, barua imeteuliwa na Rais kwa hiyo bodi itakuwa na msemo gani hapa kwake yeye na barua anayo imetoka kwa Mhe. Rais au Afisi ya Rais. Kwa hivyo bado kuna mgongano hapo wa utendaji wa kazi yake.

Mhe. Spika, katika kifungu nam. 7(2) sasa tunaingia kwenye bodi yenyewe. Taasisi kutoka katika mfuko wake wa fedha inaweza kupanga utaratibu wa mafunzo kwa wafanyakazi wake na mambo mengine yanayohusiana na hayo kama itakavyoona inafaa katika utekelezaji bora wa kazi zake. Haipati idhini ya bodi, kwa njia yoyote taasisi itakapopanga mambo yake wapate na idhini ya bodi. Kwa hivyo kifungu hichi kimekosa idhini ya bodi.

Mhe. Spika, tukija kifungu cha. 8(3) wakati wa uteuzi wa wajumbe chini ya kifungu hiki Waziri atahakikisha kuwa wajumbe hao wanauelewa. Bado bodi imeachwa, wateuzi wa bodi hao.

Kifungu cha. 8(5) Waziri anaweza kwa kutoa agizo katika gazeti rasmi la serikali kurekebisha, kubadilisha, kuondosha au kufuta na kuweka upya mambo yote au lolote katika jaduweli la sheria hii. Hapa tunampa uwezo mkubwa sana Waziri bila ya kutumia bodi ya wakurugenzi. Hapa panataka kuangaliwa, wakati kuna bodi ya wakurugenzi wa taasisi hii, lakini waziri amepewa uwezo wa kubadilisha chochote na kuondosha chochote bila ya kushauriana na bodi au bila ya kuishauri bodi. Je, ile bodi kwa pale itakuwa ina mamlaka gani?

Mwisho Mhe. Spika, katika mchango wangu kifungu cha 8(6) bodi itateuwa mwanasheria mwenye sifa kuwa Katibu wa Bodi. Hapa tena vile vile kuna matatizo ya nafasi. Kama bodi itateuwa na hii ni nafasi ya kazi kwa nini

haitangaziwi. Bodi inadi nafasi hii na waweze kuteuwa baina ya yale majina. Lakini kwa bodi tu kuachiwa kwamba itateuwa na ndio maana si vibaya kusema kwamba baadhi ya bodi, ukishaingia katika bodi una influence ndugu yake apate nafasi, mjomba wako apate nafasi, mambo kama haya yanatokea. Lakini kama nafasi zinatangaziwa hutoi nafasi, haidhuru wewe umo ndani ya bodi lakini si rahisi kutoa nafasi za upendeleo wa jamaa na marafiki.

Mhe. Spika, baada ya kusema haya napenda niseme kwamba Mswada huu ni muhimu sana na una manufaa mengi na makubwa kwa nchi yetu. Kwa hivyo mimi baada ya Mhe. Waziri kunijibu baadhi ya maswali ambayo nimeuliza naunga mkono hoja hii na nautakia kile la heri. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia nafasi hii ili kutoa mawazo yangu kuhusiana na hoja iliyokuwepo mbele yetu. Mhe. Spika, kwa kweli ningependa nichukue fursa hii kwanza kuipongeza serikali kuleta hoja hii hapa, ni hoja nzuri. Nadhani kama itapita hapa Barazani itakuwa ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, hivi sasa wakati tunazungumza kuna tatizo kubwa kwa wananchi kuhusiana na kukosa viwango na hapo wanaitumia wafanyabiashara fursa hii ya kwamba hakuna bodi inayoshughulika na viwango na wao wanapata mwanya wa kutuletea mambo ambayo ni nje ya viwango na hatimaye wakauza wanavyotaka bidhaa hizo matokeo yake hata afya za wananchi zikaathirika hasa pale wanapouza bidhaa hizi za vyakula.

Mhe. Spika, kukosa viwango katika nchi ni tatizo kwa sababu hata umkamate mfanyabiashara mathalan kaleta bidhaa chini ya kiwango anaweza akakushinda mahakamani, akasema nyinyi mnatumia kiwango gani. Kwa hivyo hoja hii iliyopo mbele yetu leo hii inaweza ikawa ni ukombozi kwa wanachi wetu.

Mhe. Spika, sasa niende moja kwa moja pamoja na kwamba Maalim Rashid kanifilisi niende moja kwa moja katika uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hii.

Mhe. Spika, ni lazima tukubali kwamba nafasi hii ni ya utendaji na ni lazima tukubali kwamba kuna mambo ambayo tukiyafanya tunamuongezea majukumu Rais wetu. Kwa sababu huyu ni mtendaji na kwa sababu Zanzibar ni nchi ambayo ina demokrasia na utawala bora. Mimi nadhani niungane na mwenzangu aliyepita kwamba nafasi hii ingetangazwa ili watu waka apply kwa mujibu wa *qualification* zilizoelezwa.

Baadaye Rais akachagua kwa mujibu wa sifa aliyekuwa na sifa zaidi katika wale. Hii itasaidia sana kwamba ile national cake anapata kila mtu kwa mujibu

wa sifa aliyekuwa nayo. Tukimuachia Rais moja kwa moja hizi sheria zetu zinaweza zikawa na tatizo kidogo. Zinaweza zikawa zinalingana na zile sheria zinazotungwa katika nchi za Monaki na Sultanet wao wanakuwa wanawachukua wana wao tu katika ukoo, sisi tutofautiane nao kidogo kusudi nafasi hizi ziwekwe wazi ili kila mwananchi aombe na akiwa na uwezo aweze kupata nafasi hiyo.

Mhe. Spika, huyu Mkurugenzi Mkuu mimi nadhani ingekuwa tumejikita katika utawala bora zaidi, baada yakuteuliwa na Rais kwa sababu ana jukumu kubwa akathibitishwa hapa. Hii ingeweza kuleta ile *democratic legitimacy* angeteuliwa na Rais halafu tukaja kumthibitisha nayo ingepunguza kero. Vile vile mkurugenzi huyu kwa sababu kateuliwa na Rais basi anaweza akafanya mambo ambayo bodi haitoweza kumdhibiti.

Niungane na mwenzangu kwamba suala la mkurugenzi huyu kuteuliwa na Rais halafu akawajibika kwa bodi ni tatizo kubwa. Bodi haiwezi kumdhibiti kwa sababu yeye ni *presidencies appointment*. Ningemuomba Mheshimiwa uteuzi wa huyu kwanza iteuliwe bodi halafu yeye ateuliwe na bodi *than* yeye awajibike kwa bodi ili aweze kuwa na nidhamu katika utendaji wake. Lakini kana kila kitu tutamuachia Rais, Rais ana mambo mengi na huyu bwana anaweza akafanya kibri asiweze kufanya kazi vizuri na hii bodi.

Mhe. Spika, katika majukumu katika ukurasa wa 187 ibara ya 2 (c) juu ya uundaji wa hii bodi ya wakurugenzi. (C) hapa inasema Mwenyekiti ambaye ameteuliwa na Rais halafu kunakuwa na Mkurugenzi, halafu kunakuwa na wajumbe wengine watano watakaoteuliwa na Waziri kutoka wizara inayohusika kama Biashara, Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Jumuiya ya Wafanyabiashara.

Mimi nasema hapa katika Wizara ya Afya ingetajwa kabisa kwamba atoke kwenye Kitengo cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanaweza wakatuletea mtu pengine ni daktari in medicine. Lakini itajwe hasa katika sheria kwamba Wizara ya Afya ituletee mtu kutoka kitengo cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maana ya mtu aliyebobeya katika masuala haya ya industry chemistry kusudi isije ikawa kuna matatizo mengine.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Allah (SW) aliyetuwezesha kuwa wazima katika jengo letu jipa hili, jengo lenye kila aina ya sifa, jengo zuri. Kwa vile hii ni mara yangu ya mwanzo kutoa mchango wangu nataka kuweka wazi neno wakala tafsi yake

haikutolewa, nashani tafsiri yake iwepo kwanza ili ieleweke, katika kifungu cha 4 (1).

Mimi nadhani neno wakala linamaanisha chombo kimoja kinawakilisha chombo chengine. Kwa kifungu hiki Nam. 4 kinaeleza kuwa taasisi ya Viwango ya Zanzibar inawakilishwa. Kwa kawaida anayewakilisha anatekeleza kazi aliyopewa na yule aliyempa mamlaka. Kwa maana hii dhana ya uwakala inamfanya anayewakilisha asiye na mamlaka zaidi ya yale aliyopewa na huyu anayemuakilisha.

Hiyo ndio maana yangu kisheria kwa upande wa wakala. Ndio maana pale endapo aliyepewa uwakala amekosea basi hatua zinaweza kuchukuliwa dhidi ya yule aliyetoa uwakala na kumpa mwengine. Kwa maana hii Wakala hawezi kuwa mwenye kujitegemea akiwa anajitegemea basi huyo anayo mamlaka yake mwenyewe aliyopewa kisheria.

Kifungu cha 4(1) na (2), kuna mambo mawili yaliyochanganyika, kuwa huwezi kuwa na wakala tu lakini wakala wa mamlaka kamili kwa vyovyote mamlaka yale unayemuwakilisha. Ushauri ni kwamba tuondoshe neo wakala kwenye kifungu Nam. 4(1) na badala yake tuweke neno taasisi.

Mhe. Spika, pia kwenye kifungu Nam. 4(2) kuwa taasisi hiyo itakuwa ni chombo kinachoweza kujitegemea chenyewe. Hapa kuna swali. Je, chombo hiki mbali na kuwa na mamlaka hii kinao uwezo?

Nimetangulia kusema kuwa chombo hiki ni vyema kuanzishwa kama taasisi ni sio wakala kwa maana kiwe na mamlaka kamili. Lakini mamlaka matupu bila ya uwazo yatasaidia. Ni lazima serikali iwe na mikakati madhubuti ya kuiwezesha taasisi hii na sio uwakala ili kuweza kufanya kazi zake vizuri.

Kwa maisha yetu ya watu wetu ni lazima ipewe uwezo wa aina zote ili kuhakikisha malengo yake yanatekelezwa. Kwa msingi huu naomba nipendekeze kuwa neno kinachoweza lililopo mara baada ya neno chombo kwenye kifungu Nam. 4 (c) lifutwe na badala yake liwekwe neno Mamlaka yenye Uwezo wa chombo.

Mhe. Spika, mchango wangu wa tatu ni kwenye kifungu 5(1), kifungu hiki kinasema taasisi inaweza kuwa na uwezo.

Mhe. Spika, mimi nina wasi wasi na haya maneno yaliyotumika hapa kwamba taasisi ina uwezo au inaweza kuwa na uwezo. Mhe. Spika, kama sheria hii inakusudiwa kuwa taasisi iwe na uwezo basi tuseme moja kwa moja tu kuwa taasisi na sio wakala. Lakini nikichangia hoja zangu za awali napendekeza sana

kuwa kifungu Nam. 5 (1) kiwe kina maneno yafuatayo: Taasisi itakuwa na mamlaka na uwezo wa kutetea kazi.

Mhe. Spika, huu mimi ndio mchango wangu kwa leo, ahsante sana.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, kazi kubwa katika kuuchambua pamoja na kupendekeza baadhi ya mambo kwenye mswada huu tulikwishakufanya katika Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo, lakini kuna maeneo ambayo nilitaka kuchangia zaidi kwa bahati nzuri mzee wangu hapa na Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani naona aliangalia vizuri na akaweza kukamata baadhi ya maeneo. Hata hivyo, nashukuru sana kwa hilo.

Mhe. Spika, lakini nina tatizo katika kifungu Nam. 20 (6) ukurasa wa 191 kinasema:

> "Endapo bidhaa zilizoingizwa hazikokatika kiwango kinachohitajika bidhaa hizo hazitoruhusiwa kuuzwa au kwa matumizi ya ndani na muingizaji au aliyezileta atatakiwa kuziondosha bidhaa hizo ndani ya Zanzibar ndani ya kipindi cha wiki mbili au kuziharibu kama taasisi itakavyoamua".

Mhe. Spika, ukitizama uwezo wa wafanyabiashara wetu hususan hapa Zanzibar ni watu ambao wengi wanakwenda katika utaratibu wa mikopo, na huu mswada tutakapokuwa tunajadiliana hapa tukishakuupitisha itakuwa ni sheria tayari. Mhe. Spika, tuna matatizo ya ma-agent ambao tunawakabidhi mizigo yetu tunapokuwa nje, ma-agent hao wakati mwengine wanafanya ukorofi wa makusudi kabisa kucheleweshe mzigo ule kuingia kwa wakati. Pia kuna baadhi ya nchi unaweza ukenda ukanunua mzigo mwengine na ukatiliwa mwengine kuja kuuleta nchini kwako na yule mfanyabiashara ambaye atakuwa analeta mzigo ule ndani ya nchi yetu mara nyingi wanakwenda katika utaratibu wa mikopo, mzigo unaweza ukafika yeye akawa hana uwezo wa kwenda kulipia ushuru.

Mhe. Spika, pengine mzigo ule ukawa katika utaratibu kama huu hivyo hauwezi kumsaidia yeye kwa maslahi yake wala kwa maslahi ya nchi yetu. Kwa hivyo, hebu tuangalie zaidi namna ya kuweza kumlinda mtu wetu na yule mtu ambaye atakuwa analeta mzigo ambao sio adhabu hii anakuja kupata mfanyabiashara wa Zanzibar. Mimi naomba tuliangalie hilo kwa makini zaidi. Ahsante sana Mhe. Spika, na baada ya maelekezo haya naunga mswada huu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii kuweza kusema mawili matatu angalau kutia baraka zangu katika matayarisho ya Mswada huu wa Sheria ya Viwango.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba sasa lazima tubadilike kwa sababu kama wenzangu walivyotangulia kusema kwamba Zanzibar ni nchi ndogo sana, lakini iliyogeuzwa dampo la bidhaa zisizokuwa na viwango na visivyofaa katika matumizi ya binadamu.

Mhe. Spika, tukitilia maanani masuala ya viwango tunaweza kusema bidhaa takriban kama sio zote basi ni asilimia 80 zinazoingizwa hapa nchini hazina viwango vya kutumiwa na Wazanzibari. Kwa mfano, bidhaa za chakula nimesema mara nyingi tunaletewa bidhaa za chakula zisizofaa hasa mchele hata mpaka ukatungiwa jina ukaitwa 'mapembe'.

Mhe. Spika, juzi moja nilikuwa na Mhe. Naibu wa Biashara akaniambia hakuna mchele wa mapembe isipokuwa sijui ilikuwaje ukaitwa mapembe lakini sasa inaeleweka kwamba mapembe ni mchele tunakula tu lakini haturidhiki nao. Mhe. Spika, inawezekana sababu ya matatizo ambayo tunayapata Wazanzibari ya kiafya ni kutokana na kula vyakula hivi.

Mhe. Spika, wengi wetu tunaumwa hapa unaweza ukamuona mtu anakwenda na kurudi lakini ukitaka kumjua kama anaumwa wewe muangalie akipanda huko juu, basi anajikamata humu kwenye magoti, magoti yote hayafanyi kazi. Kwa hivyo, tunajiuliza kwa nini maradhi ya magoti yawe ni mengi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, pia mimi sio mtaalamu wa madawa lakini nina wasi wasi na madawa tunayotumia kwenye pharmacy zetu nyengine hazina viwango. Mhe. Spika, sijui inakwenda na mazingira ya hali ya uchumi wa Wazanzibari. Lakini unaweza ukala dawa gunia nzima na hazikusaidii kwa yale maradhi uliyokwenda kusema hapo. Lakini ukivuka hapo ukenda Tanzania Bara unaweza ukapewa kidonge kimoja tu ikawa ni suluhisho la matatizo yako. Sasa mimi huwa najiuliza hizi dawa tunazokula huwa hazina viwango au tunaletewa sisi ndio uwezo wetu wa kuzinunua na zile zilizokuwa zinatibu hatuna uwezo wa kununua, lakini mimi nafikiri bado ni tatizo la viwango.

Mhe. Spika, kama wenzangu walivyoeleza pia tuna tatizo kubwa sana la viwango vya vifaa vya majenzi. Mhe. Spika, unaweza kwenda dukani ukanunua balbu zisikusaidie hata kwa masaa kumi na mbili ya usiku mmoja likaungua, na siku ya pili ukanunua tena lisifike vile vile. Kwa hivyo, mimi nadhani tuna wajibu Wazanzibari kubadilika kwa sababu matumizi ya hapo kwa hapo ya kila siku yanatupotezea fedha nyingi.

Mhe. Spika, sasa hivi imeshakuwa ni utaratibu wa kawaida katika hivi vitu vya matumizi ya nyumbani wafanyabiashara wetu karibu nusu nzima sasa hivi wameacha kuleta bidhaa mpya wanatuletea vitu vilivyochakaa. Mhe. Spika, tunazinunua kwa sababu televisheni nzima unaweza ukaikuta inauzwa shilingi 20,000/= tena unaweza kuona channel nyingi sana, lakini unapoipeleka nyumbani mara baada ya wiki ni mbovu.

Mhe. Spika, sasa hivi Zanzibar ina mzigo mkubwa sana wa vitu vya mitumba vilivyokuwa havina pakuwekwa. Kwa hivyo, nafikiri taasisi hii ya viwango ambayo leo tuko hewani tunajaribu kuinda ikazingatie mambo haya yote hivyo tunahitaji kupata bidhaa ambayo tukiinunua basi tunaweza tukadumu nayo angalau kwa miaka miwili mpaka mitatu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa napendekezo kama itawezekana na kama utaratibu wa kibiashara unakubali kwamba sasa mfanyabiashara akitaka kuingiza bidhaa yake hapa nchini lazima aoneshe viwango kabla haijaingia. Mhe. Spika, taasisi hii ikiona kama inaridhika kwamba bidhaa hiyo iingie hapa basi sawa, lakini kama hairidhiki imwambie huko huko kama bidhaa hiyo usijekuingia nayo hapa nchini. Mhe. Spika, kama hilo taratibu za kibiashara zinawezekana mimi nilikuwa nafikiri jambo zuri la kulifanya ili tusiendelee kurundika mambo ambayo hayatufai hapa nchini kwetu.

Mhe. Spika, jambo jengine muhimu sana ambalo wenzangu wamelisisitiza ni haja ya kupata wataalamu tena wa fani zote, maana sisi Wazanzibari tunamahitaji ya mambo mengi, na kila mahitaji yetu basi kunakuwa na mtaalamu maalum ambaye anaweza kuthibitisha kama hili jambo limefika kiwango kinachohitajika. Kwa mfano, tuna wataalamu wa majenzi humu wanaweza kuthibitisha kama bidhaa hizi za majenzi ziko kwenye kiwango kinachokubalika, tuwe na wataalamu wa afya wanaoweza kuthibitisha madawa, pia tuwe na ma-engineer wazuri wanaoweza kuthibitisha kama magari yanayoletwa, televisheni yote yamefikia viwango.

Mhe. Spika, hii ni kazi ya waziri na bodi yake, lakini nafikiri ni jambo moja muhimu sana lakini pamoja na hilo linakwenda sambamba na vifaa vya uchunguzi vya kujaribia hizo bidhaa zenyewe. Kwa hivyo, hapa tulipo ni mwanzo ni sawa sawa na kusema sasa bismilahi tunaanza safari, lakini tujue kwamba bado tuna kazi ngumu sana na ndefu ya kuhakikisha kama hii taasisi tunayoiunda basi inafikia malengo yale tuliyokusudia.

Mhe. Spika, sikutumia muda mwingi lakini huo muda niliyotumia nimetoa nafasi kwa wenzangu kuweza kujipanga vizuri. Ahsante sana na mimi naunga mkono hoja ya mswada huu.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi yakuweza kuchangia katika Mswada huu wa Sheria ya Viwango vya Zanzibar 2011 kwamba ni mzuri kwetu na unaweza kuleta manufaa makubwa kwa nchi hii. Mhe. Spika, zaidi katika mswada huu utakuwa unaelekeza mambo yake sana kwa mambo yote ya bidhaa, bidhaa tunazifahamu ni nyingi kuna bidhaa za chakula, kuna bidhaa za nguo, kuna bidhaa vya vitu vya umeme kuna bidhaa namna kwa namna katika nchi hii.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme pamoja na jitihada ya wizara kutaka kuweka viwango maana yake ukiweka viwango ina maana kusema kwamba tunataka kukuza kiwango cha nchi yetu kuwa kila kitakachoingia kiwe katika hali ya juu kabisa. Lakini sasa tuangalie tunakotoka na tulivyozoea kwamba tumezoea nchi hii ni nchi ambayo ni ya makachara kachara kila kibovu na kibaya kinaletwa kwetu sisi.

Mhe. Spika, kuna mambo ni lazima tuangalie tukitaka tusitake kwa sababu mtu kumtoa katika hali ambayo aliyokuwa akiendelea zamani na ukamuondosha katika hali ile kwa ghafla hiyo ukamuweka katika hali ya kiwango cha juu ina maana unataka umuweke katika hali ya juu, badala ya kununu bidhaa ambazo sio nzuri aweze kununua bidhaa zilizokuwa ni za uhakika na nzuriu.

Mhe. Spika, hapa ina maana mtu huyu kama ikiwa maisha yake yalikuwa ni duni na unampeleka katika hali ambayo ni ya juu kabisa ina maana huyu lazima tumuweke vizuri katika maisha. Mhe. Spika, sisi tuna tatizo la watu wetu kwamba tunataka tuwatoe katika umasikini, na umasikini kwa Zanzibar umejaa sana. Kwa hivyo, ni juu ya wizara itafanya nini hivi sasa wakati hali yetu tuliyozoea ni kama hiyo. Je, wizara itakuwa na mpango gani wa kuweza kuhakikisha kwamba kwa wananchi au wafanyabiashara wote kwamba bidhaa zitakazoingia ziwe ni za uhakika na ukweli?

Mhe. Spika, sisi tumejionea kwa muda mrefu hapa kwamba katika bidhaa ya chakula. Mhe. Spika, katika Baraza lililopita tumewahi kuleta mchele hapa ambao ulikuwa haufai kutumiwa na binadamu, na matatizo ya Baraza tumeona hapa kipindi kile kilikuwa kigumu sana tulitaka kufanya tume hapa ambayo kikatiba au kanuni ya hapa tunao uwezo wa kufanya kamati ya kuchunguza matatizo na tulishindwa kuweza kufanya mambo hayo. Mhe. Spika, serikali ilibidi ichukue mkondo wake tukaona hilo jambo halitowezekana lakini ilifanyika hivyo kwa sababu haiwezi kuwa yule yule aliyefanya makosa halafu umpe kazi ya kuchunguza mambo yale yale.

Mhe. Spika, kwa hiyo utakuta pana ugumu sasa hivi wakuweza kudhibiti hii hali kwa sababu watu wamezoelea kuingiza kwa njia ya rushwa. Mhe. Spika,

hii tunayotaka kuiweka sasa hivi katika kiwango cha hali ya juu basi inawezekana ikapitishwa kwa mlango wa nyuma watu wakapewa rushwa ile mali ikapita au bidhaa ambayo tunaikataa. Mhe. Spika, baada ya kufanya Serikali ya Umoja wa Kitaifa tumeona juhudi za mawaziri walizofanya, lakini muda ule ule baada ya kuingia na bidhaa mbovu ya chakula iliingia kwani mchele mbovu uliingia katika nchi na watu walikula mchele huo.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Waziri aliyepita alisema mnahangaika juu ya kutafuta mchele mbovu, lakini mchele mbovu umeshaliwa. Mhe. Spika, hii hali inaonesha na juzi mchele mbovu ulililiwa na waziri tayari alikuwemo ndani ya serikali. Kwa hivyo, hii kudhibiti hali ya maingizo vya vitu kama hivi hasa chakula kwa sababu chakula ni hali ambayo ya kuangaliwa katika nchi hii. Mhe. Spika, sasa hivi Zanzibar kuna mambo mengi, kuna magonjwa mengi sana yanaingia na hatujui magonjwa haya yanatoka wapi, lakini watu wengi wanasema ni kutokana na chakula ambacho kinaingizwa hapa nchini kwetu.

Mhe. Spika, mimi nasema waziri anayehusika ana kazi kubwa sana, kwani ni wapi tunanunua bidhaa zetu, hilo tujiulize sisi wenyewe. Mhe. Spika, sisi hatuna viwanda vya aina kama hii lakini tunategemea kupata vitu vyetu kutoka nchi jirani, basi tuangalie nchi jirani vitu ambavyo sisi hapa Wazanzibari tunanunua kutoka Bara. Mhe. Spika, mimi nafsi yangu nimeshuhudia kuona televisheni kwa macho yangu vitu vipya vinapondwa pondwa na huwezi kuamini kama vitu vile havifai.

Kwa hivyo, haya itakuwa ni mashirikiano baina ya Zanzibar katika suala la kibiashara hapa na Bara ili ipatikane kiungo cha kuonesha kwamba huko huko Bara wanaweza kudhibiti kwa sababu watu wa Unguja wanununua bidhaa kutoka Bara. Kwa hivyo, kama bidhaa zinanunuliwa kutoka Bara je, Bara kiwango chake cha kibiashara kikoje. Kwa hivyo, imekuwa ni kama dampo la kuleta bidhaa mbovu kwa sababu watu wanaleta hakuna udhibiti wa kitu chochote.

Mhe. Spika, hapa hapa kama tunataka kununua vitu vya umeme basi kuna vitu ambavyo sio vya uhakika unaweza ukatumia leo basi asubuhi yake kimeshaungua. Hii ni ishara kwamba hakuna umadhubuti wa vitu hivi. Lakini hapa tunataka kufanya kitu kama hiki tuone kwamba ni gharama kubwa na wananchi wetu itabidi wajiweke katika mfumo wa kimaisha ambao utakuwa ni mpya kabisa, mfumo ambao pengine unaweza kuwafanya watu wengi washindwe kununua baadhi ya vitu ambavyo tunataka kuviweka katika viwango vya juu. Mhe. Spika, kwa hivyo sio rahisi kusema tu kuweka sheria, sheria ambayo udhibiti wake bado utakuwa ni mdogo kudhibiti hizi bidhaa.

Mhe. Spika, kuna milango hii ambayo bidhaa zinaweza kuingia katika milango yoyote, ni nani atakayeweza kudhibiti bidhaa ambazo zinaweza kuingia katika milango ambayo sio rasmi ya serikali. Kwa hivyo, Waziri wa Biashara ana kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba pamoja na sheria hii ya kuweza kuweka viwango vya kila kitu lakini bado tuna kazi kubwa sana kuzuia milango yetu na yapatikane mahusiano mazuri baina ya Zanzibar na Bara kuhakikisha kwamba baadhi ya vifaa vinavyoingia ni vizuri na vya kutosha.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nizungumzie, mimi naamini kwa muda mrefu tulikuwa na mtu ambaye tunamwita Mkemia Mkuu wa Serikali huyu ni mtu ambaye anatuhakikishia kwamba maisha yetu ni mazuri. Lakini kwa muda mrefu kulikuwa kunapita maneno kwa maneno kusema Mkemia Mkuu anapasisha vitu ambavyo vyengine haviko katika uwezo wake wa juu, ni vitu ambavyo vinakubalika lakini ni vitu vibaya kwa wananchi kuvitumia. Kwa hivyo, mimi nasema suala hili tokea kipindi kilichopita kwamba Mkemia Mkuu ni vizuri aondoke katika wizara hii, nimesema hivyo kwa nini? Kwa sababu mambo yote yatakayothibitika pale ni kesi na kesi hizo zitakuwa ni za jinai kukipatikana makosa inabidi lazima iwe kesi. Mimi ningeshauri Mhe. Waziri kwamba huyu Mkemia Mkuu badala ya kuweko katika nafasi hii basi apelekwe sehemu nyengine na makosa yote yatakayofika huko yataweza kuamuliwa.

Mhe. Spika, lakini kama kitengo hiki bado kitaachwa katika sehemu hii hapa nina wasi wasi kwamba utekelezaji wake na maamuzi yake yatakuwa ni mazito kwa sababu hapa kilipowekwa sipo mahala pake. Kwa hivyo, mimi ningeshauri kitafutiwe mahala pake kinapohusika hiki kitengo kiweze kufanya kazi zake kwa uzuri zaidi kuliko hapa palivo sasa hivi.

Mhe. Spika, naamini kwamba wananchi wanapenda maendeleo na wananchi wanapenda vitu vizuri na wananchi wanapenda kila jambo lilokuwa zuri. Lakini tuangalie nguo ambazo zinaletwa katika nchi hii, mimi nakumbuka kipindi kimoja hapa zilitaka kuzuia nguo zile nguo za mitumba zisiletwe kabisa. Mhe. Spika, basi wananchi walianza kupiga kelele wakasema hizi nguo mnataka kuziondosha lakini sisi zinatufaa maanake tunanunua kwa bei rahisi na sisi ni wanyonge hatuna kitu.

Mhe. Spika, pia nataka nimkumbushe Mhe. Waziri kwamba pamoja na bidhaa na nguo nayo ni bidhaa ambayo inayotoka nje. Kwa hivyo, kama tunataka kuweka vitu hivi katika viwango vya juu. Je, nini standard ya watu wetu tulikotokezea hali ya kimaisha yao na sisi bado tukiwa katika mchakato wa kusema kwamba tunataka kufanya hali ya kupunguza umasikini katika nchi hii. Mhe. Spika, hapa Mhe. Waziri sijui nini atatwambia kuangalia kiwango cha wananchi wetu na maisha yao na hali yao ya unyonge na kutaka kuwaondosha hakuna mtu anayekataa kutafuta vizuri.

Mhe. Spika, mimi napenda nipate chakula kizuri, nivae vizuri, nilale mahala palipokuwa pazuri. Lakini kwa kuangalia maisha ya jumla ni kwamba hali ya wananchi wetu ya maisha yao ni lazima tuangalie sio kwa kutunga sheria tu, lakini kuitekeleza pengine sheria hii inaweza ikawa ni ngumu sana. Kwa hivyo, ningelimshauri Mhe. Waziri ajitahidi kuona kila upande, upande wa wananchi walivyo na bidhaa zetu zilivyo.

Mhe. Spika, mimi kitu ninachokihofia zaidi ni kwamba wapi Mhe. Waziri atatwambia tukanunue vitu vyetu au vitu vinavyoletwa na watu ambao wanaotoka nje ni mbinu gani zitafanywa ili kuhakikisha kwamba hao wanaotoka hapa wakenda kule nje kununua bidhaa zaidi ya Tanzania basi ijulikane kabla aina ya bidhaa ambazo wanataka kuingia nazo ni standard au sio *standard*.

Mhe. Spika, mimi nahisi mbali ya kuona kwamba katika mswada huu kuna mambo ambayo mengine yamejificha. Kwa mfano, mara nyingi huwa tunapendelea mtu unapokuwa unampa nafasi ya hali ya juu kwa mfano ya Ukurugenzi sio vyema kusema kwamba mtu atateuliwa kwa taratibu zilivyo mtu kama huo ni lazima imuwekee kiwango chake cha elimu. Inatakiwa ijulikane kwamba huyu kiwango chake cha elimu kinafaa sio kusema tu kuteuliwa, utamteuwa vipi.

Kwa hivyo, ni lazima sifa za mtu ambaye anataka kuchaguliwa kama ni Mkurugenzi ni lazima katika mswada huu zielezwe kwamba apatikane mtu mwenye shahada ya kwanza au mwenye shahada ya pili au awe na hiki na hiki, hiyo ndio raha ya mswada. Mswada sio kusema kwamba mtu atachaguliwa na Rais, sasa Rais hujampa vipi amchague hivyo unampa kazi kubwa sana. Mhe. Spika, ni bora kuweka kiwango cha elimu ikajulikana kutokana na nafasi hiyo.

Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa sana kwa hayo nakushukuru sana na mimi nauunga mkono mswada huu asilimia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu uliowasilishwa hivi asubuhi, mswada ambao ni muhimu sana. Mhe. Spika, mimi nilikuwa sina maongezi mengi katika mswada huu nilitaka nitie barka tu na mimi niseme mawili matatu niliyoyaona katika mswada huu. Mhe. Spika, lakini kabla sijaingia katika mswada nilikuwa na utangulizi mdogo.

Mhe. Spika, kwanza nataka niipongeze serikali kupitia wizara hii kwa kuweza kuleta mswada huu japo kuwa wamechelewa kidogo, lakini ndio umefika

kwenye Baraza na sisi tutauchangia na kuupitisha kutokana na umuhimu wake. Vile vile katika kutengeneza sheria, sheria ina mafungu mawili. Kuna kuiunda sheria na kuna kuisimamia sheria. Mhe. Spika, hapa petu tumeshaunda sheria nyingi tu zenye umuhimu sana kwa maisha ya binadamu lakini bado usimamizi wake unakuwa ni mwepesi sana. Mimi nina wasi wasi kwamba na sheria yetu hii tutaipitisha lakini utekelezaji nao unaweza ukaleta matatizo. Kwa mfano, sasa hivi tunaleta sheria hii ya kuona viwango vya bidhaa mbali mbali na takriban mambo mengi yanaharibika kisheria katika miji.

Kwa mfano, utakuta siagi pengine ya kilo moja lakini imepita muda basi utakuta watu wanaouza bidhaa za mikononi badala ya shilingi elfu tano ilipokuwa nzima lakini sasa imeshaharibika wanauza shilingi elfu mbili. Mhe. Spika, watu bado wanaruhusiwa wananunua na wanakwenda kutumia kama kawaida.

Mhe. Spika, mimi naona hili nalo ni tatizo kubwa katika eneo letu la hapa Mjini. Kwa hivyo, ningeshauri sheria hii ikishapita ikasimamiwa pale inapoonekana vijana wa mikononi wanauza bidhaa ambazo hazina viwango kisheria nadhani ichukuliwe jitihada ya sheria ili tuweze kunusurika na matatizo haya.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo wenzangu wamezungumza na mimi ni bora nilizungumze kwa sababu nimeliona kwa macho yangu ni kwamba mambo mengi hapa kwetu ya bidhaa zinakaguliwa na Mkemia Mkuu wa Serikali lakini ukenda kwenye jengo la Mkemia Mkuu wewe mwenyewe utahudhunika.

Mhe. Spika, kwa kweli ukiambiwa huyu ndiye anayeletewa bidhaa kupasisha iliwe ama isiliwe huwezi kuamini, hiyo ghala kwa kweli imejaa mabuibui, ikinyesha mvua huna pakupita kwenda kwa Mkemia Mkuu, bidhaa zile ambazo zinazotaka baridi yeye mwake hamna baridi anakwenda kuweka Chuo cha Afya, Mbweni. Kwa hivyo, siku anayotaka kutizama bidhaa fulani akachukue arejeshe huku. Kwa kweli Mkemia Mkuu bado hatujampa hadhi yake. Sasa naomba kutokana na muundo huu wa sheria ikishapita basi jambo la kwanza tumtengeneze Mkemia Mkuu wa Serikali ambaye ni mhusika mkuu wa sheria hii. Yeye ndiye ataeweza kutwambia hili ndilo na hili silo.

Tunaweza kufanya sheria nzuri lakini msimamizi wa sheria akakosekana itakuwa kazi bure. Sasa nashauri Mkemia Mkuu apewe nyezo, atafutiwe jengo la kisasa, apewe vitu vya kileo ili tuweze kufikia yale malengo yaliyokusudiwa.

Nikitoka kwenye utangulizi huo nije kwenye mswada wenyewe Shemu ya Kwanza Ufafanuzi. Sehemu ya ufafanuzi kuna neno limeandikwe ‘mtengenezaji’, naomba ninukuu Mhe. Spika. Anasema, “Mtengenezaji maana

yake ni mtengenezaji wa kitu au mfumo". Mimi nadhani ukiacha hivi haileti maana, ukisema mtengenezaji wa kitu ama mfumo vitu vinatengenezwa kwa aina mbali mbali kama vile kwa mikono, viwandani, mashine, sasa ukisema mtengenezaji ni kitu na mfumo haikufikia maana. Nawaomba wataalamu wa wizara pamoja na mwenyewe waziri neno hili wangekaa wakazidi kulifafanua zaidi ili mtu akisoma apate maana kamili.

Nikiendelea na mchango wangu katika mswada huu katika ukurasa wa 185 kifungu cha 5, hapa panazungumzia kazi za taasisi, ukija kwenye vifungu (f) na (g) ndio wasi wasi wangu nataka nipate ufafanuzi, naomba pia ninukuu. Kazi ya kifungu (f) anasema, "Kuanzisha, kulinda na kuridhia maabara kwa ajili ya kuweka viwango na kuzuia ubora kwa madhumuni mengine kama inavyoelezwa". Kifungu (g) kinasema, "Kutoa kibali na kuridhia taasisi zilizoko Zanzibar au nje ya Zanzibar ambazo zinajishughulisha na masuala ya kuweka viwango kwa vitu vya mfumo au kukuza ubora wa vitu na mfumo".

Sasa nina wasi wasi kidogo kwamba sheria inasema inaanzisha taasisi ya kuweka viwango, lakini huku inasema itaridhia taasisi nyengine, ina maana ndani ya taasisi hizo watapewa vibali na watu wengine kuweka viwango. Suala langu liko hapa, kwa sababu kila nikisoma sipati maana, sisi tunaanzisha taasisi na imepewa jina rasmi na serikali ambayo itakuwa inahusika na kuweka viwango vya vitu vyote ambavyo vitatumika.

Lakini hapo hapo kuna sentensi inasema inaridhia na taasisi nyengine, ina maana ndani ya taasisi itaanzishwa na taasisi binafsi pengine. Sasa naomba ufafanuzi ili niweze kufahamu madhumuni ya vifungu hivi hapa. Kama kutakuwa na taasisi nyengine watapewa ruhsa au leseni kwa kuweka viwango tuweze kujau na zitakuwa na sifa gani, la kama sikufahamu vizuri basi naomba Mhe. Waziri atapokuja anifahamishe.

Mhe. Spika, nikiendelea nije ukurasa wa 187 Bodi ya Wakurugenzi. Hapa imeelezwa Bodi ya Wakurugenzi, napongeza uundwaji wake kwamba mwenyekiti atateuliwa na rais kwa sifa maalum, mkurugenzi wake halkadhalika. Lakii kifungu (c) kuna wajumbe wametajwa hapa ambao watateuliwa na waziri, naomba ninukuu.

Kifungu (c) kinasema kwamba,

> "Wajumbe wengine watano watateuliwa na waziri kutoka wizara inayohusika na biashara, wizara inayohusika na afya, wizara ianyohusika na kilimo, Aafisi ya Mwanasheria Mkuu na Jumuiya ya Wafanyabiashara".

Sasa na mimi nilikuwa naomba niongeze na Jumuiya ya Wakulima. Kwa sababu hao ndio wanaoajiri watu wengi zaidi katika nchi yetu. Sasa kama kuna uwezekano aongezwe mtu mmoja kutoka Jumuiya ya Wakulima. Yeye anaweza kuleta matatizo yake mengi ambayo sasa hivi yamezuka hasa katika matunda, unaweza ukaiona embe nzima lakini ukiikata ndani mna funza, unaweza kukuta tofaa zima ukilikata ndani unakuta lina funza. Hii imesababisha bidhaa zetu nyingi za matunda zinashindwa kupelekwa nje kutokana na matatizo hayo. Sasa labda na yeye mkulima akipata mwakilishi katika bodi hii anaweza kueleza matatizo yao na yakazingatiwa na yakapatiwa ufumbuzi ili mkulima aweze kugomboka katika kilimo.

Mhe. Spika, baada ya mchango huo nimalizie kwenye ukurasa huo huo kifungu cha tano (5), naomba pia ninukuu halafu nimuombe waziri anipe ufafanuzi.

Kifungu cha 5 kinasema:

> "Waziri anaweza kwa kutoa agizo katika Gazeti Rasmi la Serikali kurekebisha, kubadilisha, kuondoa, kufuta na kuweka mambo mapya au lolote lile katika jadweli hii".

Mhe. Spika, nadhani kuna wenzangu mwanzo walitangulia kuzungumza hivyo, lakini mimi nadhani kama bodi tumeshaipa kazi tena tusipenyeze mambo mengine kabla bodi haijatekeleza kazi hizo. Hiki kifungu sijui kimewekwa sipo au kimeingia kwa makosa, au kimeingia kwa uhakika basi nipewe ufafanuzi kilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nitoe ushauri kidogo kwenye wizara na baadae niunge mkono mswada huu. Ushauri wangu ni kwamba hivi sasa nchini petu pamezuka bidhaa nyingi za kachara zinaletwa kutoka nje, zinaletwa hapa zimeshatumika lakini kwa kuwa sisi wanyonge tunazitumia bidhaa hizo. Lakini ila iliyopo kwenye nchi yetu ni kwamba, nikianza kuleta baskeli kachara mimi leo basi ukikaa miezi miwili watu mji mzima wameleta baskeli kachara na matokeo yake zinashindwa kununuliwa zote na zinabaki kama taka mbovu.

Lakini ukisema naleta friji leo, ama friza au televisheni, ambapo tunaambiwa nyengine zikimaliza mwaka huwa hazifanyi kazi hapa ndio utakuta kila mtu kaleta televisheni matokeo yake hazinunuliwi, pakutupa hatuna. Sasa nadhani serikali kupitia wizara ingetizama mahitaji ya nchi yetu, kwamba je, sasa hivi televisheni zilizopo *recondition* zishakidhi haja? Kama zimeshakidhi haja basi bora sasa hivi tuagize mpya tu mpaka hizi zilizopo zimalizike.

Kwa upande wa baskeli halkadhalika, kama baskeli zimeshakuwa nyingi lakini mpya zipo basi tuangalie je, hizi kuukuu zimeshakwisha ndio baadae kitolewe

kibali cha kuweza kuletwa nyengine. La si hivyo hali itakuwa mbaya kuliko ilivyo hivi sasa.

Mhe. Spika, baada ya mchango wangu mfupi naunga mkono mswada nakushukuru.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Asante Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa hii ya kuchangia mswada huu. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima tukaweza kufika hapa na kujadili mswada huu, kuipongeza serikali na hasa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na uongozi mzima wa wizara kwa kuchukua hatua ya kuleta mswada huu muhimu sana katika kuifanya Zanzibar kufikia lengo lake la kuwa kituo cha biashara katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

Mhe. Spika, kama Zanzibar inataka kufikia lengo lake hilo, basi suala la viwango haliwezi kukwepeka. Kwa sababu huwezi ukawa kituo cha biashara lakini ukawa huonekani kwamba unajali udhibiti wa viwango. Kwa hivyo naipongeza sana serikali na hasa wizara kwa hatua hii muhimu sana katika kufikia malengo yetu hayo.

Kama walivyosema wenzangu Mhe. Spika, tatizo la kutozingatiwa viwango limekuwa tatizo la muda mrefu sana Zanzibar, tunaamini kwamba kuletwa kwa sheria hii na baadae Inshaallah kupitishwa katika Baraza hili kutasaidia kudhibiti suala hilo.

Sasa Mhe. Spika, mimi nina michango kwanza kuhusu lugha za uandishi na baadae kuhusu baadhi ya vifungu vilivyomo katika sheria hii. Nianze na hili la lugha. Hili Mhe. Spika, naomba nilisemee hapa kwamba tunaomba sana afisi ambayo nafikiri itakuwa ni Afisi ya Mwanasheria Mkuu inayohusika na kutafsiri miswada hii, ijitahidi kidogo kuwapunguzia wajumbe kazi kwa kuhakikisha kwamba tafsiri zinazofanyika zinakwenda sambamba na yale madhumuni yanayoonekana katika miswada ya Kiingereza ambayo mara nyingi huonekana kwamba ndio iliyoandaliwa kwanza.

Mhe. Spika, naomba kupendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha tano (5) katika uandishi, ukisoma Kiswahili kinasema kifungu (5) (1) (a), “kuanzisha, kutangaza, kuendeleza, kubadilisha au kurekebisha muda hadi muda toleo la kiwango cha juu kwa ubora, wingi na sehemu ya vipimo vya kutumika ambavyo vitakwenda sambamba na toleo la wakati katika mfumo wa kimataifa”. Ukiisoma Mhe. Spika, maana yake haiji kirahisi, lakini unaielewa ukiisoma Kiingereza kwamba inatoa shida kwa sababu kwanza hili neno muda hadi muda linatumika mara nyingi, Kiswahili hatusemi hivi kwambamtu

kurekebisha *from time to time* kwamba ni muda hadi muda. Tuseme kila baada ya muda au mara kwa mara kama ambavyo tumezowea.

Lakini la pili hii sehemu ya vipimo au kabla ya hapo niseme kiwango cha juu kwa ubora, hapa Kiingereza neno lililotumika lilikuwa ni *updated version of a standard for the quality, quantity and unit of measurement*. Sasa hapa imetafsiriwa kiwango cha juu kwa ubora, wingi. Mimi nadhani hapa *quantity* si wingi ni idadi, inaweza kuwa ni wingi inaweza kuwa ni uchache. Lakini pia sehemu ya vipimo haitafsisi sawasawa *unit of measurement, n*adhani *unit of measurement* ni aina ya vipimo ambavyo vinatumika. Kwa hivyo, naomba hilo tulirekebishe.

Lakini pale kilipomalizia kinasema, vitakwenda sambamba na na toleo la wakati katika mfumo wa kimataifa ambapo imekusudia kutafsiri *shall been. conferment with the latest version of the international system of unit*. Mimi nadhani ingetafsirika vizuri zaidi ingesema itakwenda sambamba na toleo la karibuni kabisa la mfumo wa vipimo vya kimataifa. Nadhani hiyo inaweza kutafsirika vizuri zaidi.

Halafu kifungu hicho hicho cha (5) (1) (b) kuna neno la Kiingereza pale *quality assurance and certification of commodities.* Sasa *certification commodities* zimetafsiriwa cheti kwa bishaa, mimi nadhani hiki si cheti hasa lakini ni kuthibitisha bidhaa. Kwa hivyo, nadhani ingewekwa hivyo ili ikatafsirika vizuri.

Halafu kuna neno hapa naomba nilitaje hapa halafu linajirejea mara kadhaa katika kifungu cha (5) (1) (c). Kuna neno la Kiingereza limetumika *any material or substance*, ukisoma katika Kiswahili kila pahala pametumika malighafi. Sasa malighafi Mhe. Spika, sio *material substance* malighafi ni *row material*. Kwa hivyo, naomba na hili vile vile hapa na kila pahala lirekebishwe, malighafi haitafsiriki sawa sawa kwa dhamira iliyomo katika tafsiri ya Kiingereza.

Mhe. Spika, ukiacha hayo katika kifungu hicho hicho kwenye kifungu cha (J), yako mengi lakini nayasema yale yaliyoko kwenye hali mbaya zaidi. Kifungu hiki ukikisoma kinasema kukusanya, kuchapisha na kutoa taarifa na mambo mengine ya uwekaji wa viwango. Hapa Mhe. Spika, katika Kiingereza inasema, *collect publish and disseminate information and other material on standardization*. Kwa hivyo, hapa si mambo mengine ya uwekaji wa viwango, lakini inakusudiwa labda matoleo mengine yenye taarifa zinazohusu uwekaji wa viwango.

Lakini hata kule mwisho ilivyotafsisi na kutoa vifaa kwa jamii ili kupata vitu hivyo, hii Mhe. Spika, ndio imepotosha kabisa. Kwa sababu neno lililotumika hapa ni, *to provide feacilities for the member to the public to have access to the materials*. Mimi nadhani ingesomeka kuweka utaratibu unaohakikisha wananchi wanapata taarifa hizo, ndivyo ambavyo imekusudiwa hasa ukiisoma kwa Kiingereza.

Kuhusu mambo ya lugha naomba niishie hapo kwa sababu yako mengi kidogo, lakini mengine naweza nikampelekea kwa maandishi Mhe. Waziri. Lakini sasa nataka niingie kidogo katika baadhi ya vifungu vinavyohusika.

Mimi Mhe. Spika, kwanza nadhani hili suala la uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu kuteuliwa na rais mimi naona ni sahihi na ni utaratibu wa kawaida uliozoeleka. Na ninadhani sifa zimewekwa pale, ukisoma kifungu cha (6) (2) kimetaja mtu atafaa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa ana a, b, na c. Kwa hivyo, kimetaja sifa ambazo mtu huyo anapaswa kuwa nazo na rais anapaswa kuzingatia atapokuwa anateuwa mtu huyo.

Utaratibu Mhe. Spika, nadhani unaeleweka, kuwa mara nyingi kunakuwa na mapendekezo yanayofanywa huku chini mpaka yakafikishwa kwa rais halafu baadae akafanya huo uteuzi. Lakini nililonalo la msingi hasa linahhusu kifungu cha 16 na kitu kama hicho katika kifungu cha 20.

Kifungu cha 16 (3) ukurasa wa 190 vile vile ukisoma kifungu cha 20 (6) hivi ninavyoviona vimekusudia kufanya ni kosa la jinai mtu ambaye amefanya makosa hayo. Naomba nikisome ili nieleweke. Kifungu hicho kinasema, “pale ambapo waziri ametangaza viwango kuwa ni viwango vya lazima, mtu hataruhusiwa kuuza bidhaa yoyote isipokuwa iwe na viwango hivyo au iwe imetengenezwa, imezalishwa, imefanywa au imeundwa kwa mujibu wa viwango hivyo”. Sasa inakataza hapa, lakini hiki kifungu hakiweko wazi kwamba kwa mtu ambaye atakuwa anafanya hivi ilivyokatazwa atakuwa ametenda kosa. Kwa hivyo, nadhani kama madhumuni yalikuwa ni ku-*criminalize* basi hicho kifungu kiseme wazi.

Hivyo hivyo, katika kifungu cha 20 (6) ukurasa wa 191 kinachosema, “endapo bidhaa zilizoingizwa haziko katika kiwango kinachohitajika bidhaa hizo hazitoruhusiwa kuuzwa au kwa matumizi ya ndani na muingizaji au aliyezileta atatakiwa kuziondosha bidhaa hizo ndani ya Zanzibar ndani ya kipindi cha wiki mbili au kuziharibu kama taasisi itakavyoamua. Sasa kitu kikubwa kama hichi lakini baadae hakisemi kama hili itakuwa ni kosa. Mimi nadhani ilikuwa yatajwe haya kwamba ni makosa.

Katika kuhusisha hilo hilo Mhe. Spika, tunapokwenda katika kifungu cha 25 na 26 hapa mimi kidogo napata matatizo. Vifungu hivi viko katika ukurasa wa 193 wa Gazeti mahasusi la Serikali. Kifungu cha 25 kinasema taasisi inaweza kumaliza kosa lililofanywa na mtu chini ya sheria hii au kanuni kwa kumuagiza mtu huyo kulipa faini iliyowekwa kwa kosa hilo ikizingatiwa kwamba mtu hoyo ikaendelea mbele. Sasa napata tabu moja, kwanza kwamba mtu akitenda kosa anaweza kulipishwa faini tu, kwa sababu hakuna ulazima wa kupelekwa mahakamani, tena atalipa faini iliyowekwa hatuambiwi ni faini gani na sheria hii haisemi.

Sasa unapoweka sheria Mhe. Spika, halafu ikaweka *essential* kama hizi ni vizuri katika mfumo wa utawala bora ikawa inaonekana hasa kwamba, kama ni kosa kuna *section* gani na kama ni faini zitajwe hapa. Lakini hata katika jewali ukienda hakuna jadweli inayotaja faini hizi. Faini unazipata katika kifungu cha 26 kwa wale ambao wamepelekwa mahakamani, ndio inataja faini pamoja na kipindi ambacho mtu anaweza kuhukumiwa kwenda kifungoni.

Mhe. Spika, sasa naona mambo mawili, moja hiki kifungu cha 25 nakiona mimi kina uwezekano wa kuja kutoa mwanya hapa watu kupenyeza rushwa. Kwa sababu ukishakuipa taasisi uhuru wa kuamua yupi anashtakiwa na yupi hashitakiwi, na yupi analipishwa faini kwa taasisi tu na yupi anapelekwa mahakamani hapo tunajua mambo haya yanavyofanyika, panaweza pakapita mchezo ambao unaweza kuathiri utekelezaji mzima uliokusudiwa wa sheria hii.

Mimi nadhani Mhe. Spika, kwa pale ambapo pametajwa hasa kwamba haya ni makosa labda na mle ambamo hayajatajwa tungependekeza yatajwe. Nadhani ingewekwa wazi kwamba, mtu huyo atapelekwa mahakamani na siku zake zitakuwa zile ambazo zimetajwa katika kifungu cha 26, tusitoe mwanya huo kwa taasisi kuwa yenyewe ndio inayoamua kwamba yupi apelekwe mahakamani au hapelekwi mahakamani.

Ukiachya hilo Mhe. Spika, kuwa kuna sehemu imenipita lakini inazungumzia kwamba kutapokuwa na mashtaka hayatapelekwa isipokuwa yametolewa idhini yake na Mkurugenzi wa Mashtaka, nitakiangalia baadae. Lakini nilikuwa nasema ni kifungu cha 25(2) kinachosema kwamba, “ikiwa mashauri ya jinai yameanzishwa zidi ya mtu uwezo ulioelezwa chini ya kifungu hiki hautotekelezwa bila ya ruhusa ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai wa Zanzibar”.

Nilikuwa nataka kusaidiwa tu kwamba ninavyoelewa mimi utaratibu tuliouanzisha chini ya katiba na baadae katika sheria, swali lolote linalopelekwa mahakamani linalohusu jinai halipelekwi kama halijaridhiwa na Mkurugenzi wa Mashataka kwa sababu ndiye anayesimamia mashtaka. Sasa je,

kulikuwa kuna haja kwa sheria hii kuweka kifungu kama hicho kwa jambo ambalo tayari katiba na sheria imeainisha?

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, na baada ya kupatiwa maelezo na Mhe. Waziri kuhusiana na vifungu hivyo alivyovitaja napenda kusema kwamba, naunga mkono hoja hii ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Spika na mimi kupata nafasi hii kuchangia mswada ambao unatusumbua kidogo. Ni imani yangu kwamba mswada huu utakapopitishwa mpaka Wizara ya Afya nayo bajeti yake itapungua, kwani wale wagonjwa wa mafigo, miguu kuingia maji, watapungua kwani tutapata mchele au bidhaa ambazo zitakuwa zina kiwango.

Lakini Mhe. Spika, katika hili ningependa kusema kwamba, zitakuwa na athari nyingi moja wapo ni kukosa ajira na baadhi ya wafanyabiashara kufa kabisa. Kwa sababu mitaji ya kuleta bidhaa ambazo zina viwango hawatakuwanayo na wale ambao wanachukua bidhaa ambazo hazina kiwango na wao watakuwa hawana pa kuzipata kwa hivyo, watakuwa hawana la kufanya.

Kwa hivyo, ningependa kuishauri wizara kwamba, katika kufanya hili basi wangekwenda *gradual* wasije wakaingia moja kwa moja serikali ikaja ikapata *grievances* kutoka kwa wananchi na ikawa ni *crisis* ambayo itasababisha kama yale yaliyotokea nchini Tunisia.

Jengine ninalotaka kulisema ni kwamba bidhaa ziko za aina nyingi, kuna zile bidhaa ambazo zinaleta athari moja kwa moja kama bidhaa ya chakula na kuna zile bidhaa kama vile za baiskeli ambazo hazina madhara makubwa. Kwa hivyo, ningeomba tu wizara katika kufanya hivi ikazingatia zile bidhaa ambazo zina athari moja kwa moja zikaanza kuwekewa vikwazo moja kwa moja zikawa hazipo kabisa katika soko. Lakini zile bidhaa ambazo kwa kuwa nchi yetu hasa wananchi wetu kwa vile ni masikini, kipato chao ni kidogo, hawana uwezo wa kuzinunua bila ya kupata hizo ambazo hazina kiwango na athari yake ni ndogo, basi tukawa na mtizamo mwengine.

Mhe. Spika, kwa hivi sasa kwanza labda tungeanza kuziruhusu zikaanza kuja. Kwa sababu mwananchi kama hana basketi hatoweza kwenda shamba kulima itabidi apande daladala ambapo nauli hana. Juu ya hayo niliyoyasema naunga mkono hoja.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kusema machache. Mimi mswada huu nimeshauchangia sana lakini nisiposimama sitamtendea vyema waziri.

Mhe. Spika, kwanza naipongeza serikali kwa kuleta mswada huu na nimpongeze waziri na watendaji wake kwa mswada huu na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujalie tunaomba upite kwa salama ili tupate mafanikio.

Tukija katika huu ubora wa bidhaa na utafiti, kwanza Mhe. Waziri atueleze katika huu utafiti hao watakaotufanyia utafiti tutaweza kuwatoa hapa katika nchi yetu au tutakwenda katika nchi nyengine ili kutizama utafiti wa wenzetu walioufanya na kupata bidhaa bora zitakazoingia katika nchi yetu.

Halafu Mhe. Spika, hizi bidhaa bora hapa nchini petu pamezoeleka kuingia bidhaa ambazo hazistahiki binadamu kuzitumia. Lakini tutasema sijui ni unyonge au serikali inaachia kwa kuwa ni masikini sana.

Mhe. Spika, nitarudi kidogo alikosema Mhe. Suleiman katika mitumba. Ukienda katika mitumba nguo zinazoletwa nyengine hata hazistahiki kuvaa mwanadamu, tunaletewa mpaka nguo za ndani kuja kuuzwa, sasa tujiulize tuko radhi sisi kununua nguo kama zile na tukazifaa wala hatujui zinakotoka? Na serikali mambo haya wanayaona wala hayakemewi, vitu vyengine kuingia katika nchi ni madhara makubwa.

Halafu katika hawa wanaoleta bidhaa mimi namshauri Mhe. Waziri, kwa sababu matajiri wanataka wapate wao tu hawataki wapate wenzao. Tajiri mmoja yeye ndiye atakaeingiza hapa vitu kwa kumbana tajiri mwenzake na akiona mwenzake anataka kufanya bidhaa yeye atarudisha chini bidhaa ile ili ambane mwenzake. Kwa hapo tunasema matajiri wanaoingiza vitu na vikikamatwa vitu vile havina ubora wa kuingia, basi mtu huyo apigwe faini kubwa na adhabu. Kwa sababu huyu ndiye anayeingiza wale wafanyabiashara wadogo wadogo wakenda pale kuchukua.

Kwa mfano ana biashara yake yeye ya shilingi laki tano anakwenda pale anauziwa vitu rahisi anakuja kuuza, halafu akikamatwa yule akipewa adhabu ni kuonewa, adhabu itoke juu kwa mwenye kuleta vitu ambao ni matajiri.

Halafu Mhe. Spika, tunaloliona kubwa katika nchi yetu kwa sababu huu utafiti kwanza mimi nina wasi wasi kwamba ukija labda utatugusa mpaka majumbani, tunalima Mhe. Spika. Sisi tunalima mihogo, mipunga, ndizi, tujue katika ule ubora wa bidhaa utakaokuja ili tusije tukaathirika, patangazwe mapema wananchi wajue kuna nini na tujue tuna viwango gani vitakavyoingia katika nchi na kuja kufanya utafiti. Tusije tukafanyiwa utafiti mara moja tukaja tukaambiwa muhogo haufai, mtu atakuwa hana chakula, au ndizi hii haifai ukachukue ndizi Bukoba, pengine bora hii iliyopo hapa kuliko itakayokwenda kuchukuliwa huko Bukoba. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri utapopita mswada huu basi matangazo ni muhimu sana kwa wananchi.

Mimi nilikuwa nataka nisimame kidogo tu, kwa kuunga mkono mswada huu na nimuunge mkono waziri utakapopita huu basi awe na himaya katika vitu vingi kukaguliwa. Hapa tutapopata huyo Mkemia Mkuu Mhe. Spika, basi awe na uwazi, sio akifika pale anataka kwenda kukagua akakagua kitu kimoja chengine aseme siku ya pili kuwa hiki kibovu lakini chengine kinafaa. Biashara ni ile ile, kontena ni lile lile, lakini patakuja unga wa ngano atasema unga ule polo nne ni mbovu na kumi ni nzima, haya ilikuwaje ata ikawa yanageuka mambo hayo. Kwa hivyo tunaomba wawe wawazi, tunatiliwa vyakula vibovu Mhe. Spika na tunaodhalilika ni sisi wananchi. Kwa sababu watu waliokuwa masikini sana wakifika pale wao wanajikumbia tu.

Mhe. Spika, mimi wameshanikuta mara moja hivi karibuni. Nilikuwa na hitma nimekwenda kununua maboksi ya biskuti tunakuja kuzifungua biskuti zinatoka mafunza ni mbovu zote zilifukiwa, hasara si ndogo huna tena vya kufanya watu wote ushawaweka pale uwanjani. Tunawatuma watu pale kukimbilia kwenda kuchukua halua. Kwa hivyo, tuwe *serious* katika vitu vinavyoingizwa nchini kwa sababu vitu vinaingia kinyemela wala havijulikani.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru na naunga mkono mswada huu mia fil mia. (*Makofi*)

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mswada uliopo mbele yetu. Mhe. Spika, pia niishukuru serikali pamoja na Mhe. Waziri kwa kuanzisha mswada huu wenye lengo jema na dhamira nzuri. Kwa sababu kila mtu anatambua kwamba bidhaa bora ni afya bora.

Mhe. Spika, mimi nina michango miwili, mchango wa kwanza ni kifungu cha 8 (1) na (2) naomba kunukuu:

Kifungu cha 8 (1) “Kuanzishwa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Viwango ya Zanzibar ambayo itakuwa na dhamana ya usimamizi wa kazi za Taasisi”

Kifungu cha 8 (2)“Bodi itakuwa na wajumbe:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;
(b) Mkurugenzi Mkuu; na
(c) Wajumbe wengine watano watakaoteuliwa na Waziri kutoka Wizara inayohusika na biashara, Wizara inayohusika na Afya, Wizara inayohusika na Kilimo, Afisi ya

Mwanasheria Mkuu na Jumuiya ya Wafanyabiashara ya Zanzibar.”

Mhe. Spika, maoni yangu kwamba mimi naona kuna haja ya kuongeza kifungu chengine cha kuteua mtu mwengine ambaye ataonekana anafaa. Kwa sababu inawezekana Mhe. Waziri ikawa kuna mtu anaonekana anafaa na ana uwezo wa kumuingiza katika bodi lakini kama hayumo katika taasisi hizi kwa mujibu wa sheria atakuwa hana uwezo wa kumuingiza. Kwa hivyo,
nadhani kuna haja ya kuongeza kifungu cha mtu ambaye ataonekana anafaa kuingizwa katika bodi hii ama awe katika taasisi au awe nje ya taasisi zilizotajwa katika kifungu hichi.

Mhe. Spika, mchango wa pili nataka kuchangia katika suala zima la faini kifungu cha 26 (3). Mhe. Spika, sheria zetu nyingi mara nyingi tunapoziunda basi zinakuwa zinachukua muda mrefu. Sasa tunakuwa tunaweka faini lakini faini ile baada ya muda unaikuta ile thamani ya pesa imeshashuka na lengo na dhamira ya faini ni kutokomeza yale mambo maovu.

Mhe. Spika, hata hivi sasa kuna sheria zetu unazikuta mtu anakwenda kutozwa faini ya shilingi elfu moja. Kwa wakati ule ilikuwa inastahiki lakini kwa wakati huu unaikuta kwamba ile faini ya shilingi elfu moja haina uzito. Sasa kama haina uzito mtendaji wa kosa anakuwa haoni tabu kuleta ile bidhaa kwa wakati huo wa baadae kwa sababu hata akibainika atakuwa haoni tabu kutoa ile pesa ambayo thamani yake ni ndogo.

Sasa kwa maoni yangu Mhe. Spika, mimi nilikuwa naona baada ya kutaja ile thamani ya pesa basi tungeweka asilimia ya ile biashara yenyewe. Kama ni biashara ya shilingi milioni tano basi iwe asilimia 25 ya bidhaa yake ndio itakuwa ni adhabu kwa yule mtenda kosa. Hii itasaidia kwenda na ule wakati wenyewe na thamani ya pesa yenyewe vile ilivyo. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja, ahsante.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu. Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha mswada huu ambao ni kero katika kisiwa chetu cha Zanzibar.

Mhe. Spika, nataka tutambue kwamba watu kutumia vitu ambavyo havina viwango ni kutokana na hali zetu za unyonge na umaskini ndio unaochangia kwa kiasi fulani. Mhe. Spika, tutazame huu mchele wa mapembe tunaoutumia si kwa sababu michele mingine haipo, michele ipo mizuri ambayo anastahiki kula binadamu.

Mhe. Spika, pia naomba nimwambie Mhe. Waziri atambue kwamba katika kisiwa chetu cha Zanzibar tumezungukwa na bahari, kwa maana hiyo kutakuwa kuna njia nyingi ambazo zitasababisha kuingia bidhaa zisizokuwa na viwango na zitatumika katika nchi hii.

Mhe. Spika, vile vile nimuombe Mhe. Waziri kutokana na mswada huu basi wananchi waelimishwe kuhusu suala hili la kutumia vitu vyenye ubora. Kwa sababu elimu pia inachangia kuwa watu hawana habari pengine anapotumia kitu hichi kinaathiri kiasi fulani. Kwa hiyo, namuombea dua Mhe. Waziri mswada wake huu wajumbe waupitishe kwa asilimia kubwa na mimi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, ahsante.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuchangia katika mswada huu muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Mhe. Spika, kwanza naomba niipongeze sana serikali kwa kufanya maamuzi ya kuleta mswada huu katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, pia nimpongeze sana ndugu yangu hapa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuleta mswada huu katika muda huu. Nampongeza kwa kuwa waziri wa mwanzo kuleta mswada katika awamu hii ya saba. Kwa kweli mswada wake umekuja wakati muafaka. Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando ambao nawawakilisha hapa Barazani naunga mkono mswada huu. (Makofi)

Mhe. Spika, mswada huu una umuhimu mkubwa sana. Wenzangu wengi wamezungumzia bidhaa ambazo zinaletwa na ubora wake. Sasa mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri na serikali kwa jumla kwamba mswada huu sio tu utadhibiti bidhaa zinazoingia nchini, lakini pia utadhibiti bidhaa zinazozalishwa nchini. Maana na hilo ni jambo muhimu sana.

Mhe. Spika, katika maendeleo ya uchumi ambayo tunakusudia basi kuwa na viwango katika bidhaa zinazozalishwa ni jambo la msingi sana. Wawekezaji wa nje hawawezi kuja katika nchi kuwekeza fedha zao nyingi ikiwa nchi yenyewe haina utaratibu wa kuweka viwango vya bidhaa zinazozalishwa maana zitakosa soko kule ambako wanalenga kuuza.

Mhe. Spika, hata katika sekta ya mifugo na uvuvi utakapopitishwa mswada huu utawasaidia sana wafugaji na wavuvi wetu. Hivi sasa bahati nzuri Mhe. Spika, tuna mahoteli mengi, lakini unapoangalia katika mahoteli yetu maziwa yanayotumika, mayai yanayotumika sio yale ambayo yanazalishwa ndani. Wenye mahoteli wanahofia kutumia maziwa na bidhaa nyengine za mifugo za ndani kwa sababu hazina utaratibu wa kuwekewa viwango.

Mhe. Spika, kwa wenzetu mayai yana-expire, kwetu sisi mayai huwa tunayatumia mpaka yale ambayo yana mtoto. Sasa hili ni jambo ambalo haliwezi kukubalika katika biashara. Kwa hiyo, upitishwaji wa mswada huu utaraghabisha sana wawekezaji wa sekta ya mifugo waje Zanzibar wawekeze katika uzalishaji wa mayai, maziwa, nyama wakijua tu kwamba baada ya kuzalisha kuna taasisi ya viwango inayoshughulikia bidhaa zao ili iweze kupata soko katika mahoteli yetu na masoko ya nje. Sasa hili ni jambo zuri na kwa kweli litakuwa na mapinduzi makubwa katika sekta ya mifugo.

Lakini pia Mhe. Spika, hata sekta ya uvuvi wawekezaji nao watapata nafasi sasa ya kuja kutusaidia katika uzalishaji mkubwa wa bidhaa za baharini. Kwa sababu katika ulimwengu wa leo huwezi kuzalisha katika kiwango kikubwa kama bidhaa yako hasa ya mambo ya bahari haina code ambayo inatolewa na taasisi ya viwango.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu kwa sababu naamini kwamba wafugaji na wavuvi wa Zanzibar kwa kupitishwa mswada huu sasa watakuwa na chombo ambacho kinasaidia kuona kwamba shughuli za uzalishaji wao zinawekewa viwango ili iwe rahisi kuweza kupata soko la uhakika la bidhaa zao.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja kama nilivyosema na nampongeza sana Mhe. Waziri na namtakia kheri katika usimamizi wa mswada huu, ahsante. (Makofi)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nikushukuru na mimi kunipa nafasi hii nikazungumza machache sana. Mhe. Spika, kwanza nataka niipongeze sana serikali kwa kuweza kusikia kilio cha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, tumekuwa tukilalamika kwa muda mrefu kwamba nchi yetu baadhi ya wafanyabiashara wetu wamekosa uzalendo kwa kuleta bidhaa ambazo zimekosa viwango. Suala hili tumelipigia kelele kwa muda mrefu na kuna kipindi niliwahi kuleta kasheshe Barazani wengine wakatishiwa amani. Lakini tunashukuru kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kwamba serikali imesikia kilio cha wananchi.

Kwa sababu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndio watetezi wakubwa wa wananchi, bila ya sisi basi wananchi hawana msemaji. Kwa hiyo, tunaishukuru sana serikali kwa kusikia kilio cha wananchi kwa muda mrefu na sasa hivi tunashukuru utekelezaji wake tunategemea utaanza.

Mhe. Spika, sitaki nianze na bidhaa tu zinazoletwa nchini lakini nataka nizungumzie hata bidhaa ambazo Zanzibar tunazipeleka nje ya nchi. Mhe. Spika, nakumbuka katika kipindi cha mwanzo mwanzo hapa ilipotangazwa "Zanzibar njema atakaye aje" kwa kweli walikuja watu wengi kuja kutaka kuwekeza. Lakini vile vile kwa kuwa uhuru ulitolewa kwa Wazanzibari na wao wana bidhaa zao kusafirisha nje.

Mhe. Spika, tulikuwa tunashuhudia hapa maembe masusu kwa masusu utayakuta pale uwanja wa ndege yanasafirishwa kupelekwa nje. Tuliwahi kupeleka ndizi za mkono mmoja na bidhaa nyengine mbali mbali hasa katika nchi rahisi kufanya biashara kwa kipindi hicho ilikuwa ni Dubai. Kwa bahati mbaya sana, kwa kuwa tulikuwa hatuna udhibiti wa viwango kwa bidhaa zetu matokeo yake wakulima walianza kukosa soko. Mhe. Spika, ilifika pahala susu la embe ilikuwa kulipata lina kazi kwa sababu tayari kuna wafanyabiashara wanapeleka nje ya nchi.

Lakini Mhe. Spika, kutokana na kwamba hatuna utamaduni wa viwango, sisi tunaona ikishakuwa nyekundu ndio inaliwa. Sasa ile embe baada ya kusubiriwa kuiva maana yake sitaki nitumie lugha mbaya lakini inawezekana mfano huo, wakulima wetu walikuwa wanatumia embe kuzibaka. Kwa nini nikasema kuzibaka, maana yake wanazilazimisha kuliwa kabla ya wakati wake. Mhe. Spika, embe zilikuwa zinachumwa changa zinapigwa moto, zinatiwa kwenye masusu, zinapelekwa Dubai.

Matokeo yake Mhe. Spika, kwa kuwa wenzetu wanajua kula, maana yake kujua kula ni kujua kile unachokila na kuangalia afya yako. Kwa sababu tusiangalie umaskini tu, unaweza ukawa maskini lakini ukanunua bidhaa ambayo inakuzidisha umaskini. Kwa ajili ya umaskini wako ukanunua bidhaa mbovu afya yako itaanza kuathirika. Pesa badala ya kununulia chakula na watoto kuwanunulia sare za skuli itabidi sasa ununue madawa ya kujitibu wewe mwenyewe. Kwa hiyo, wenzetu kule wakaanza kuzuia embe zetu zikawa hazitakiwi.

Sasa mfanyabiashara mmoja alisababisha na wengine kuweza kukosa soko. Kwa hiyo, suala la viwango tusiangalie tu labda kwa bidhaa zinazoletwa, hata na bidhaa ambazo Zanzibar inasafirisha kupeleka nje hasa bidhaa za vyakula na nyengine, basi kama tutakuwa tunapeleka biashara ambazo hazina viwango inawezekana ndio tukawa tunaizibia soko.

Mhe. Spika, Mhe. Said Ali Mbarouk alizungumza hapa kwamba katika mambo ya biashara haya kuna *code*, ina maana *code* fulani inajulikana hii bidhaa inatoka pahala fulani. Maana yake bidhaa ile ikiwa mbaya basi tayari

umeshaharibu biashara yote. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuweka viwango katika suala zima la biashara.

Mhe. Spika, nikizungumzia suala la viwango sio kama kwa chakula tu lakini hata bidhaa nyengine. Kuna baadhi ya waheshimiwa wamezungumza hapa ni kweli. Nadhani sasa hivi kama serikali itafanya utafiti wa kina basi maduka mengi yenye bidhaa za *electronic* itabidi zipigwe doza. Mhe. Spika, tumeshuhudia wenzetu Tanzania Bara bidhaa zinafuatwa ndani ya makontena zinatolewa zinapigwa doza. Kama walivyosema wenzangu kuna TV wakati mwengine, kuna kompyuta na bidhaa mbali mbali kwa sababu sasa hivi watu wanatafuta kila kitu cha rahisi.

Mhe. Spika, mimi nadhani wakati umefika sasa hivi hebu tujitahidini kwa umaskini wetu tujilinde, maana yake kisiwe kisingizio cha umaskini tukaiharibu nchi yetu. Sasa hivi ni wakati muafaka kabisa wa kuweza kuhakikisha kwamba Zanzibar na sisi angalau kuna bidhaa zinazokuwa na ubora.

Mhe. Spika, ukiangalia hata wafanyabiashara wa Zanzibar biashara zao nyingi sasa hivi zinatoka China. Biashara nyingi zinazotoka China sitaki kuharibu jina la China lakini tunazungumza bidhaa zinazoletwa. Sasa na wao wenyewe sijui huko kwao hawana udhibiti wa viwango kwa bidhaa zinazosafirishwa nje au vipi.

Kwa sababu mimi najua katika nchi yoyote kuna bidhaa ambazo hizi ni *export* na kuna bidhaa ambazo zinakuwa ni za ndani. Sasa sijui China wao kule hawana utamaduni wa kuweka viwango vya zile bidhaa zinazotoka katika nchi yao kuja katika nchi nyengine. Sasa hii kwa sababu kama watakuwa na wao wenzetu wanaachia inaweza hata ikaharibu na hilo soko lao.

Mhe. Spika, sasa hivi kuna simu za mkononi na nyingi zao ukiziangalia zinatoka China, akinunua mtu baada ya miezi 6 hata yale maandishi ile namba 1, 2, 3, 4, 5 unakuta zimeshafutika. Sasa Mhe. Spika, hizi ndio bidhaa ambazo hazina viwango na tunaziruhusu zinaingia katika nchi yetu. Kwa kawaida bidhaa kama hizi utazikuta zinauzwa shilingi ishirini elfu mpaka arubaini elfu.

Mhe. Spika, kwa mnyonge ataona ile ndio bidhaa rahisi lakini kumbe yule ndio tajiri. Kwa sababu huyu ambaye anaitwa tajiri ambaye anaweza kumiliki kununua simu ya shilingi laki moja anaweza akakaa nayo miaka mitatu, lakini huyu aliyeinunua simu kwa shilingi elfu thalathini isiyokuwa na kiwango kila baada ya miezi 6 inabidi apate simu nyengine mpya ile biashara inakuwa kubwa. Sasa hapa sijui nani aliyekuwa tajiri na nani maskini.

Kwa hiyo, hapa mimi nadhani tuangalie katika maeneo yote. Kama alivyosema Mhe. Raya Suleiman Hamad pale kweli wakati mwengine tunawaonea wafanyabiashara wadogo wadogo. Mtu amekwenda katika duka la jumla amenunua pengine mchele, unga au sukari lakini anakuja kukamatwa yeye na anayekamatwa na ngozi ndio mwizi. Matokeo yake bidhaa pale tuseme paketi 40 zinateketezwa lakini yule aliyeleta bado anaendelea ku-survive.

Hata akenda kule hakuna compensation, au hawezi kusema kwamba wallahi ile bidhaa niliyokuuzia tayari imeshatupwa basi chukua hii nakukopesha angalau uanze kidogo kidogo. Kama kenda benki kakopa tena ndio mzee ngoma inamsubiri Mahakamani.

Mhe. Spika, nataka nimalizie la mwisho. Mhe. Spika, kuna lugha imekuwa inazungumzwa sana kidogo mimi siifurahii kwa sababu naweza nikasema haimtendei haki pengine mfanyabiashara, au haitendei haki ile bidhaa nyengine, au haiwatendei haki hata wale wananchi ambao wanatumia. Mhe. Spika, sasa hivi unapozungumza chakula kibovu yanazungumzwa mapembe. Sasa waziri akija hapa atwambie mchele wa mapembe haufai kuliwa? Kwa sababu wananchi wetu sasa hivi wanakuwa na hofu.

Mhe. Spika, mimi ninavyojua mapembe ni nembo ambayo ilikuwepo katika mchele uliokuwa unaletwa na mfanyabiashara. Hata Chimbeni alikuwa anatangaza katika matangazo yake, kuna mapembe ya kijani na mapembe mekundu. Wengine walikuwa wanavutiwa na rangi ya vyama vyao, CCM wananunua mapembe ya kijana, CUF wananunua mapembe mekundu. Lakini sasa hivi imekuja lugha kwamba ukitaja mapembe ina maana mchele mbovu. Mimi nadhani lazima tuitendee haki bidhaa na wafanyabiashara.

Mhe. Spika, kwa kuwa nimemuuliza swali waziri sitaki nilijibu. Maana yake mimi nilitaka nitoe ufafanuzi mchele gani mbovu lakini unaposema mapembe je, ina maana mchele wote ule mapembe tunaokula ulikuwa mbovu. Sasa kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri wa Afya hapa itabidi sote tukapange foleni tukapime maana tumeula kweli kweli na wananchi wetu wameanza kujenga hoja.

Mhe. Spika, wananchi wakipewa kauli na Mhe. Waziri kwamba mchele wa mapembe ni mbovu au mchele wa mapembe ulikuwa si mbovu. Hata basmati inaweza ikawa mbovu.

Lakini hata tende Mhe. Spika, unakwenda pale Darajani unanunua tende inatoka unga. Mhe. Spika, tende inatoka unga na mwezi wa Ramadhani ndio kama hivyo inavyosemwa mtu akishaona pale tende imeshaanza ku-expire basi kama kilo shilingi elfu moja unauziwa shilingi mia tano. Sasa kwa yale

tunayosema kwa kuwa mimi najiona mnyonge nakimbilia kwenye ile kilo shilingi mia tano, lakini huo umaskini wako unakula tende mbovu baada ya wiki tatu hospitali unapimwa pressure juu, mara sukari, mara figo.

Kwa hiyo, kuna vitu vingi ambavyo vinakuwa vibovu lakini tusizungumze tu suala la chakula. Kuna bidhaa nyingi ambazo hazifai kutumiwa na binadamu lakini vile vile zinazidisha umaskini nyengine. Kwa sababu ukinunua bidhaa tuseme electronic kama haina kiwango baada ya muda mfupi inabidi kifaa kile ubadilishe. Au wakati mwengine Mhe. Spika, shoti za umeme zinatokezea kutokana na ule waya unakuwa hauko katika kiwango.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja, ahsante.

Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Haji Faki Shaali): Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipatia fursa hii kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu.

Mhe. Spika, nataka niungane na wenzangu kumshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote katika wizara hii kwa kutuletea mswada huu ambao utatusaidia katika mambo mawili makubwa. Kwanza kuinua kiwango cha biashara katika nchi yetu, lakini pili utalinda afya za wananchi wetu. Naona hayo ndio madhumuni mawili makubwa ya mswada huu. Una madhumuni ya kibiashara lakini pia una madhumuni ya kiafya. Kwa hivyo, ni mtambuka kwa kweli.

Mhe. Spika, kwanza imani yangu kwamba mswada huu utasaidia wafanyabiashara lakini pia utasaidia wasiokuwa wafanyabiashara. Nadhani ndio Mhe. Waziri katika tafsiri akaweka bidhaa na kitu. Kwa sababu bidhaa ni ile inayokusudiwa kwa ajili ya biashara, kitu inawezekana mimi nimechimba kisima changu nina maji yangu mwenyewe natumia katika nyumba yangu, lakini naweza nikayachukua nikayapeleka kwenda kupimiwa je, maji haya yametimiza viwango. Sasa kwa sababu sijakusudia kwenda kuuza huwezi kuita bidhaa hiyo itakuwa ni kitu.

Nadhani kwa tafsiri ya kisiasa ndio ninavyofahamu kwamba bidhaa ni ile iliyokusudiwa kuingia katika soko kwa ajili ya kuuzwa, lakini kitu ni kile ambacho pengine mwananchi anakwenda mwenyewe kupimiwa kuona tu kwamba kiko salama au hakiko salama. Sasa ile huwezi ukaiita bidhaa hicho ni kitu. Ukichukua kwa tafsiri ya *Carl Max* katika *Capital ile Volume I Commodity and Material.*

Mhe. Spika, la pili na mimi nataka niungane na Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba sheria hii itasaidia sana wafanyabiashara wetu ambao wamepata

kikwazo kwenda kuuza bidhaa nje kwa sababu hatuna viwango bidhaa zetu hazikubaliki.

Mhe. Spika, Pemba hasa ukanda wa mashariki sasa hivi wananchi wanazalisha chumvi kwa kiwango kikubwa. Lakini bado ukenda katika mikahawa na hoteli hapa Zanzibar chumvi inayotumika ile ya unga ni kensalt kutoka Kenya. Lakini hii chumvi inayozalishwa kutoka Pemba ambayo pia na Unguja sasa hivi naona wamekwenda Pemba kule kwenda kupata utaalam naona inazalishwa. Kuna mtaalam mmoja mzuri sana na nafikiri Mhe. Waziri huyu kijana atamfuata anaweza akamsaidia sana maarifa katika masuala haya. Yuko mtaalam mmoja Pemba naona ana shahada ya pili ya mambo ya *chemical industry*, huyu ndie anayewasaidia hawa wakulima wa chumvi.

Wamejaribu kuji-*organize* wenyewe pale, wamepata misaada ya mitambo ya kutilia madini joto na kwa kweli chumvi yao sasa hivi huwezi kusema kwamba inatimiza viwango lakini wenyewe wana *reagent* zao za kujaribia. Hata katika maonesho waliyokuja Baraza la Wawakilishi mara mbili wametupa chumvi, wametupa reagent zile za kuweza kuijaribu kama ile chumvi madini joto yamo au hamna, mimi mmoja niliwahi kupata mambo hayo. Lakini nafikiri itakapokuwa pana taasisi inayokubalika kisheria ya nchi basi itakuwa hakuna haja tena kukupa *reagent* wale. Kwa hivyo, nadhani ile chumvi itaweza kusafirishwa katika masoko ya nje.

Lakini leo hapa mwenye hoteli gani atakayekubali kutumia chumvi ile ambayo haina uthibitisho wowote wa chombo kinachokubalika. Sasa mimi naona hii itakuwa ndio ukombozi mkubwa sana kwa wazalishaji wa chumvi na nadhani soko la chumvi la ndani basi itakuwa tumejikomboa. Wakati tunatafuta juhudi ya kuhamasisha wakulima wa mazao mbali mbali lakini kwa hili suala la chumvi ambalo mimi nimeona inazalishwa kwa wingi nasema angalau tutakuwa tumepiga hatua kujikomboa.

Mhe. Spika, ukisoma historia ya Zanzibar utaona kwamba Zanzibar ilikuwa na jina kubwa la biashara duniani. Lakini kama mwanafalsafa mmoja Bwana *John Craw* anavyosema naomba kunukuu: *"It takes twenty years to build reputation and five minutes to ruin it"*. Kutengeneza jina zuri inaweza ikakuchukua miaka ishirini lakini kuharibu lile jina ni dakika tano tu kwa mujibu wa mwanafalsafa huyu.

Sasa kwa mujibu wa Mhe. Hamza Hassan Juma alivyozungumza ndivyo kweli ilivyojitokeza. Jina zuri la Zanzibar lililojengwa kibiashara siku za nyuma kwa kusafirisha karafuu zenye ubora, haidhuru wakati huo duniani ilikuwa hakuna mambo ya viwango, ilikuwa viwango watu wanaangalia kwa macho tu kupimia mambo. Lakini kutokana na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu basi lile

jina la Zanzibar kwa kweli likaondoka. Hata kuna baadhi ya wafanyabiashara wengine walikuwa wanasafirisha karafuu magendo Kenya hapo walikuwa wanatia michanga, wanatia kwenye maji, wakazidisha vile vile kubomoa jina zuri la Zanzibar.

Kwa hivyo, lile jina lililojengwa kwa miaka 20 kama alivyosema huyu Bwana John Craw basi liliharibiwa kwa dakika 5. Sasa imani yangu kwamba hii taasisi ya viwango itaweza kurejesha jina zuri la Zanzibar kwa miaka mitano, sio kwa miaka 20 kama alivyozungumza Bwana John Craw. Ndani ya miaka mitano Zanzibar inaweza jina lake likarudi wala isifike miaka 20 kujenga reputation kama alivyosema huyu bwana. Kwa hivyo, nashukuru sana kwamba Mhe. Waziri kwa kweli kaja na ukombozi mpya wa biashara na afya zetu.

Mhe. Spika, mimi kwa sababu nimeshapata fursa nyingi za kuchangia mswada huu nimesimama kwa madhumuni ya kuunga mkono, ili na mimi nionekane katika hansard kwamba nimeunga mkono mswada huu. Mhe. Spika, nakushukuru na naunga mkono mia kwa mia. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Haji Faki Shaali, Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum. Nafikiri muda hautoshi tutaendelea jioni.

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuahirisha kikao hichi kuna matangazo matatu. Ndugu zetu wa Idara ya Vitambulisho wametuletea taarifa kwamba baadhi ya picha tulizopiga Waheshimiwa Wajumbe hazikutokeza vizuri. Kwa hiyo, wapo nje *reception* hapo ili kurekebisha kwa kupiga tena picha za baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe ambao hazikutokeza vizuri. Ya kwangu imetoka vizuri sana. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, waheshimiwa wafuatao wanaombwa wakarudie tena kupiga picha pale. Nao ni:-

1) Mhe. Salma Mussa Bilal,
2) Mhe. Shadya Mohammed Suleiman,
3) Mhe. Nassor Salim Ali,
4) Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban,
5) Mhe. Farida Amour Mohammed,
6) Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi,
7) Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi,
8) Mhe. Dk. Sira Ubwa Mamboya,
9) Mhe. Raya Suleiman Hamad na
10) Mhe. Amina Iddi Mabrouk.

Wanaombwa wakarudie tena kupiga picha hapo.

Tangazo la pili mara baada ya kuahirisha kikao hichi Waheshimiwa Wajumbe kutoka Chama cha Mapinduzi wanaombwa wabaki humu ndani kutakuwa na mkutano. Nimeombwa na nimekubali watumie ukumbi huu kwa huo mkutano.

Tangazo la tatu tunayo Jumuiya ya UWAWAZA yaani Jumuiya ya Wawakilishi Wanawake katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar na ni msimu - wao kufanya uchaguzi wa viongozi wa jumuiya hiyo. Fomu tayari zimeshachukuliwa na kwa hiyo wanaombwa wote wale waliochukua fomu kugombea nafasi mbali mbali kwamba kesho itakuwa ni siku ya mwisho kurejesha fomu hizo. Haikutajwa saa ngapi lakini ili mradi kesho wale waliochukua fomu kugombea nafasi za UWAWAZA wanaombwa fomu hizo wazirejeshe kesho ndio mwisho.

Nakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe, baada ya matangazo hayo sasa naahirisha kikao hichi hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 6:58 Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum: (Mhe. Machano Othman Said): Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii ya leo kufika hapa Barazani.

Pia nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu unaohusiana na uendelezaji, ukuaji na uwekaji wa viwango bora vya bidhaa na usimamizi wa huduma zitokanazo na mswada huu.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mswada huu ni muhimu sana katika kuimarisha huduma zetu za kiuchumi kwa kupitia bidhaa na vitu mbali mbali.

Mhe. Spika, Zanzibar kama nchi kwa muda mrefu hatukuwa na taasisi kama hii lakini kutokana na uono wa watendaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na kwa umuhimu wake katika shughuli hizi za kiuchumi, wizara kwa kupitia Mhe. Waziri wameweza kutengeneza mswada huu ambao ni muhimu sana. Mhe. Spika, mswada huu una umuhimu kwa pande mbili. Upande wa kwanza kwa wazalishaji wa ndani na upande wa pili kwa waagiziaji wa bidhaa.

Mhe. Spika, Zanzibar tunazalisha bidhaa nyengine tunatumia wenyewe na nyengine tunasafirisha, lakini hata zile tunazotumia ndani mfano maji na bidhaa nyengine kama furniture na mambo mengine, huwa zinapata changamoto kubwa kwa watumiaji na zaidi wanaotoka nje ya Zanzibar hata kama wakiwa hapa. Mhe. Spika, changamoto yake inakuja kwamba hazikufanyiwa kuangaliwa ubora wake kwa hapa Zanzibar. Kwa baadhi ya bidhaa ambazo zinazalishwa Zanzibar, inabidi zipelekwe TBS kuangaliwa ubora wake.

Mhe. Spika, ni lazima tujue kwamba TBS sio shirika ambalo lina mamlaka ya kufanya kazi Zanzibar, likiwa linafanyakazi basi ni kwa kuombwa. Kwa sababu TBS ipo kisheria kwa Tanzania Bara, kwa hivyo uwezekano wa kutokutoa kipaumbele kwa Zanzibar ulikuwa ni mkubwa. Ingawa walikuwa wana ushirikiano wa karibu kati ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ya Zanzibar na TBS.

Mhe. Spika, watu wanasema kwamba cha kuazima hakistiri mwili. Kwa hivyo, na sisi ni vyema kuwa na chetu na kwa bahati nzuri hichi sasa ndio chetu. Kwa hivyo, ni lazima tushukuru na tujenge matumaini kwamba taasisi hii inaweza kusaidia uendelezaji wa shughuli zetu za kupima na kuimarisha uchumi wetu.

Waheshimiwa Wajumbe asubuhi walizungumza hapa kwamba bila ya kuwa na kodi ya kibiashara ya ubora basi ni vigumu sana kusafirisha bidhaa. Tulikuwa tunawasikia watu kwamba tuanzishe viwanda mfano vya kusindika samaki na kupeleka nje, hata tungekuwa na mamilioni ya tani ya samaki, basi kama hakuna upimaji wa ubora wa hizo bidhaa zenyewe basi itakuwa ni kazi bure, huyo samaki usingeweza kumuuza popote, ungekuwa unaye na ungebidi utumie mwenyewe.

Mhe. Spika, mimi katika miaka ya 1990 nilikuwa ni mfanyakazi wa Shirika la Viwanda vya Serikali. Kwa hivyo, nilikuwa naona zile juhudi zetu katika kutafuta jinsi gani tufanye ili bidhaa zetu ziwe bora. Tulikuwa tukishiriki maonesho kama yale ya saba saba na mengineyo, lakini bado wenzetu walikuwa juu kwa sababu bidhaa zao zina viwango vya kupimwa. Kwa hivyo, na sisi tukianzisha hivi ingawa inawezekana mwanzo wake ukawa mgumu kwa sababu hatujazowea, inawezekana ikawa mgumu kwa wafanyabiashara wenyewe wakaona ni usumbusu au inaweza ikawa mgumu kwa sisi wanasiasa na inaweza kuwa ngumu kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, mimi nawaomba sana kwa pande zote tuvumilie sheria hii iende na ianze kufanyakazi, tuwape mashirikiano, halafu tuangalie faida zake na hasara zake. Lakini mimi naona faida zake zinaweza kuwa kubwa zaidi kuliko hasara.

Mhe. Spika, kwa sababu tumedhamiria kuwa na viwanda vya usindikaji wa samaki, viwanda vya size ya kati na vidogo, basi tukianzisha sheria hii ili tupate mafanikio na wafanyabiashara wetu nao wabadilike, wabadilike waanzishe viwanda, wabadilike waanzishe biashara ambazo zitatoa tija kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, tunaingia katika soko la Afrika ya Mashariki, nafikiri na sisi mlango uko wazi kwa upande wa Zanzibar. Katika soko hili la Afrika ya Mashariki ukizalisha unasamehewa mambo ya kodi na mambo mengine. Zaidi kwa upande wa Tanzania na Uganda, wenzetu Kenya kidogo bado kodi itatozwa kwa kiwango fulani, lakini kwa Tanzania nafikiri tuko kidogo. Kwa hivyo, ni muhimu kwamba tunaanzisha kitu hiki, basi jamii ya Wazanzibari hasa wale wenye uwezo wa fedha, nafikiri ni muda mzuri na wao wa kuanzisha kitu cha pamoja.

Mhe. Spika, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe kwamba hebu na sisi tujaribuni kujikusanya kama watu watano watano au kumi tutafute fedha na tufanye ushirika wa kuzalisha kitu, tusimamie haya mambo ili na sisi tuwe katika uzalishaji, tusiwe watazamaji wa nje tu.

Mhe. Spika, mfano Waheshimiwa Wajumbe watano au kumi wakitoa milioni 50 kila mmoja, yaani wakienda kukopa benki kisha wakizikusanya hizo, basi milioni 500 mnaweza mkafanya jambo ambalo mkaanza kulishughulikia na nyinyi na mkaweza kujiendeleza nyinyi wenyewe, lakini pia nchi yetu ikasonga mbele. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko atupe changamoto na kama kuna milango ya kupita na sisi kuweza ili tuweze kufaidika na shughuli hii.

Pia Mhe. Spika, mswada huu ukipitiswa na nina hakika tutaupitisha, basi tutapata heshima sana katika soko la dunia kwamba Zanzibar sasa na wao wamejitutumua. Pengine katika uanzishaji huu tunaweza kukumbana na tatizo la watendakazi wa hii taasisi, tunaweza kukumbana na vifaa vya kufanyia kazi. Lakini mimi naona hayo yote sio mambo ya kutuvunja moyo, wala sio mambo ya kutukatisha tamaa. Jambo lolote ukilianza ni gumu lakini nina hakika tukianza basi baadae tutakuwa na wafanyakazi wa kutosha wenye ujuzi, lakini pia tutakuwa na vifaa vya kutosha vya kufanyia shughuli hizi. Ingawa na wakwepaji na wajanja watakuwepo, lakini ni shughuli za kawaida.

Polisi wanasema bila ya kuwa na wahalifu basi Jeshi la Polisi litakosa kazi. Hata mahakimu kama hakuna wakosa sheria basi mahakimu watakuwa kule hawana kazi, itabidi tuwe hatuna mahakimu. Kwa hivyo, challenges tutakazozipata katika utekelezaji wa sheria hii ikiwemo pengine upungufu wa

wataalamu wa kutosha, ujanja na maarifa yaliyotuzidi wafanyabiashara. Haya yote tujue kwamba ni mchanganyiko wa kutupeleka mbele.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwamba atakapoanza hizi shughuli basi wafanyakazi alionao ni wazuri, lakini awasisitize kwamba wawe waadilifu sana, wawe waadilifu kwa sababu watakuwa wanachezea au wanashikilia maisha yetu Wazanzibari, katika ubora wa bidhaa na wasiwaumize wafanyabiashara ambao hawana makosa. Wale ambao wamekosa wawaelimishe na waweze kupeleka bidhaa zao kwenye soko ili ziwe nzuri.

Mhe. Spika, nilisoma kama wiki tatu nyuma kwenye sehemu kuwa kuna mfanya biashara mmoja sio Mtanzania, lakini yuko Tanzania anazalisha tomato katika sehemu za Kigamboni, maroli kwa maroli anapeleka sokoni lakini hayako katika viwango. Lakini akiingia mjini basi watu wanayachukua na wanayatumia, wauza chipsi wanauza. Sina hakika kama na Zanzibar hayaingii maana yake Kigamboni na Zanzibar sio mbali, kama yanaweza kufika mikoani kwa nini yasiweze kufika Zanzibar.

Kwa hivyo, mambo haya ndio ambayo yanaturejesha nyuma. Lakini na sisi nina hakika kwamba tunaweza kuzalisha tomato na mambo mengine. Hivi viwanda vidogo vidogo kama cha Mhe. Waziri ni lazima vitiliwe mkazo ili tuweze kuwa navyo. Tusikubali tu kukaa nje ya uwanja tukasema kwamba hatuwezi kuzalisha Zanzibar, tunaweza sana, lakini ni lazima tuwe na mipango endelevu.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi sikuwa na mchango mkubwa kwa sababu nilishawahi kuuchangia mswada huu, maoni yangu nilitoa. Hapa nilisimama kwa kuusaidia tu kwamba mswada huu ni muhimu na kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi kuwa suala hili tulichangie kwa sababu litakuwa lina umuhimu sana katika maisha yetu, kwa upande wa biashara, uletaji wa bidhaa na usafirishaji wa bidhaa.

Mhe. Spika, kuna watu wana ushirika wao wa kusafirisha hizi spices, nafikiri kupeleka Japan na kwengineko. Lakini walikuwa wanalalamika, kwa sababu hapa Zanzibar hatuna haya mambo ya viwango, basi wanapata usumbufu na biashara yao inakwama na wengine watakaoanza kuzalisha watakwama.

Kuna wakati mwengine Mhe. Spika, tunazalisha madirisha sijui yale ya aluminum, tukenda Bara yanaulizwa haya kweli yanatayarishwa Zanzibar, kwa sababu hayana kitu ambacho kinaonesha kwamba yanazalishwa Zanzibar. Mimi nina hakika kuwa tukianza basi kila mmoja atatambua kwamba Zanzibar nako mambo haya yanafanyika vizuri.

Mhe. Spika, zaidi mimi naona nguvu kubwa tuielekeze katika uzalishaji wa ndani. Ule uagiziaji nao ni muhimu kuulinda. Hatuwezi kutarajia tu kwamba tumeunda sheria hii kwa wale waagizaji ili wakamatwe, hapana. Tumeunda sheria hii ili zile bidhaa zetu ambazo zinazalishwa Zanzibar ziwe nzuri, ziwe na ubora na zipate soko. Kwa sababu kama wazalishaji wa Zanzibar wao wanazalisha lakini hawapati soko, basi utakuwa ule uchumi hauwezi kwenda mbele, itakuwa kazi yetu kupokea tu na ukipokea utaletewa chochote kwa sababu na wewe utakuwa huna. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nimalizie kwa kusema kwamba naunga mkono kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chumbuni mswada huu kwa asilimia mia moja. Nakushukuru Mhe. Spika (*Makofi*).

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia mswada huu wa sheria ya kuweka masharti ya uendelezaji, ukuzaji na uwekaji wa viwango na ubora wa bidhaa.

Mhe. Spika, kama tunavyojua kuwa taasisi hii kwa muda mrefu hapa Zanzibar ilikuwa haipo na hali ya Zanzibar katika uagiziaji wa vifaa, kwa vile ambavyo ni muhimu kwa matumizi ya binadamu, ilikuwa hakuna utaratibu wa haraka haraka wa kuona kuwa vifaa hivi kweli vinafaa kwa matumzi ya binadamu.

Mhe. Spika, leo Zanzibar kama tunavyoshuhudia wafanyabiashara wetu kwa sababu ya kutokuwepo kwa chombo hiki, basi wanaingiza bidhaa tu, bidhaa ambazo nyengine bila uchunguzi zikifika tu unajua kuwa hizi ni za kuokota na hizi hazifai kutumika kwa binadamu, kutoka vitu vya kutumia na mpaka vyakula vya kula binadamu.

Mara nyingi Mhe. Spika, ilikuwa kikiingizwa chakula ambacho hakifai kuliwa na binadamu na tukikizungumza na tukipiga kelele. Wakati mwengine Mhe. Spika, tunaambiwa kuwa kimetupwa na wakati mwengine yalikuwa mazingira ndio hivyo hivyo. Hivi sasa naamini katika bidhaa zetu nyingi tulizonazo ambazo tunazitumia, zimo katika hali ya kutisha.

Mhe. Spika, mimi nafarajika kwa makusudi kabisa kupata mswada huu ambao naamini kabisa, sheria hii itakapofanya kazi au itakapoanza kufanyakazi na wataalamu wa kuundwa katika taasisi husika wakikamilika basi Zanzibar itakuwa katika hali ya matumizi ya vifaa ambavyo binadamu anatakiwa avitumie.

Mhe. Spika, ukiangalia wenzetu wa Bara mara nyingi, vile vitu ambavyo sisi wenyewe tunaviona kuwa ni vizuri hapa na tunawania kuvinunua basi kule

vinapigwa moto kabla ya kutumika. Hii ina maana kutokuwepo kwa chombo hiki ni hatari ya maisha yetu.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wake wa chombo hiki, kiwango ambacho kinakusudiwa ni kuwa kiwango hicho kiwe kinamlinda mlaji au mtumiaji dhidi ya hatari kwa afya na usalama wake. Mhe. Spika, hapa anayekusudiwa ni mtumiaji binadamu, lakini kuna baadhi ya vifaa vinaingia katika nchi hii kama ni chakula cha wanyama.

Mhe. Spika, juzi nilipoangalia kwenye TV, kuna nchi moja iligundua kuwa chakula kinachotengenezwa na wanyama ambao ni kuku, basi kina sumu fulani ambayo athari yake ni mpaka yale mayai yenyewe yalikuwa hayafai kwa kuliwa.

Kwa hivyo, katika sheria hii sikuona kumlinda mnyama na chakula anachotengenezewa. Mhe. Spika, ningeomba kujua je, utaratibu huu ukoje, kwa sababu ninahofia tukaja kuathirika kwa kutumia kitu ambacho hakikuingizwa katika utaratibu kwa maradhi ambayo kwa lugha fupi, maradhi yanayopatikana kupitia kwa mnyama mwengine.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha ubora unaokubalika, sisi wenyewe hapa tuna bidhaa ambazo zinatengenezwa sio za kuuza, lakini ni za matumizi ya hapo kwa hapo na kila mtu anatumia kwa ujuzi wake. Kwa mfano, tunajiondoshea ugumu wa maisha kwa kuuza biashara kama juisi kwa wingi na vitu kama hivyo. Je, vitu hivyo vya hapo kwa hapo vitakuwa na utaratibu gani wa kuangaliwa kabla mtumiaji hajaanza kutumia wakati vinatengenezwa kila mahala. Ni kweli hii taasisi inayohusika na kuangalia vitu hivyo, haina uwezo wa kuweza kufanya kazi kwa Pemba na Unguja kwa wakati mmoja kwa wafanyabiashara ambao ni wengi kabisa.

Halafu jengine Mhe. Spika, mimi nimefarajika sana kuona kuwa kama itatokezea kuonekana kuwa kuna bidhaa zimeletwa ambazo ziko chini ya kiwango, basi bidhaa hizi ama zitarudishwa au zitazuiwa kuuzwa na kama ni kuharibiwa basi mwenye kuleta bidhaa basi itabidi alipie gharama zote.

Mhe. Spika, hapa suala langu ni kuwa tunazo bidhaa nyingi sana ambazo ziko chini ya kiwango, na tukitizama nchi yetu ilivyo ndogo sana na ukitizama bidhaa nyengine zilivyo ni bidhaa ambazo kama ukiziweka kwenye ardhi au ukizitia kwenye bahari, basi zinaweza zikaharibu mazingira. Sasa bidhaa kama hizi uharibifu wake utakuaje.

Jengine Mhe. Spika, moja katika kazi zinazoangaliwa ni kuwa kwenye viwanda vyetu utengenezaji wa bidhaa pia unaangalia mazingira, yaani kuwe kunatolewa bidhaa na mazingira yanaangaliwa kuwa hayaharibiki.

Mhe. Spika, tuna viwanda. Kwa mfano kama Kiwanda cha Mpira kilichoko Pemba na Kiwanda cha Makonyo. Kiwanda cha Mpira kinatengeneza mpira lakini matokeo yake kinatoa harufu ambayo ukipita pale basi unahisi hasa kuwa inaleta athari. Maeneo yale kuna watu wanaishi na utengenezaji wa kiwanda ni kutoa harufu zile, sasa sijui kiwanda kama hiki na kile cha makonyo ambacho sasa moshi wake unaotoka basi unawakera sana wale majirani wa eneo lile. Je, kutafanywa rai gani ili kiwanda kiendelee kwa maslahi yetu, lakini pia na mazingira yawe safi.

Mhe. Spika, la mwisho kwa sababu sitaki nichangie sana ni kuwa kuna uagiziaji wa wanyama kwa ajili ya kitoweo na wanyama hawa wanatoka nje ya Zanzibar. Kwa utaratibu chakula chochote kiwe ni wanyama na kiwe matunda kinapotoka nchi za nje na kuingia nchini kwetu, basi inabidi kifanyiwe utafiti wa hali ya juu. Kwa bahati mbaya Zanzibar ilivyo, sio wote wanaotumia bandari zetu za kudumu kwa kuleta bidhaa zao, wengine wanapita katika njia ambazo sizo na bidhaa zile zinaingia na kutumika.

Kwa zile bidhaa zinazokuja kwa njia za uchochoroni, sijui Mhe. Spika, ni utaratibu gani utakaowekwa kwa ajili ya kuelimisha jamii ili tuone kuwa kila kinachoingia, kinaingia kinachunguzwa na kinakuwa na haki ya kutumika kwa kukamilisha hivyo viwango vinavyohitajika. Vile vile kuepukana na maradhi, kama chakula hicho kilikuwa na maradhi yoyote ya kuambukiza basi kisije kikasababisha au kikaleta maradhi hayo huku kinakoletwa.

Mhe. Spika, nchi yetu ya Zanzibar inaingia katika soko huria la Afrika ya Mashariki na tunatarajia kuagiza na kusafirisha. Kwa hizi bidhaa zetu ambazo zitakuwa zinasafirishwa, ninataka kujua, kutakuwa na utaratibu gani hasa kwa sababu hilo suala limo katika matayarisho karibu litaanza na hii sheria bado pamoja na mazingira yake haijakamilika. Je, itakuwa katika utaratibu gani wa kuona kuwa na sisi tunasafirisha na bidhaa tutakazosafirisha ni zile ambazo zina viwango kamili. Je, tutashirikiana na TBS au tutasubiri mpaka ZBS itakapofanya kazi.

Mhe. Spika, michango yangu mingi ilikuwa ni maswali, naomba kumalizia hapa, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, awali ya yote niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai. Vile vile nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu.

Aidha, kwa vile ni mara yangu ya mwanzo kusimama hapa, naomba uniruhusu niwapongeze vingozi wetu Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa kwake.

Vile vile niwapongeze na wasaidizi wake Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais kwa kuchaguliwa kwao. Ni imani yangu kwamba watamsaidia vizuri Rais wetu.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Dk. Aman Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kutuunganisha Wazanzibari mpaka imefikia leo hii tuko wamoja na tuko hapa kwa nia moja.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa nije moja kwa moja kwenye kuchangia hoja iliopo mbele yetu. Mimi nitaanza na bidhaa kutoka nje. Kwanza naishukuru serikali kwa kutuletea mswada huu kwa sababu tatizo la ubora wa viwango ni kubwa sana kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa hivi ninavyosema katika visiwa vyetu kumekuwa na uingizaji mkubwa wa bidhaa zisizokuwa na viwango ambavyo vimekuwa ni usumbufu, sio kwa watumiaji tu bali hata kwa sisi wakaazi wa visiwa hivi. Mhe. Spika, kumekuwa na mrundikano wa biashara zisizo na viwango kama mabaiskeli mabovu, mafriji na matelevisheni. Hali ambayo visiwa vyetu vimepelekewa kama ni jalala la kutupiwa bidhaa chakavu.

Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba mswada huu utatusaidia katika kuondosha usufumbu mkubwa kwenye utekelezaji wake. Kwa hivyo, matarajio yangu ni kwamba mswada huu utaondosha kabisa dhiki hii pamoja na kuwabana wafanyabiashara walete biashara zenye viwango, pia kuondosha biashara ambazo hazina viwango.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu naomba sasa niende moja kwa moja kwenye suala la chakula na madawa. Kwa kweli kutokuwepo kwa Sheria ya Viwango kumesababisha wimbi kubwa la kuingia vyakula visivyo na viwango. Suala hili limekuwa ni tishio kwa wananchi wa Zanzibar kwa kuhofia afya zao.

Kwa upande wa madawa ni tatizo zaidi, kwani hakuna utaratibu wa wazi unaochukuliwa kupitia maduka ya madawa kwa ajili ya kukagua dawa zisizo na kiwango na zile zilizomaliza muda wake. (Makofi)

Kwa hivyo, matarajio yangu ni kuwa mswada huu utatukomboa kutokana na jinamizi tulilonalo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naunga mkono hoja. (Makofi)

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi hii kuweza kuchangia mswada uliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kunukuu kifungu cha 13 (5) kama hivi ifuatavyo:-

Kifungu cha 13 (5)	"Taasisi inaweza kufuta au kuzuia leseni yoyote iliyotolewa chini ya kifungu hiki au kubadilisha masharti ya leseni hiyo".

Sheria hii haikuweka vigezo vinavyowezesha taasisi kufuta, kuzuia au kubadilisha leseni, isipokuwa imesema tu taasisi inao uwezo wa kufanya hayo.

Sasa Mhe. Spika, kwa sababu nchi yetu inaendeshwa kwa misingi ya sheria na utawala bora, ingekuwa vyema na sahihi na mimi ningekubaliana moja kwa moja na kifungu hiki kama ingetaja vigezo au mambo ambayo yatawezesha taasisi kufuta, kuzuia au kubadilisha leseni.

Lakini kwa namna kifungu kilivyo basi ni wazi uwezo huo unaweza kutumika vibaya na kuathiri wananchi wetu ama wafanyabiashara na hata taifa kwa jumla. Kwa hivyo, ni lazima kuwe na vigezo maalum vya kuweza kufutiwa ama kubadilisha leseni.

Mhe. Spika, serikali yetu ya Awamu ya Saba imeleta jambo zuri sana kwa kuweka ubora wa viwango vya biashara. Lakini tukiangalia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamezungumza vizuri na Mwenyezi Mungu akitujaalia mswada huu utapita na hatimaye kuwa sheria, basi ni vyema kusimamia kwa wale wahusika, kwani bila ya usimamizi mzuri mambo yote haya hayawezi kufanikiwa.

Kwa kweli nasema hivyo kwa maana, kwa mfano wetu Tanzania Bara wao wanalo Shirika la Viwango *(Tanzania Bureau Standard)*. Mhe. Mjumbe mwenzangu hapa Mhe. Salim Abdalla Hamad aliwasifu sana hapa, lakini kuna mambo mengine bado si mazuri. Kwa mfano, tukiangalia Soko la Samaki la Feri ni la kimataifa na biashara ya samaki walaji au wateja wake ni wengi, lakini Wallahi nasubutu kusema katika sehemu inayouzwa samaki wabovu inaongoza.

Kwa hivyo, ndio maana nikasema kwamba lazima mswada utakapopita na hatimaye kuwa sheria, basi yote haya yatafanikiwa kwa usimamizi mzuri ambao utatuweka katika pahala pazuri na kupata ubora wa viwango.

Mhe. Spika, kwa haya machache naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kufika hapa. Pili nakushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii adhimu. Tatu namshukuru Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein pamoja na viongozi wetu wote wakubwa kwa kukaa na kupanga kwa kutuunganisha hapa sote kuwa kitu kimoja, yaani kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. (Makofi)

Viongozi wenyewe ni Mhe. Rais Mstaafu Dkt. Amani Abeid Karume na Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad kwa kutufikisha hapa na kuwa kitu kimoja, kwa kweli humjui nani CUF wala CCM, yaani sote ni kitu kimoja na Mwenyezi Mungu atupeleke salama. (*Makofi*)

Vile vile naunga mkono hoja hii ya serikali. Kwa kweli mswada huu ni mzuri, lakini ili ubaki na uzuri wake basi ninaomba kiongozi kutoka ngazi yoyote na kuweka kifua kwa mtu yeyote ambaye atakwenda kinyume na sheria hii baada ya kupita, nadhani ni vyema ichukuliwe nidhamu haraka sana ipaswavyo.

Mhe. Spika, kwa mfano bidhaa haifai basi iharibiwe na tuhakikishe au tushuhudie kwamba imeharibiwa au imechomwa na kila mmoja afahamu hali hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa haya machache naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moaj. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya jioni ya kuweza kuchangia kidogo pamoja na kumpongeza Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Spika, tunajadili Mswada wa Sheria ya Viwango naomba kutoa taarifa tu kwamba mswada huu wa sheria unakwenda sambamba kikazi na Sheria ambayo tunayo sasa ya *Food, Drugs and Cosmetic*s na viwango hivi vinavyotajariwa kuwepo vitakuwa haviendi kwenye chakula tu, lakini hata kwenye urembo wa akinamama na akinababa. (*Makofi*)

Moja miongoni mwa matatizo ambayo yaliyokuwa yakipatikana ni kwamba hata ule urembo wa akinamama wakati mwengine unahatarisha hata kuchubua nyuso zao, kwa sababu ya kukosa viwango na mara nyengine huwa

wanaambiwa kuwa hiyo si nzuri, lakini tunajua mapenzi. Kwa hivyo, urembo pia una matatizo yake. (*Makofi*)

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumzia tumekuwa na tatizo kama walivyosema baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe hapa, kwamba tunakuwa na sheria lakini hatuzisimamii ipasavyo au pengine tukizisimamia malalamiko ya wale wanaochukuliwa hatua huwa wana *godfathers* na mara nyengine inakuwa tabu.

Hapa mkono ninayo sheria ambayo tayari ina viwango kamili *Caption 78* ya mwaka 1956 na mpaka sasa ninavyofahamu bado haijafutwa hii. Mhe. Spika, kwa kweli humu ndani mpaka yale maziwa yanatakiwa yawe kiwango gani basi yametajwa, yaani sio maziwa ya ng'ombe tu lakini yawe na fate kiasi hiki, mchele, maharage, chizz na hata kile cha kuwekea *preservative*, yaani unachokifanya kitu kisioze pia kimewekwa kwamba uweke kiasi gani. Sasa sheria hizi taratibu zimepotea na wala si kwa sababu hazikuwepo, isipokuwa usimamizi wetu hauna nguvu.

Kwa hivyo, hivi sasa nategemea Sheria ya Chakula na hii ya Viwango zikiunganishwa pamoja, basi huko tunakokwenda kutakuwa na nusra na wananchi wetu watasalimika na matatizo tuliyonayo sasa.

Mhe. Spika, kwa taarifa yako kwa kitu kisichopendeza hivi karibuni nimesikia tumemkamata mtu anapika supu ya pweza na kuongeza Viagra. Kwa kweli ni hatari kiasi hicho watu anaona wanakunywa supu ya pweza kumbe wanakula na sumu ya *Viagra*. (*Makofi*)

Hali hiyo, ni kutokana na usimamizi wa shughuli hizi tumeuregezea kamba na wengi wamepata kupenya na kufanya yale mambo ambayo hayaelekei.

Mhe. Spika, siku moja nilikwenda kumtembelea Mhe. Salim Mzee aliniambia zamani yule anayekwenda na kuchunguza virusi kwenye mitungi ya maji katika mitaa akiogopwa kuliko *Inspector* wa Polisi. Kwa hivyo, watu walikuwa wakisikia anapita walioko nyumbani wanatetemeka, kwamba maji umeyaweka na kuonekana na viluwiluwi vya mbu ni kosa na unatiwa adabu inayostahiki tena alikuwa akitisha mpaka walikuwa wakimwita jina la kuchokoza.

Kwa kweli hawa si kwamba walikuwa watu wa ajabu, walikuwa ni Wazanzibari hawa, yaani ndio sisi, lakini hivi sasa sisi wenyewe ndio tunaofuga mbu kwenye vitalu vya nyumba zetu. Kwa maana hiyo, yote haya yametokea kwa sababu sheria zetu tumeacha kuzisimamia vizuri.

Kutokana na hali hiyo, ninampongeza Mhe. Waziri kwa kuuleta mswada huu wa sheria. Pamoja na hayo, wakati Waheshimiwa Wajumbe wanachangia wametaja hapa suala la Mkemia Mkuu nadhani ni Mhe. Ali Abdalla Ali kama sikosei ndiye aliyesema, kwamba tunaye Mkemia Mkuu na pale anapokaa si pazuri.

Vile vile tufahamu kwamba hata sheria ya kumsimamia yule Mkemia Mkuu hatuna, kwa hiyo anaweza kusema hata hivyo vitu vyako ulivyovileta kwa ajili ya kupimwa ni vibaya, isipokuwa sheria inayomsaidia Mkemia Mkuu ni Sheria ya Chakula na Madawa ndiyo ametajwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba wizara yangu hivi sasa inashughulikia kutayarisha mswada huu na tunategemea kama kila kitu kitakwenda vizuri, basi kikao kijacho cha mwezi wa April tutauleta mswada huu, ili Mkemia wetu awe na nguvu za kisheria pale anaposimama kuyasema yale ambayo si mazuri. (*Makofi*)

Hata hivyo, kuna sheria muhimu ambayo nayo ni vyema tuitayarishe kwa Lugha ya Kiswahili hatuna maneno mawili, madawa na chemicals, yaani dawa tunaita *drugs* na *chemicals* kwa Lugha ya Kiingereza ni kitu chengine. Lakini kuna Sheria ya Madawa na hapa yanaingia madawa hapa yanayofanyiwa sabuni pamoja na yanayotumika kwenye viwanda mbali mbali ambayo hayana viwango na yanaingiwa na hatuwezi kuyachunguza au kuyasimamia kisheria.

Mhe. Spika, kwa mfano juzi nilikuwa nikitizama taarifa ya habari nadhani ni Kinondoni pale kwa wale wenzangu walioiona, basi kuna jamaa amechukua packet ya mtu ambaye anazalisha vitu Mombasa na kuchukua label, siku hizi computer unaweza kufanya kitu chochote. Kwa hivyo, akachukue label na kujifungia nyumbani kwake na kutizama zile dawa wanazochanganya, basi anauza sabuni hizo katika mazingira ya ajabu, yaani anatia label kwamba sabuni inaonekana inatoka Mombasa kumbe vile inatoka Kinondoni.

Kwa kweli ni hatari Mhe. Spika, katika hali kama hii kukosa viwango. Kwa hiyo, nategemea mswada wa sheria aliouleta Mhe. Waziri utatusaidia sana katika kuondoa matatizo haya pale utakapopita na kuwa sheria.

Pamoja na hayo, napenda kuwashauri viongozi wenzangu kwamba tunahitaji kushirikiana sana katika kusimamia matatizo haya. Pengine ni kweli watu maradhi wanayoyapata sasa ni kwa sababu ya vyakula vibovu na hii ni dhana. Sasa tuone kama tukivizuia hali ya afya zetu zitabadilika na sisi Wizara ya Afya tutanusurika kutibu watu wengi zaidi kuliko vile inavyostahiki.

Kwa maana hiyo, napenda kumwambia Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba nitashirikiana naye kwa ajili ya kusimamia sheria hizi. Hivi juzi tu napenda Waheshimiwa Wajumbe wafahamu kwamba mimi na yeye tuliposikia kuna matatizo ya mchele mbovu basi tulikwenda mpaka madukani mule mnamouzwa, kwa lengo la kuhakikisha. Kwa hivyo, sasa tumewaambia wafanyabiashara kuwa hatuwezi kumuachia mtu kuleta vyakula vibovu eti hakuna usimamizi.

Kwa kweli tulikwenda na kusachi na kuhakikisha kwamba ni kweli suala linaloelezwa na wananchi na tukakubaliana mimi na Mhe. Waziri na kwa bahati nzuri sote vijana kuwa tukisikia meli yoyote hatutoacha watu wetu, yaani watendaji wafanyakazi yao, lakini pamoja na sisi tutahakikisha tunafika pale kwa lengo la kudhibiti na kupata sifa tunayostahiki. (Makofi)

Mhe. Spika, kuna wakati fulani nilikuwa Katibu Mkuu Biashara na sote tunajua kwamba ilikuwa dunia nzima karafuu ya Zanzibar ndiyo yenye sifa kwa zile sigara zinazofanywa kule Indonesia. Sasa baada ya kujulikana kuwa karafuu zetu ndizo zenye sifa na karafuu zetu zilikuwa zikipakiwa kwenye magunia na kuandishwa ZSTC, yaani yale magunia yalikuwa yakibandikwa bamba la ZSTC from Zanzibar.

Sasa kulikuwa na jamaa pale Singapore na wala si vizuri kuwataja maana ni watu na biashara zao, walikuwa wakifanyisha yale magunia na kuyapiga muhuri wa ZSTC na kuchukua karafuu za Brazil pamoja na Malagasy sasa kama ni *three by two au three by three* zinatiwa kidogo za Zanzibar zinajazwa na kuuzwa Indonesia eti zinatoka Zanzibar.

Matokeo yake mnafahamu kwamba sasa tumepoteza soko hilo duniani, bila ya shaka na uzalishaji umeongezeka, lakini moja miongoni mwa mambo yaliyotupotezea soko ni hizi counter free zinazofanyika.

Kwa hivyo, ni muhimu sana kuwa na vipimo vyetu pamoja na standard yetu na kuweza kuitetea na kuwa na hakika ya kumshtaki yeyote yule ambaye anakwenda kinyume na sheria zetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono waraka huu na ninategemea Baraza litaupitisha. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu.
Mchango wangu utakuwa katika maeneo mawili matatu. Kwa kuanzia mchango wangu niende kwenye kifungu cha 6 kihusu uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa hii taasisi.

Mhe. Spika, naomba kushauri hapa kidogo kuhusu sifa za Mkurugenzi, yaani awe na sifa za kuwa Mkemia ingawa zimeandikwa kwamba awe na taaluma ya shahada ya pili ya fani ya uongozi na biashara, pia awe na uzoefu wa kazi angalau miaka mitano katika masuala ya viwango au uhakiki wa ubora, biashara na uongozi wa viwanda. Lakini mimi ninaomba awe na sifa ya ziada, yaani anafaa kuwa Mkemia, labda nahisi ingelingana na hii kazi ambayo anakwenda kuifanya.

Vile vile kwenye kifungu cha 8 (6) kuhusu sifa za Mwanasheria kuwa Katibu. Sasa hizi sifa hazikuelezwa wazi Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 8 (6) kinasema hivi:-

> "Bodi itateua mwanasheria mwenye sifa kuwa Katibu wa Bodi."

Sasa zile sifa zenye za uwanasheria hazikuainishwa kama vile awe na uzoefu wa miaka mingapi na mambo mengine kama hayo. Kwa hivyo, ninaomba hapa tuelezwe au zielezwe wazi sifa zake, yaani baada ya kuwa mwanasheria awe na sifa nyengine za ziada, kwa sababu mwanasheria inawezekana ametoke chuoni jana na kuitwa mwanasheria, lakini ule uzoefu wake haukuoneshwa hapa, basi naomba hili lifanyiwe marekebisho hapa.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye kifungu cha 14 kuhusu mambo ya Rufaa, Mhe. Spika naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 14 (1) "Mtu yeyote atakayekuwa hakuridhika na:-

(a) kukataliwa kupewa leseni na taasisi; au
(b) masharti yoyote yaliyowekwa katika leseni au
(c) kubadilishwa masharti kufutwa au kuzuiwa kwa leseni, anaweza ndani ya kipindi cha siku kumi na nne baada ya kupokea taarifa kujuulishwa juu ya jambo hilo, kukata rufaa kwa maandishi kwa waziri ambaye naye ndani ya kipindi cha siku 30 anaweza kutengua au kubadilisha uamuzi utaolalamikiwa".

Mhe. Spika, mamlaka makubwa hapa naona atakuwa amepewa waziri. Kutokana na hali hiyo, ninashauri kwanza kingeundwa chombo cha kukata

rufaa kabla ya kufika kwa waziri, yaani kiwepo chombo cha kukata rufaa ambaye hakuridhika na maamuzi ya wale watendaji, basi awe analalamika kwa kile chombo badala ya kwenda kulalamika kwa waziri, anaona tukimuachia waziri mambo haya yote nadhani itakuwa tumempa mamlaka makubwa sana ya kiutendaji.

Pia kwenye kifungu cha 19 Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 19 "Kwa mujibu wa masharti ya sheria hii, endapo kiwango cha bidhaa kimejaribiwa au kimechunguzwa na kugundulika kuwa hakifanani na kiwango kinachohitajika, bidhaa hiyo ama itarudishwa inapotoka au haitotolewa kwa matumizi na itaharibiwa kama taasisi itakavyoamua."

Mhe. Spika, ninashauri hili suala la kurejeshwa inakotoka lisikuwepo, isipokuwa iharibiwe tu ile bidhaa moja kwa moja, kwa sababu kurejesha kuna watu wajanja wanaweza kusema kwamba inarudi na baadae kurejeshwa kwa mlango wa nyuma na kurudi tena hapa na kutumika. Kwa hivyo, jambo la msingi ni kuharibiwa tu na wala sio kurejeshwa. (Makofi)

Pamoja na hayo, ninaushauri kidogo kuhusiana na bidhaa hasa zile ambazo zinazalishwa hapa Zanzibar. Kwa mfano, spices na mambo mengine kwenye huu uuzaji wa nje, wakati tutakapokuwa tumegonga muhuri wetu wa Zanzibar Bureau Standard (ZBS) kupeleka nje.

Sasa tukiangalia nje ya mipaka yetu Zanzibar inajulikana kwa mwemvuli wa Jamhuri ya Muungano. Je, hatutokuwa na migongano na watu wa *Tanzania Bureau Standard (TBS),* kwa sababu kule nje watakuwa wanaifahamu *Tanzania Bureau Standard (TBS)* na wala sio Zanzibar Bureau Standard (ZBS). Kwa hivyo, katika hili namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie kidogo, ili tuweze kupata ufafanuzi juu ya suala hili.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkwajuni naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, kwanza sinabudi kumshukuru Allah (*Subuhanahu Wataalla)* kwa kutuwezesha kufika katika Baraza hili tukufu kwa muda huu. Pili nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu kwenye Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu ambao tokea asubuhi wanasimama hapa kwa ajili ya kuelezea suala hili la uwekaji wa viwango wa bidhaa. Kwa kweli wenzangu wengi tayari wamekwisha kuzungumza mengi, isipokuwa mimi nitazungumzia zaidi kwenye bidhaa zinazoingia ambazo ni *recondition au used*.

Nadhani wenzangu hawajagundua kwamba hizi used na hasa mafriji na televisheni zinakuwa zinaingia na wadudu ambao wanamfano wa mende. Sasa tukiangalia hapa Zanziba hivi sasa wameshaenea, ambao hawa watakuwa si mende walioko katika nchi yetu na sisi tumewazoea wale mende wakubwa wanazo athari, lakini niseme hawa ni vyema Mhe. Waziri kufanya utafiti kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Afya kwa ajili ya kuwachunguza wadudu hawa ambao wanazaliana haraka sana.

Kwa kweli wadudu hawa kwa haraka nimeona kama wanasababisha maradhi ya ngozi, huko wanakotokea wanasema wenyewe hasa ikiwa wadudu hawa watavamia kwenye nyumba basi kwa wale waliokuwa wako chini ya uangalizi wa serikali huwa wanahamishwa nyumba.

Kutokana na hali hiyo, nafikiri ni vyema wadudu hawa kufanyiwa utafiti zaidi, kwa sababu tunasema bidhaa hizi zinatusaidia sote. Kwa mfano, hata mimi mwenye binafsi wakati ninapokuta kitu kizuri ambacho nimekipenda basi ninakinunua na wengine pia.

Vile vile katika suala la mitumba kuna wanachama wa biashara hizi kabla ya kufunguliwa basi kuna kuwa na suti nzuri, naweza kusema kwamba sote tunatumia. Kwa hivyo, Inshaallah Mhe. Waziri afanye utafiti kwanza kuhusiana na hawa wadudu ambao wanaingia na hatujui athari zake zaidi ni ipi.

Mhe. Spika, nije kwenye kuchunguza ubora wa viwango kama alivyosema Mhe. Waziri wa Afya kuhusu vipodozi, wanawake wanaelekea sena huko kwa hivyo pia navyo vichunguzwe ubora wake.

Mhe. Spika, na mimi naungana na wenzangu naunga mkono mswada huu mia kwa mia kwa niaba ya wananchi wangu, pamoja na walionichagua kuingia katika Baraza hili tukufu. Ahsante sana (Makofi)

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii tukiwa hapa wenye afya njema. Pili nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuchangia .

Mhe. Spika, Serikali itaanzisha haraka taasisi hiyo ya ubora wa bidhaa ili ziwe za viwango bora, je tukianzisha taasisi hii sheria ya kumlinda mlaji itafutwa. Serikali iwe makini na wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa ambazo ziko chini ya kiwango, mtu ambae atakutwa na bidhaa mbovu asiachiwe mwenyewe kuziharibu hizo bidhaa bali serikali ichome moto kwa gharama za mletaji.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana (Makofi)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ili kutoa mchango mfupi sana kwa mswada huu wa Mhe. Waziri kwa ajili ya kumsaidia malengo yake ya kuweka viwango hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa uamuzi wake sasa kuja na mswada huu kwa lengo la kuwaokoa Wazanzibari, niseme kamba maamuzi ya serikali kuunda ZBS hapa Zanzibar ni maamuzi muafaka na yatasaidia serikali hii na wananchi wake kuepukana na magonjwa ambayo nadhani yanasababishwa na vyakula ambavyo havina sifa.

Mhe. Spika, kwanza mimi nianze kwa kumuunga mkono Mhe. Mtando kwamba si vyema wala haipendezi bidhaa iliyogundulika na hapa Zanzibar kwamba haina kiwango ikaamuliwa kurejeshwa kule inakotoka, serikali ikigundua kwamba bidhaa hii haina viwango ichomwe moto hadharani na isipewe nafasi hata dakika mbili, kwa sababu wafanya biashara ni wajanja na sisi Zanzibar tuko kwenye visiwa. Kwa hivyo ukimruhusu mtu arejeshe maana yake unamwambia apeleke Pemba kama kipo Unguja na kama kipo Pemba basi unamwambia azungurushe kwa Makunduchi alete Unguja. Kwa hivyo mimi nasema kwamba bidhaa ambazo hazina viwango ziwekwe moto hadharani bila ya kuoneana haya, huo ndio utawala bora na uwajibikaji katika serikali.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningeligusia ni kwamba ningemuuliza Mhe. Waziri kwamba hii ZBS itakuwa na maabara ya kugundua kwamba bidhaa hivi zina iwango au tunategemea maabara ile ya Mkemia Mkuu, kama tunategemea maabara ya Mkemia Mkuu maana yake tuongeze nguvu mara mbili. Kuboresha afisi hii kwa maana ya kuwapa uwezo wa kitaalam na uwezo wa kifedha ili waweze kushughulikia mambo mbali mbali hapa Zanzibar, tukitegemea maabara hii maana yake hivi sasa ilivyo japo kwamba Mhe. Waziri wa Afya ana nia safi ya kurekebisha maabara hii ya Mkemia Mkuu lakini kachelewa sana kufika. Sasa kama ni kutegemea maabara hii ya Mkemia Mkuu iliyopo Zanzibar basi ni kwamba serikali ijipange kuongeza uwezo maradugu kwa ajili ya kuwaka ufanisi.

Jengine ambalo ningeligusia ni suala zima la kuweka maghala, tatizo ambalo linatokezea hapa ni kwamba tunategemea maghala ya wafanyabiashara,

Serikali haina maghala katika bandari wala haina maghala katika viwanja vya ndege. Kwa hivyo mfanya biashara tunamruhusu alete mzigo wake mpaka Mombasa pengine keshokutwa ndio ukafanye ukaguzi, lazima serikali ijenge maghala yake katika viwanja vya ndege na bandari na hapo mzigo ukifika lazima uingizwe mle na ufanywe ukaguzi kabla ya kupelekwa kwenye maghala ya wafanya biashara, vyenginevyo ukitwambia kwamba mfanya biashara alete mzigo wake uende kwenye ghala Mombasa au kwa Mchina baadae ndio taasisi yako ifanye ukaguzi huo ni mchezo wa kiini macho.

Mhe. Spika, ushauri wangi ni kuwa serikali iamue sasa kujenga maghala ya kutosha katika maeneo zetu za Unguja na Pemba ili mzigo ukifika kwanza ukaguliwe kabla ya kuingia kwenye soko la wananchi, vyenginevyo kazi ambayo tunafanya hapa itakuwa haina maana kubwa. Kwa hivyo namshauri Mhe. Waziri kwamba kama tumedhamiria kudhibiti viwango vya bidhaa zetu lazima wajenge maghala ya kutosha ya serikali ili mzigo mwanzo uingie kwanye maghala yale ukaguliwe ndio baadae upelekwenye maghala ya watu binafsi.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ningeligusia haraka haraka humu tumeona kwamba bodi itajipangia kwenye kifungu cha 7 ukurasa wa 187. Kwamba bodi itaajiri wafanyakazi kama inavyoona inafaa na itajipangia naomba kunukuu.

“Taasisi kutoka katika mfuko wa fedha inaweza kupanga utaratibu wa mafunzo kwa wafanyakazi wake na mambo mengine yanayohusiana na hayo kama inavyoona inafaa katika utekelezaji wa kazi zake”.

Mhe. Spika, mtu ukishampa ajipangie mwenyewe kujipatia mafunzo na mambo mengine kama anavyoona mwenyewe inafaa nadhani tunataka kuwapa bodi badala ya kufanya viwango ni kufanya hii taaluma ya mafunzo tu, tutakapowajengea bodi na fedha kwa ajili ya kuwafundisha tu usiku na mchana, nani anayekataa semina usiku na mchana. Kwa hivyo hapa nadhani tuangalie kwa makini tusiwape mwanya kwamba wajipangie mafuzo kama wanavyoona wao inafaa, mimi ukinambia unifunze kwa semina niko tayari siku arubaini zote unifunzo, kwa sababu mafunzo yana afaida zake na kuna kitu ambacho kinaingia.

Sasa tusitoe mwanya kwamba mtu ajipangie mwenyewe kujifunza lazima tudhibiti utaratibu mzuri wa matumizi ya fedha za umma tudhibiti tusimpe mwanya mtu ajajipangia, ukimwambia Mkurugenzi panga semina zako kama vile unavyopenda basi atajipangia atakavyo na itakuwa kazi ni hiyo kujipangia semina tu hakuna kazi ambayo tunalenga. Mhe. Waziri nakushauri hapo uzingatie na tuwe makini katika utekelezaji.

Mwisho Mhe. Spika, nimuunge mkono Mhe. Fatma kwamba tumekuwa na soko la bidhaa za mafriji, mafriza pamoja na TV sasa nadhani kuna haja ya kuwa na ghala maalum la serikali, kwamba mafriza yale yanapoingia kwanza yakaguliwe lakini ukitoa mwanya kwamba mafriza yale na TV zisambae tu Zan zibar hatimae Zanzibar itakosa jaa la kutupia mafriji yale na TV. Kwa hivyo viwango vya vitu vile nadhani vingedhibitiwa Zanzibar sasa hivi imekuwa na wimbi kubwa la uingizaji wa vifaa vile kwa maana ya urahisi au kwa sababu ni jaa, lakini lazima tudhibiti hali ile tusise rahisi kwa sababu ya unyonge wetu na umasikini wetu kupokea kila mzigo unaotoka nje, sasa hivi Zanzibar imeingia vifaa kutoka nje hata majina havina. Kwa hivyo tudhibiti kwa malahi ya Afya na mazingira ya hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu hayo naunga mkono hoja hii.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa jioni hii ya leo kuchangia mswada huu wa viwango vya biashara. Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii ya leo na mimi kuniwezesha kusimama nikatoa mchango wangu.

Pili nakushukuru na wewe kuchaguliwa tena kutuongoa katika Baraza hili la Wawakilishi, naomba Mwenyezi Mungu akupe hekima na busara ili uendelee kutuongoza katika kipindi hichi tulichonacho. Tatu nawashukuru wananchi wa jimbo langu la Micheweni kwa kunichagua tena kuwa Muwakilishi wao na leo hii nimesimama hapa kuendelea kuwawakilisha wao.

Mhe. Spika, pia na mshukuru Mhe. Wasiri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kutuletea mswada huu ambao ameuleta mahala ndipo, kwa kweli mswada huu alioleta ni roho ya wananchi wetu wa Zanzibar na wao wanausubiri kwa hamu mswada huu na wanatusikiliza kwa hamu kubwa sana. Mhe. Spika, suala la viwango ni suala ambalo kuwa limetugusa sana kwa sababu Zanzibar bidhaa zinazoingizwa havina viwango, kwa bahati mbaya ilikuwa hatuna chombo cha kuangalia hivi viwango vya biashara hivi zinazoletwa.

Mhe. Spika, naiomba serikali mswada huu inaouleta basi ishaalla kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ukishapitishwa na kuwa sheria basi namuomba Mhe. Waziri kama alivyosema Mhe. Waziri wa Afya kwamba wao wanakwenda madukani wenyewe kuangalia sasa hivi basi naomba isimamie kwa dhati kabisa kwani tnapitisha sheria lakini hatzisimamii. Kwa hivyo hili naomba lisimamiwe kwa dhati kabisa kwa sababu bidhaa zinazoletwa ni bidhaa ambazo zinaletwa zinakuwa ni mbovu na vinatuathiri tulio wengi na wananchi wetu wanaathirika kwa bidhaa hizi.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri asimamie kwa dhati kabisa lakini wakati huo huo hichi chombo ambacho kitakuwa kinasimamia hizi bidhaa ambao ni ZBS naomba wapewe vifaa vya kisasa ambavyo vitawafanya kusimamia kwa dhati na waone kwamba kweli hizi bidhaa zinazoletwa zina uhakika na ndizo zinazofaa kwa binaadam, kwa sababu kama hawana chombo watakwenda kwa kubahatisha na kama watakwenda kwa kubahatisha mwisho wake utakuja ule ule.

Mhe. Spika, halafu niungane na wenzangu kwamba endapo mtu atakamatwa na hizi bidhaa ambazokuwa hazifai basi lisiwepo hili suala la kuwa zirudishwe, lakini ziteketezwe kwa sababu unapomwambia mtu arudishe harudishi anapita mlango wa nyuma yanakwenda kubadilishwa mapolo tayari wananchi wanakuja kupewa tena wanakula.

Mhe. Spika, karibuni Mhe. Waziri wa Bishara, Viwanda na Masoko alitangaza kwamba umeletwa mchele mbovu na tayari ukaambiwa urudishwe kwao Pakistan, lakini uvumi uliokuweko kwa wananchi wetu sina uhakika kama ni kweli au uvumi, lakini uvumi uliokuweko ni kwamba bidhaa ile ilirudishwa mpaka Kenya na Kenya ikapakiwa tena ikaletwa Pemba lakini imebadilishwa vipolo tu. Mchele ule unasemakana umeliwa Pemba .

Kwa hivyo Mhe. Spika, mtu kama amekamatwa na bidhaa mbovu ukamwambia airudishe hairudishi kabisa atazunguruka na kwenda kubadilisha mapolo tayari unaletwa tena unakuja kuliwa, kwa hivyo kama ni bidhaa ya mchele basi ikikamatwa ni bora iteketezwe na kila mmoja aone kama hii bidhaa kweli imeletwa ni mbovu na imeteketezwa itakuwa ni fundisho kwa mfanya biashara yoyote, mwengine atajua kwamba nikileta bidhaa sio basi itateketezwa kwa hivyo atajua kwamba hii ni hasara yangu. Naomba hili lizingatiwe na asirudishiwe mtu kwamba arudishe yeye mwenyewe.

Mhe. Spika, suala jengine niungane na wenzangu kuhusu bidhaa hizi ambazo kuwa zinaingizwa ambazokuwa na baiskeli, mafriji, mafriza, TV hizi nazo imekuwa sisi Zanzibar kazi yetu ni kukusanya vifaa vibovu, badala yake itakuwa sisi kama ni jaa la kutupia taka taka kwa sababu sasa hivi wenzetu wana vifaa ambavyokuwa havifai sasa hivi, kuna vifaa vya kisasa ambavyo ndivyo vinaingizwa. Sasa sisi wafanyabiashara wetu wanakwenda kuchukua yale yaliyokwishapitwa na muda wanakuja nayo huku wanawaozua wananchi na wao wananchi wanauziwa rahisi wanachukua tu, ni vifaa ambavyo vimeshapitikiwa na muda.

Kwa hivyo mwisho Mhe. Spika, takujakuwa hiyo sehemu ya mwisho ya kutupa hayo makachara tutakuwa hatuna, kwa hivyo na hili nawaomba wahusika hiyo tume ambayokuwa imeundwa ya kuchunguza vifaa ikae pale mili ikiingia

makontenda yakiteremshwa basi wawe wanaangalia hiki kinafaa kupelekwa huku na hiki hakifai.

Mhe. Spika, baada ya mchango huo mfupi naunga mkono hoja mia juu ya mia. (*Makofi*)

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kunijaalia kupata fursa hii ya kuzungumza jioni hii katika Baraza lako tukufu kuchangia hoja juu ya mswada huu ambao tunauongelea tokea asubuhi. Pili nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza, tatu namshukuru he. Waziri kwa kuleta mswada huu ambao kwa kweli kama walivyozungumza waheshimiwa wajumbe tokea asubuhi mpaka jioni hii kwamba ni roho ya viwili wili vyetu watu wa Zanzibar, kwa sababu bidhaa ambazo hazifikii viwango hapana shaka zinaharibu viwili wili vyetu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, sitaki nizungumze kwa urefu sana kwani michangio mingi sana iliyochangiawa hapa ni kuzungumzia ubora wa bidhaa, mimi kwanza namuomba Mhe. Waziri wa Bisahra, Viwanda na Masoko Mhe. Nassor Mazrui yeye kwa vile ni mfanya biashara aonyeshe mfano bora katika biashara zake kutuletea biashara iliyo bora, unapokuwa kiongozi unatakiwa uwe mfano bora kwa unaowaongoza. Kwa hivyo Mhe. Waziri kwa sababu ni mfanya biashara aonyeshe mfano wa bidhaa bora katika bidhaa zake mpya atakazoleta visiwani Zanzibar.

Halafu jambo la pili ambalo napenda kuzungumza tokea asubuhi hilo sijasikia likizungumza lakini mimi nataka nilizungumze hapa, pamoja na biashara kuwa na kiwango na mfanya biashara naye nae afikilie kiwango. Kwa nini nikasema hivyo, kuna wafanya biashara wana maradhi ni wagonjwa wana maradhi ya kuambukiza na hawa wanaweza kuleta bidhaa zikasababisha watumizi kupata maradhi kwa sababu yao, kwa hivyo wafanyiwe uchunguzi wa kutosha mara kwa mara ziangaliwe afya zao ili walete biashara zilizo madhubuti kabisa. Tuna hakika binaadamu kila mmoja na alivyo inawezekana kwamba ana maradhi lakini anajiweza weza lakini maadhi yale inaweza kusababisha kumchangia mwenzake kutokana na biashara yake ambayo amekuja nayo, hili ndilo ambalo na mimi nimesema uwe ni mchango wangu.

Mhe. Spika, kwa haya machache ambayo nimezungumza kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Chambani naiunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana (*Makofi*)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia mswada huu wa sheria, kwanza mimi nikushukuru san asana kutokana na umahiri wako tangu asubuhi mpaka sasa

hivi sijakuona kuinuka hili ni moja kati ya ushujaa wako ambao unakuweka kafika fani nzuri ya kufanya kazi.

Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu ambao kwetu Zanzibar itakuwa ni jambo geni sana, hii ni moja katika tosha ya kumuelewa Mhe.Waziri kwamba ni mbunifu wa mambo ya biashara na hasa alivyoona hali halisi ya kuwa Zanzibar tunaletewa vitu ambavyo havistahiki kama ni wananchi wa Zanzibar kula, siku zote mimi huwa napenda kuzungumza hara Rais anapoteua watu basi ajaribu kuteua watu ambao wanalingana na ile fani ya sehemu yenyewe.

Kwa mfano hapa kama Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mhe. Mahammed Mazurui yeye ni mfanya biashara hakuna asiyamjua katika Zanzibar hii, kwa maana kupata nafasi hii imetusaidia Wazanzibari kuweza kupata mswada kama huu wa kutaka kutuondolea maradhi ya kila siku kutokana na vyakula vibovu na sumu ambazo zinaatiwa huko kwa kukaa muda mwingi katika maghala, lakini wenzetu kule wanaona wapi kwa kupeleka vyakula hivi ni Zanzibar ambao wana njaa zaidi ndio maana tukaleteewa. Lakini Mhe. Waziri ameona suala hili kwa hilo nakuunga mkono kwa jitihada zako na Mungu akusaidie.

Lakini ukurasa wa 190 kuhusu viwango vyenyewe hapa ambavyo vinakusudiwa Mhe. Spika, nakumbuka karibuni hivi kwenye Baraza lako lililopita sifahamu tarehe gani lakini lilikuja suala la mchele mbovu baadhi ya viongozi tulilikataa suala hili tukawa wabishi sana kutokana na ule mchele ambao tulikuwa tunausema hauhalisi kwa binaadamu kuula. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri siku hiyo Mhe. Zahara Ali Hamad aliuleta ukisogea ulipo tu unakwenda chafya kutokana na vumbi na unavyonuka, chakula kile kilimpasa ale binaadam na ndio maana kila siku tuna mpa matatizo Mhe. Naibu Waziri hapa kujibu suala la sukari kumbe mambo mengi yanachangiwa na yale madawa yanayotiwa kwenye chakula kuwekwa ghalani kwa muda mrefu mpaka kuletwa Zanzibar, sasa ile inakuwa imechajifanya sumu ya kumdhuru mtu kwenye tumbo.

Mhe. Spika, mimi sio mtaalam sana kwa mambo ya. biology lakini hiyo ni moja katika uchunguzi wa macho nilichogundua hapa Zanzibar kinachotupa tabu ni hizi kamikali hizi kwa sababu hatupati kile kitu fresh, mfano leo hii twende kwenye mabonde yetu ya mpunga ukilima unavuna na kuutwanga ukitoka pale unaingia kwenye chungu kile ni kitu fresh hakina kemikali kama hivi vitu vyengine vilivyokuja sasa hivi.

Halafu jengine Mhe. Spika, Zanzibar kuna vitu vingi tuna uwezo na sisi kwenda kuvisafirisha nje lakini kwa kuwa hatuna ujuzi tunashindwa, ndio

maana mpaka leo Zanzibar unaingia umasikini lakini tumeona katika maeneo haya Zanzibar tunalima muhogo, muhogo ukiutengeneza ukiwa quality basi mtu wa Dubai anautaka, Uingereza anautaka, Japani anautaka. Lakini kwa kuwa vile vitu hatuna taaluma wa kufanya kiwe na kiwango cha kuweza kusafirisha lakini kama ingekuwa tunayo kabla ya Mhe. Mazrui kutoa mswada huu basi mimi nafikiria muhogo ungekuwa tabu wala usingezagaa kama unavyozagaa sasa hivi, lakini kwa kuwa hiki kitu tayari tunakikusudia hasa kutoa nembo zetu za kuonyesha kwamba Zanzibar na wao wanaweza kupeleka kitu ambacho kule nje kinakubalika.

Mhe. Spika, tuna kazi zetu za mikono wenzetu kila siku zikienda wanatuletea mikoba ambayo hatuna, sisi tuna mikoba yetu ya asili hapa mikoba hiyo ingekuwa tuna nembo kama hii anayoitaka Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko hivi sasa basi naamini kila mwananchi wa Zanzibar angepata ajira yake. Lakini kwa kuwa hatukuwa na taaluma sasa namuomba Mhe. Waziri aiueneze hii taaluma huko chini, sisi sawa ndio tumeshaipata hapa lakini sasa aipeleke huko chini ili wananchi wazidi kupata taaluma hasa kwenye majimbo yetu ili wapate taaluma ya kutengeneza vitu ambavyo bora na kuweza kuuza huko nje.

Mhe. Spika, nchi za nje sasa hivi embe ya Zanzibar ya Muyuni ilikuwa ikisafirishwa lakini inauliwa kutokana na vile wanavyofanya wenzetu wanakuwa wanaiua kwa makusudi kwa kuwa ni nzuri, lakini uzuri wenyewe haikuwa katika ufungaji mzuri wa bidhaa wala haina nembo ya kuonyesha kwamba hili zao linazalishwa sehemu gani, au kutoka kijiji gani kwa sababu kuna vijiji ambavyo vina asili ya kua kutoa mazao ya aina kama hayo. Sasa mimi nafikiria Mhe. Wairi aendelee hivyo hivyo kutuletea miswada kama hii ya kumsaidia Mzanzibari kuweza kupata ajira kwa kupeleka vitu koliti huko.

Laskini nikiingia katika sheria Mhe. Spika, sheria hii ni ndogo tena ndogo sana kwa sababu ninasema ndogo mtu kulipa laki moja hapa mimi kidogo nitakuwa mkali, kwa sababu nimetoa mfano na ndio maana nikaanzia kifungu cha huku kwa kuelekea kunako sheria, hii sheria haikidhi haja kwa sababu nimekupa mifano ya kusema kuwa wanatuletea vyakula vya kutuua sasa mtu kama huyu unamuwekea faini ya laki moja, au kifungo hii sheria naomba tuiangalie tena bado ni nyepesi sana. Kwa sababu unapoweka sheria kali ikawa nzito sidhani kama mtu atakuja kutuletea tena matatizo yale, kwa sababu huyu mtu anatumaliza tena vibaya vibaya kwa sababu yeye haangalii maslahi ya watu anaangalia maslahi yake yeye. Yeye anasema wakinunua sawa, wasiponunua sawa lakini najua watanunua tu ikiwa unga, mchele, sukari sasa suala hili naomba lifikiriwe.

Mhe. Spika, kuhusu habari ya Mchunguzi wa Maabara zetu (Mkemia) nimemsikia Mhe. Waziri anasema kuwa yumo katika kutafuta sheria za kuweza kutusaidia. Hili nakubaliana nalo kwa sababu haya masuala ya kuingiza madawa ya kulevya, mama ya vijana wanasema hupigwa changa la macho hapo hapo. Hebu tuiangalie hii sheria jinsi ambavyo unapokamatwa ule unga mpaka unapomfika yeye.

Kwa sababu unapomfika yeye hapa njiani ndio panapohatari yenyewe. Ukimfika yeye kule tayari kile kitu kimeshabadilishwa na unaambiwa ni jivu. Hili suala kwa kweli tujaribu tuweze kumsaidia hasa hapa katika kuanzia kukamatwa kwake ule unga je, sheria itampa mamlaka ya kuwa kule kulipokamatwa aweze kufatilia na aweze kwenda kuuchukua mwenyewe, hii sheria hebu tuitizame. Au tusubiri awepo kule afisini kwake yeye aanze kuuchunguza kama huu ndio au siyo. Kama ni hivyo kwa kusubiri Afisi kwake hatutokamata watu wanaouza unga. Siku zote hao tutakuwa tunateketeza watu.

Mhe. Spika, ukisema kakamatwa kituoni anangojea muendesha mashtaka auchukue ule unga kwa kwenda kuuhasisi kwa mkemia pale aah! Hili suala Mhe. Spika, kwa kweli bado mimi linanipa mashaka. Mhe. Waziri husika nakuomba uiangalie running yako ya sheria itampa kuweza kwenda kule kwenye kituo chenyewe bila ya kuondoka ule unga. Kama ipo sheria hiyo basi mimi nakuomba kwa ushauri wangu tuifanye hiyo sheria ili auwahi kule fresh kabisa kuliko kuja kwenda zake njiani. Ukija zake njiani utapigwa changa la macho, utaachiwa saruji, ukifika kule unasema huu siunga, kesi hakuna, huku watoto wanateketea.

Hili nalo ningeliomba kuwa sheria Mheshimiwa mnapokuja kutuletea itizamwe kwa makini ili tuweze kukusaidia na kukupa nguvu zaidi. Kwa sababu sasa hivi hali halisi inazidi kuwa mbaya. Vijana wetu wanapukutika kwa hali hiyo.

La mwisho kuhusu hali ya kima mama juu madawa haya ya mchubuko daah! Sheria hii nayo tuiangalie, tuliitunga sheria lakini bado ipo nyepesi. Hali imekuwa ni ngumu sana Mheshimiwa, tunateketeza watu, watu wanapata kensa kutokana na hii hali. Na kwenye Wizara yako ndio imo sheria hiyo, kwa hivyo na hili nalo naomba ulitizame.

Mhe. Spika, kwa kuheshimu wakati wako nauunga mkono Mswada huu pamoja na wananchi wangu wa jimbo la Kitope mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kukutana hapa katika Kikao chetu kujadili Mswada wa sheria uliopo mbele yetu kuhusu viwango.

Mhe. Spika, pili nashukuru kwa kupata nafasi hii na kusema machache juu ya Mswada huu. Kwa kweli Zanzibar katika bidhaa zetu tunazoagizia tupo pabaya sana. tunachokosea kuwa zaidi ya asilimia 50 ya bidhaa zinazoziingia nchini ni bidhaa ambazo hazina viwango, kuanzia za vyakula na hata zile za kutumia tu. Kwa mfano bati, bati unaichana kama unavyochana karatasi, msumari wa kuezekea ukikutana na ubao kidogo tu msumari unapinda. Misumari ya zamani ulikuwa ugonga nyundo inatoka moto lakini msumari haupindi, sasa hivi ukiugusa tu unapinda. Kwa ufupi vifaa vingi vinavyoagizwa ni vifaa ambavyo havina viwango na havifai. Lakini ndio vimo nchini na tunavitumi, tufanye nini? Bati hii unayoichana kama karatasi mwananchi ndio anaona rahisi na ndio anayopenda kuinunua.

Juzi mimi kabla sijaja huku katika vifaa vibovu niliuziwa betri mbovu ya simu, tena nimeuziwa kwa sifa nimeiweka chaji usiku wa kucha masaa sita niliyoelekezwa, nimeitumia siku moja tu. Lakini nilibaini kuwa ni vile vifaa ambavyo toka nyuma tunapiga kelele kuwa vimeingia vifaa feki, sasa watu wanavitoa wanaviuza huko huko mashamba na mimi nikanasa nikanunua moja, chupa za chai. Zamani ukinunua chupa ya chai mfanyabiashara anakupa gerentii anakwambia weka maji moja saa 24 ikiwa imepowa ilete. Leo hakubali kukwambia hivyo, ukiichukua ndio umeichukua, kwa sababu ana hakika nayeye pengine ni mbovu. Sasa ukimrudishia na yeye amrudishie nani.

Kutokana na sheria hii itabidi tuwe makini sana na bidhaa ambazo tunaagizia. Zile bidhaa ambazo zinahitaji kutumiwa na mwanadamu ama kwa kujipodoa au kwa chakula lazima mkemia au anatakayehusikana na usimamizi huu awe ni mtu mwaminifu na muadilifu. Asije akatoa OK kwa kitu fulani kumbe kina kasoro, atakuwa anafanya uhalifu. Ni mtu atosheke, aridhike, awe muadilifu na atutumikie kama vile ambayo inatakiwa akihisi kitu kinafaa atujulishe kinafaa, asimuonee haya mfanyabiashara. Akihisi kwamba hakifai aseme hakifai asiwaonee watumiaji.

Mhe. Spika, Mswada huu pindipo ukipita na sheria itakayotungwa ikisimamiwa kwa kiasi fulani itapunguza vifaa feki au bidhaa ambazo hazina viwango kuingia katika nchi yetu. Lazima wafanyabiashara wawaonee huruma raia wenzao. Mtu anafanya biashara kwa ajili ya kupata faida yake lakini vile vile afanye biashara na mtu vile vile afaidike na biashara atakayonunua. Kwa kweli haitokuwa haki wala si halali kumuuzia mtu kitu leo kesho asubuhi ikawa kitu hicho hakifai tena. Pengine anajua kuwa ni mbovu, hivi bidhaa mbovu zimo tena hapa ndani. Mhe. Waziri vitu hivi vitafanywa nini?

Mara moja kenda kusikiliza redio mwahala mbali mbali kulikuwa kuna bidhaa fulani za viwanda zinatafutwa hapi zitupwe, bidhaa zimeshakuwa mbovu

inakuwa ni mzigo kwa mtu husika kwa vyovyote utakavyoiweka itakuwa inaharibu mazingira ama ardhini au baharini. Na hakuna mtu yeyote aliyekuwa tayari kuharibiwa mazingira ya sehemu yake. Hata sisi kama tukiambua kuviteketeza vyote ambavyo hivi sasa havifai tutaviteketeza wapi na vyengine kama madawa yanakuwa yanasumu. Kwa hivyo vitu vyote vile ambavyo vitabainika kuwa havifai tutafute tufanye nini kwa usalama wa ardhi yetu na sisi wenyewe.

Baada ya kutoa maelezo haya mafupi nami niungane na waliotangulia kuiunga mkono hoja hii. Ahsante.

Mhe: Spika: Nifikiri tumefikia pahala na nimeshauriana na Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake wakanipa taarifa kwamba itamuafaka kwamba wafanye majumuisho kesho. Kwa kuwa hatuna shughuli nyengine baada ya michango tuliyopokea basi nadhani tukapumzike.

Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa mashirikiano makubwa na sasa naahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 25 Januari, 2011 siku ya Jumaane Saa 3:00 za asubuhi.

(*Saa 12:39 Jioni Baraza liliakhirishwa mpaka kesho tarehe 25/01/2011 saa 3:00 asubuhi)*